SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

## RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA TAWALA ZA MIKOA, MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023



SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

## AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

# RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

# KUHUSU UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA TAWALA ZA MIKOA, MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023

**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR**
2 Mtaa wa Tume, S.L.P 258, 71125 Kilimani, Zanzibar
Simu/Nukushi: +255 24 223 400, Barua Pepe: info@ocagz.go.tz
Tovuti: www.ocagz.go.tz

**MAREJEO NAM: CAC.132/385/01/4** **TAREHE: 26 MACHI, 2024**

**MHE. DKT HUSSEIN ALI MWINYI,**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI,**
**AFISI YA RAIS, IKULU,**
**S.L.P. 437,**
**ZANZIBAR, TANZANIA.**

**KUH: KUWASILISHA RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA HESABU ZA TAWALA ZA MIKOA, MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

- - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - -

Ninayo furaha kuwasilisha kwako Ripoti ya Mwaka inayohusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 kwa mujibu wa kifungu nambari 112(5) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na kifungu nambari 46(1) cha Sheria nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023.

Naomba kuwasilisha.

Ahsante.

.............................................
**DKT. OTHMAN ABBAS ALI**
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU**
**WA HESABU ZA SERIKALI**
**ZANZIBAR.**

# AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

## Mamlaka

Kwa mujibu wa kifungu nambari 112 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na kifungu nambari 46(1) cha Sheria nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kikatiba kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa za ukaguzi huo angalau mara moja kila mwaka.

## Dira

Kuwa na Taasisi ya ukaguzi iliyo huru na inayoongoza katika kusimamia uwajibikaji na uwazi.

## Dhamira

Kusimamia uwajibikaji wa Taasisi za umma kwa kufanya ukaguzi wa hesabu wenye kuleta tija na kulihakikishia Taifa kwamba rasilimali za Umma zitatumika kama ilivyokusudiwa.

## MISINGI YA MAADILI YA UKAGUZI

1. **Uaminifu** — Kuhakikisha Afisi ina kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala bora unaozingatia Sheria.
2. **Uadilifu** — Kuwa ni Afisi inayozingatia misingi ya uadilifu kwa kutoa huduma bila ya upendeleo.
3. **Kuwa Huru** — Kuwa ni Afisi iliyo huru na inayotekeleza majukumu yake bila ya kuingiliwa kwa mujibu wa Sheria.
4. **Uwezo na Taaluma ya Ukaguzi** — Kuwa ni Afisi yenye kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora wa kiwango cha juu.
5. **Kutunza Siri** — Kuwa ni Afisi yenye kutunza siri katika utekelezaji wa kazi zake.
6. **Uwazi na Uwajibikaji** — Kutoa taarifa sahihi na muhimu kwa wadau ili kuweza kupima uwajibikaji katika matumizi bora ya rasilimali za Umma

# YALIYOMO

YALIYOMO ........................................ III
ORODHA YA MAJADWELI ........................................ VI
VIFUPISHO ........................................ IX
SHUKURANI ........................................ X
DIBAJI ........................................ XII
MUHTASARI ........................................ XIV
**SURA YA KWANZA** ........................................ XXII
1.0 UTANGULIZI ........................................ 1
1.1 MAJUKUMU YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ......... 1
1.2 UPEO NA MADHUMUNI YA RIPOTI YA UKAGUZI ........................................ 2
1.3 NJIA ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI ........................................ 3
1.4 UMUHIMU WA UKAGUZI KATIKA KUIMARISHA UTAWALA BORA ...................... 4
1.5 KAMATI ZA BARAZA LA WAWAKILISHI ........................................ 4
**SURA YA PILI** ........................................ 6
2.0 MUHTASARI WA MAMBO YALIYOBAINIKA PAMOJA NA UFAFANUZI WA HATI ZA UKAGUZI ........................................ 7
2.1 MUHTASARI WA MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 ........................................ 7
2.2 DOSARI ZA KIUTENDAJI ZILIZOBAINIKA KATIKA UKAGUZI ........................................ 7
2.3 UWASILISHAJI WA HESABU ZA MWISHO WA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 ... 9
2.4 HATI ZA UKAGUZI ........................................ 11
2.5 AINA YA HATI ZA UKAGUZI ........................................ 11
2.6 MSINGI WA HATI ZA UKAGUZI ........................................ 12
2.7 HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 ........ 13
2.8 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA HOJA ZA UKAGUZI KWA MWAKA ULIOPITA ........................................ 16
**SURA YA TATU** ........................................ 17
3.0 TATHMINI YA MIFUMO YA UDHIBITI WA NDANI ........................................ 18
3.1 MATOKEO YA TATHMINI YA MFUMO WA UDHIBITI WA NDANI ...................... 18
3.1.1 DOSARI ZA UJUMLA ZILIZOBAINIKA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 ........................................ 18

**SURA YA NNE** ........................................ 51
4.0 MAANDALIZI YA BAJETI NA UTEKELEZAJI WAKE ........................................ 52
4.1 MTIZAMO WA JUMLA WA BAJETI ........................................ 52
4.1.1 MWENENDO WA MAPATO YA NDANI IKILINGANISHWA NA BAJETI ILIYOIDHINISHWA ........................................ 52
4.1.2 MWENENDO WA MAPATO YATOKANAYO NA VYANZO VYA NDANI IKILINGANISHWA NA RUZUKU ........................................ 56
**SURA YA TANO** ........................................ 60
5.0 MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 ... 61
5.1 TAARIFA ZA UKAGUZI WA HESABU ZA TAWALA ZA MIKOA ........................................ 61
5.1.1 FUNGU D 07 - MKOA WA MJINI MAGHARIBI ........................................ 61
5.1.2 FUNGU D 08 - MKOA WA KUSINI UNGUJA ........................................ 62
5.1.3 FUNGU D 09 - MKOA WA KASKAZINI UNGUJA ........................................ 67
5.1.4 FUNGU D 10 - MKOA WA KUSINI PEMBA ........................................ 70
5.1.5 FUNGU D 11 - MKOA WA KASKAZINI PEMBA ........................................ 71
**SURA YA SITA** ........................................ 74
6.0 TAARIFA ZA UKAGUZI WA HESABU ZA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA ......... 75
6.1 UANZISHWAJI WA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA ........................................ 75
6.2 LENGO LA KUANZISHWA KWA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA ........................................ 75
6.3 UKAGUZI WA HESABU ZA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA ........................................ 75
6.3.1 FUNGU 201 - BARAZA LA JIJI LA ZANZIBAR ........................................ 76
6.3.2 FUNGU 202 - BARAZA LA MANISPAA YA MJINI ........................................ 77
6.3.3 FUNGU 204 - BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI “B” ........................................ 81
6.3.4 FUNGU 205 - BARAZA LA MJI WILAYA YA KASKAZINI “A” ........................................ 84
6.3.5 FUNGU 206 - BARAZA LA MJI WILAYA YA KASKAZINI “B” ........................................ 85
6.3.6 FUNGU 207 - BARAZA LA MJI WILAYA YA KATI ........................................ 86
6.3.7 FUNGU 208 - HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI UNGUJA ........................................ 89
6.3.8 KASMA 209 - BARAZA LA MJI WETE ........................................ 93
6.3.9 KASMA 210 - BARAZA LA MANISPAA CHAKE CHAKE ........................................ 98
6.3.10 KASMA 211 - BARAZA LA MJI MKOANI ........................................ 101
6.3.11 KASMA 212 - HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI ........................................ 104

**SURA YA SABA** ........ 108

7.0 TAARIFA ZA UKAGUZI WA HESABU ZA IDARA MAALUM ZA SMZ ........ 109

7.1 UTANGULIZI ........ 109

7.1.1 FUNGU D 04 - KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM) ...... 109

7.1.2 FUNGU D 02 - JESHI LA KUJENGA UCHUMI ........ 119

7.1.3 FUNGU D 03 - CHUO CHA MAFUNZO ........ 128

7.1.4 FUNGU D 06 - KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR ........ 131

7.1.5 FUNGU D 05 - KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI ........ 134

8.0 HITIMISHO ........ 144

## ORODHA YA MAJADWELI


Jadweli Nambari 1: Orodha ya Taasisi zilizowasilisha taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka ........ 10

Jadweli Nambari 2:Taasisi za Serikali zilizokaguliwa na kupata Hati za ukaguzi ........ 14

Jadweli Nambari 3:Dosari za kiutendaji zilizobainika kwa vitengo vya usimamizi na udhibiti wa ndani ........ 19

Jadweli Nambari 4:Taasisi zilizochelewa kuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka ........ 20

Jadweli Nambari 5:Taasisi zilizobainika kuwa na mapungufu katika daftari la Kuhifadhia Mali za Kudumu ........ 21

Jadweli Nambari 6:Taasisi zilizokosa buku linaloonyesha mienendo ya safari katika vyombo vya moto (log book) ........ 22

Jadweli Nambari 7:Taasisi zisizokuwa na bajeti ya mapato na matumizi ........ 24

Jadweli Nambari 8:Taasisi zilizobainika na dosari katika mfumo wa MUTM pamoja na vifaa vya kukusanyia mapato (POS) ........ 25

Jadweli Nambari 9:Dosari za kutokuwepo/kutokufanyiwa maboresho kwa daftari la kumbukumbu za mikataba ........ 26

Jadweli Nambari 10:Taasisi zenye dosari za kiutendaji za Kamati za Ukaguzi ........ 27

Jadweli Nambari 11:Watumishi wa kutwa walioajiriwa bila ya Kibali ........ 28

Jadweli Nambari 12: Mali za Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizokosa nyaraka za umiliki ........ 30

Jadweli Nambari 13:Vyombo vya Usafiri Ambavyo Havijakatiwa Bima ........ 31

Jadweli Nambari 14: Ununuzi wa vifaa vya kuandikia kwa watoa huduma wengine ........ 36

Jadweli Nambari 15:Taasisi ambazo hazikuandaa Mkataba wa Huduma kwa Umma ........ 37

Jadweli Nambari 16:Taasisi zisizokuwa na Kitengo cha Usimamizi wa Mali pamoja na Mpango wa matengenezo wa Mali zinazomilikiwa na Afisi ........ 38

Jadweli Nambari 17:Malipo ya matengenezo ya magari katika gereji binafsi ........ 39

Jadweli Nambari 18:Gari ambazo hazijafanyiwa matengenezo kwa muda mrefu ........ 42

Jadweli Nambari 19:Taasisi ambazo hazikufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato ya vyanzo vya ndani kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ........ 44

Jadweli Nambari 20:Mali za Taasisi ambazo hazina hati miliki ........ 45

Jadweli Nambari 21:Taasisi ambazo hazina vifaa vya huduma ya kwanza ........ 46

Jadweli Nambari 22:Taasisi ambazo hazina Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi ........ 47

Jadweli Nambari 23:Taasisi za Serikali zilizoshindwa kuandaa au kuboresha Mpango Mkakati ........ 48

Jadweli Nambari 24:Taasisi ambazo hazina Mpango wa Kukabiliana na Maafa ........ 50

Jadweli Nambari 25:Taasisi ambazo hazijaandaa Mpango wa likizo........................... 50
Jadweli Nambari 26:Mtazamo wa Jumla wa Bajeti................................................ 54
Jadweli Nambari 27: Taarifa ya Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ikilinganishwa na Ruzuku ........................................................................ 58
Jadweli nambari 28:Mali za Taasisi ambazo hazina hati miliki .................................. 63
Jadweli Nambari 29:Matumizi ya Mafuta kwa Viongozi wateule wa Rais.................... 65
Jadweli Nambari 30:Madeni ya muda mrefu ya Ofisi............................................... 67
Jadweli Nambari 31:Deni la fidia ya vipando vya wananchi ..................................... 68
Jadweli Nambari 32:Kutokulipwa kwa fidia ya vipando kwa Wananchi ...................... 69
Jadweli Nambari 33:Watumishi Ambao Hawajapatiwa Mafunzo ya Awali .................. 71
Jadweli Nambari 34: Nyaraka zilizokosekana katika Majalada binafsi ya Watumishi.... 73
Jadweli Nambari 35:Mapato ya ada ya taka za Mahoteli ambayo hayakuweza kukusanywa ........................................................................ 88
Jadweli Nambari 36:Skuli ambazo hazijakata leseni ya biashara ............................... 91
Jadweli Nambari 37:Watumishi waliopatiwa mafunzo bila ya kuwepo kwa Mpango wa Mafunzo.................................................................... 93
Jadweli Nambari 38: Madeni yaliyokosa Nyaraka za Uchambuzi ............................... 94
Jadweli Nambari 39: Malipo ya fedha ambayo hayajawafikia wadai .......................... 95
Jadweli Nambari 40: Hati za malipo zenye nyaraka pungufu .................................. 96
Jadweli Nambari 41:Malipo yasiyokuwa na mkataba wa ununuzi wa mafuta............. 99
Jadweli Nambari 42:Tofauti ya taarifa za mapato baina ya Mfumo wa MUTM na taarifa nyengine za mapato ............................................... 101
Jadweli Nambari 43: Utofauti wa Taarifa za Mapato ............................................. 103
Jadweli Nambari 44: Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu................................. 105
Jadweli Nambari 45: Malipo ya ununuzi wa mashine za kukaushia Mwani ............... 107
Jadweli Nambari 46:Matumizi yaliyofanywa bila ya kuzingatia bajeti....................... 110
Jadweli Nambari 47:Vifaa vya ujenzi ambavyo havijawasilishwa na Mzabuni ........... 113
Jadweli Nambari 48:Malipo ambayo hayakufuata taratibu za manunuzi ................. 114
Jadweli Nambari 49:Mapato yatokanayo na kazi ya ulinzi wa Kampuni za Mafuta .... 115
Jadweli Nambari 50: Malipo yaliyofanyika kwa njia ya fedha taslimu...................... 116
Jadweli Nambari 51:Miradi ambayo haikutekelezwa ............................................ 117
Jadweli Nambari 52: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu ................................ 119
Jadweli Nambari 53:Vifaa vilivyochelewa kuwasilishwa katika eneo la ujenzi ........... 121

Jadweli Nambari 54:Kutokuwepo kwa uhalisia katika utayarishwaji wa nyaraka za BOQ........................................................................ 121
Jadweli Nambari 55:Malipo ambayo hayakufuata taratibu za manunuzi .................. 125
Jadweli Nambari 56: Gari za JKU zinazoonyesha kumilikiwa na watu binafsi............ 126
Jadweli Nambari 57: Makusanyo ya mapato yaliyotumiwa kinyume na taratibu ....... 127
Jadweli Nambari 58:Makusanyo ya mapato yaliyotumiwa kinyume na utaratibu ...... 134
Jadweli Nambari 59:Ukiukwaji wa taratibu za malipo ya Posho mbali mbali............. 135
Jadweli Nambari 60:Tofauti iliyobainika baina ya fedha halisi na makisio................. 137
Jadweli Nambari 61:Hali halisi ya Magari katika vituo vya Zimamoto na Uokozi ....... 141
Jadweli Nambari 62 : Makusanyo ya mapato yaliyotumiwa kinyume na taratibu ...... 144

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| BOQ | Mchanganuo wa Gharama za Ujenzi |
| CAG | Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu na Serikali |
| EY | Ernst & Young |
| IFRS | International Financial Reporting Standards |
| INTOSAI | Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi |
| IPSAS | International Public Sector Accounting Standards |
| ISA | Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Hesabu |
| ISSAIs | Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi katika Taasisi za Umma |
| LAAC | Kamati ya Kudhibiti na Kuchunguza Hesabu za Serikali za Serikali za Mitaa na Mashirika |
| MUTM | Mfumo wa Kukusanyia mapato ya Serikali za Mitaa |
| Nam. | Nambari |
| NAOT | Afisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| NBAA | Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu Tanzania |
| OCAGZ | Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar |
| PAC | Kamati ya Kudhibiti na Kuchunguza Hesabu za Serikali Kuu |
| POS | Point of Sale |
| SAIs | Supreme Audit Institutions |
| SMZ | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| TAC | Tanzania Audit Corporation |
| Tshs/Tsh. | Shilingi ya Tanzania |
| UNCDF | United Nation Capital Development Fund |
| UNICEF | United Nation International Children Emagency Fund |
| USD | Dola ya Kimarekani |
| VAT | Kodi ya Ongezeko la Thamani |
| ZANMALIPO | Mfumo wa Malipo wa Kielektroniki wa Serikali |
| ZICTIA | Shirika la Miundombinu ya Tehama Zanzibar |

# SHUKURANI

Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada zake za mara kwa mara anazoendelea kuzichukuwa ikiwa ni pamoja na kuweka msisitizo na kutoa maelekezo katika kufanya marekebisho juu ya dosari mbali mbali zinazobainishwa katika Ripoti za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali pamoja na hatua anazoendelea kuzichukua kutokana na hoja za ukaguzi zinazoibuliwa kuhusu matumizi ya fedha pamoja na usimamizi wa rasilimali za Umma.

Vile vile napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Viongozi Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar akiwemo Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Othman Masoud Othman, Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Hemed Suleiman Abdulla, pamoja na watendaji mbali mbali wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mashirikiano yao wanayokupatia katika utekelezaji wa majukumu yako ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa lengo la kuwaletea maendeleo endelevu ya nchi yao.

Shukurani zangu za dhati ziende kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Zubeir Ali Maulid, Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa kujitolea kwa dhati kujadili na kutoa mapendekezo pamoja na kufuatilia hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuyafanyia kazi mapendekezo yanayotolewa katika Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu kusimamia uwajibikaji na utekelezaji wa majukumu ya watendaji katika sekta mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aidha, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba Sheria, Utumishi na Utawala Bora Mhe. Mwalimu Haroun Ali Suleiman kwa kuniunga mkono na kunipa nguvu katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kikatiba, pamoja na jitihada zake anazozichukuwa katika kusimamia misingi ya utawala bora.

Vile vile nitoe shukurani zangu za dhati kwa Bodi ya Utumishi ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kusimamia maadili

na nidhamu ya wafanyakazi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kupelekea kuimarika kwa nidhamu na uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu ya kazi zao.

Kwa namna ya kipekee, niwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyengine kuanzia kazi za ukaguzi, ufuatiliaji wa maeneo mbali mbali yaliyokaguliwa hadi kukamilika kwa ripoti hii ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Aidha, nitakuwa mchache wa shukurani kama sitatambua jukumu la vyombo mbali mbali vya habari kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuutambulisha Umma juu ya kazi zinazofanywa na Afisi ya Mdhibiti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambapo matokeo na mapendekezo ya kazi hizo huwasilishwa moja kwa moja kwa jamii kupitia vyombo vya habari.

Natumia fursa hii, kuwasihi wafanyakazi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuendelea kuwa na moyo wa dhati katika kufanya kazi kwa bidii na kuongeza mashirikiano kwa ajili ya siku zijazo ili kuendelea kudumisha nidhamu katika utekelezaji wa majukumu yao.

## DIBAJI



Ninafuraha kubwa ya kuwasilisha Ripoti ya Ukaguzi inayohusu Ukaguzi wa Hesabu za Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023. Wasilisho hilo ni kwa mujibu wa Kifungu cha 112(5) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 pamoja na kifungu nambari 46(1) cha Sheria Nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023, ambapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kikatiba kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa zake za ukaguzi huo angalau mara moja kwa kila mwaka.

Taarifa hizo zitaelezea hali halisi ya mapato na matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na utekelezaji wa Sheria mbali mbali zikiwemo Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016, Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 pamoja na sheria mbali mbali zilizopitishwa na Baraza la Wawakilishi na kutumiwa ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa Mujibu wa Mamlaka niliyonayo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ni jukumu langu la kutoa taarifa huru, zilizosahihi na zilizojitosheleza kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhusiana na usimamizi wa fedha pamoja na matumizi sahihi ya rasilimali za Umma na hatimae taarifa hizo kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi kwa hatua za utekelezaji.


Ripoti hii inajumuisha mambo muhimu yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa taasisi za Serikali kwenye tathmini na ukaguzi wa taarifa za fedha pamoja na nyaraka husika, mifumo ya udhibiti wa ndani, taratibu na mchakato wa manunuzi na uzingatiaji wa Sheria na Kanuni mbali mbali. Kufuatia kukamilika kwa ukaguzi huo nimetoa hati za ukaguzi kwa kila taasisi kuhusiana na taarifa za fedha zilizoandaliwa kama zinaonesha hali halisi ya shughuli zilizofanywa kulingana na mfumo wa uandaaji wa taarifa za fedha.

Nilifanya ukaguzi huo kwa kuangalia mifumo ya udhibiti wa ndani, taratibu za ununuzi, utayarishaji wa taarifa za fedha na nyaraka zilizoambatishwa, kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zilizowekwa pamoja na kuzingatia Viwango kubalifu vya Kitaifa na Kimataifa vya Taasisi za Juu za Hesabu za Serikali (ISSAIs) vinavyotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi za Juu za Ukaguzi (INTOSAI) ambazo zinahusu ukaguzi wa Sekta za Umma.

Nimetoa Hati za Ukaguzi kwa kuzingatia Taarifa za Fedha nilizozikagua na kuzitolea ripoti ya ukaguzi kwa kila taasisi ambayo ilikaguliwa. Aidha, nilitoa barua za ukaguzi "Management Letters" zinazoonesha dosari zilizobainika kwa kila Taasisi iliyokaguliwa na mapendekezo ya kutekeleza ili kuboresha na kuondoa dosari zilizobainika kwa lengo la kutokujirejea.

Ni matumaini yangu kwamba Baraza la Wawakilishi litaona taarifa zilizomo katika ripoti hii ni za muhimu katika kuisimamia Serikali na kuongeza uwajibikaji katika matumizi ya fedha na usimamizi wa rasilimali za umma ili kuhakikisha kunakuwa na utoaji bora wa huduma kwa umma wa Wazanzibari ambao unawahudumia. Katika suala hili nitashukuru kama nitapokea maoni kutoka kwa watumiaji wa ripoti hii juu ya jinsi ya kuiboresha zaidi katika siku zijazo.

Kwa mara nyengine tena nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa jitihada zake anazoendelea kuzichukuwa pamoja na kutoa maelekezo kwa viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya kuyafanyia kazi mapendekezo yanayotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yanayohusu matumizi ya fedha na usimamizi wa rasilimali za Umma.



...................................................

**DKT. OTHMAN ABBAS ALI**
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**
**ZANZIBAR**

## MUHTASARI

Ripoti hii imekusanya jumla ya sura saba (7) zenye kuelezea mambo mbali mbali yaliyobainika katika ukaguzi uliofanyika kwenye Taasisi za Tawala za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Ukaguzi uliofanyika umebaini uwepo wa dosari mbali mbali ambapo dosari hizo zimewasilishwa kwenye uongozi wa Taasisi zilizokaguliwa kwa njia ya hoja za ukaguzi na kutolewa mapendekezo kwa lengo la kuimarisha dosari hizo, baadhi ya dosari ziliweza kufanyiwa kazi na Maafisa Masuuli wakati wa kipindi cha ukaguzi na kutolewa majibu kwa wakaguzi ili kuweza kujiridhisha juu ya uhalali wa dosari hizo. Aidha, baadhi ya dosari zilizobainika hazikuweza kupatiwa majibu wakati wa ukaguzi na kupelekea kuingizwa katika Ripoti hii. Mambo yaliyobainika yamefafanuliwa katika sura tofauti zilizomo katika ripoti hii kama ifuatavyo:-

**Sura ya Kwanza:** Sura hii imekusanya taarifa za Utangulizi wa ripoti ikiwemo majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, upeo na madhumuni ya ukaguzi, njia zilizotumika katika ukaguzi. Vile vile imeeleza umuhimu wa kufanya ukaguzi pamoja na taarifa za Kamati za Baraza la Wawakilishi.

**Sura ya Pili:** Sura hii inaeleza kwa muhtasari mambo yaliyobainika katika ukaguzi wa hesabu pamoja na ufafanuzi wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo miongoni mwa mambo yaliyobainika ni utoaji wa hati za ukaguzi, pamoja na utekelezaji wa mapendekezo ya hoja za ukaguzi kwa mwaka uliopita.

**Sura ya Tatu:** Sura hii inaeleza tathmini ya Mifumo ya udhibiti wa ndani pamoja na dosari za ujumla zilizobainika katika ukaguzi uliofanyika ambazo zimesababishwa na mapungufu ya mfumo wa udhibiti wa ndani.

**Sura ya Nne:** Sura hii inaeleza kwa kina mchanganuo wa utekelezaji wa mipango na bajeti za Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Vile vile inaeleza

mwenendo wa ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha kutoka katika vyanzo mbali mbali ikiwemo vyanzo vya ndani, ruzuku kutoka Serikali Kuu pamoja na misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo.

**Sura ya Tano:** Sura hii imefafanua kwa kina kuhusu matokeo na mapendekezo ya ukaguzi uliofanyika kwa Taasisi tano (5) za Tawala za Mikoa ambapo dosari mbali mbali za kiutendaji zimebainishwa, athari zake na kutolewa ushauri kwa uongozi wa Taasisi hizo.

**Sura ya Sita:** Sura hii imeeleza kwa kina kuhusu matokeo na mapendekezo ya ukaguzi uliofanyika kwa Taasisi kumi na mbili (12) za Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo dosari mbali mbali za kiutendaji zimebainishwa pamoja na athari zake na kutolewa ushauri kwa uongozi wa Taasisi hizo.

**Sura ya Saba:** Sura hii imeeleza kuhusu matokeo na mapendekezo ya ukaguzi uliofanyika kwa Taasisi tano (5) za Idara Maalum za SMZ ambapo dosari mbali mbali za kiutendaji zimebainishwa pamoja na athari zake na kutolewa ushauri kwa uongozi wa Taasisi hizo.

## Tathmini ya Mifumo ya Udhibiti wa Ndani

Ukaguzi ulitathmini mifumo ya udhibiti wa ndani ikiwemo udhibiti katika kitengo cha ukaguzi wa ndani, kamati ya ukaguzi pamoja na Bodi ya Zabuni. Kwa ujumla tathmini iliyofanyika imebainika kujitokeza kwa maboresho makubwa katika vitengo vya ukaguzi wa ndani, Kamati za Ukaguzi pamoja na Bodi za Zabuni kwa baadhi ya Taasisi kupiga hatua za mafanikio ingawa zipo baadhi ya Taasisi zimebainika kuwepo kwa dosari mbali mbali katika mfumo wa udhibiti wa ndani ambapo miongoni mwa dosari kubwa zilizobainika ni kwamba baadhi ya Taasisi zimeshindwa kushirikisha vitengo vya ukaguzi wa ndani na Kamati za Ukaguzi kupitia taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka za Taasisi hizo jambo ambalo lilipelekea hesabu zilizowasilishwa kuwa na dosari za kiutendaji na hatimae kurejeshwa ili ziweze kufanyiwa marekebisho katika hatua za awali za ukaguzi jambo ambalo lilipelekea kutokukamilika kwa kazi za ukaguzi kwa wakati uliopangwa.

## Tathmini katika ukusanyaji wa Mapato

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023, ukaguzi ulibaini hali ya ukusanyaji wa mapato katika Taasisi mbali mbali umeimarika ukilinganisha na ukusanyaji wa mapato kwa mwaka uliopita. Hata hivyo baadhi ya taasisi zimebainika kuwa na dosari za kiutendaji ambazo zinahitaji marekebisho ya haraka ili kunusuru kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma unaotokana na baadhi ya taasisi kukusanya mapato nje ya mfumo, mapato kutumika kabla ya kuwasilishwa benki, ucheleweshwaji wa mapato kuwasilishwa sehemu husika, upotevu wa vitabu vya kukusanyia mapato, kutokulingana kwa mapato halisi yanayokusanywa na yale yanayowasilishwa benki pamoja na kutokuoneshwa kwa mapato halisi yaliyokusanywa katika hesabu za mwisho wa mwaka.

Kutokana na dosari zilizobainishwa hapo juu zimepelekea baadhi ya Taasisi kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kulikosababishwa na baadhi ya watendaji kushikilia fedha za mapato mikononi pasi na kuziwasilisha sehemu husika na hatimae hesabu za taasisi hizo kutokuonesha sura halisi na sahihi.

## Mwenendo wa Mapato ya Ndani ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa

Mapato ya ndani yanajumuisha kodi za ndani, ada, tozo, ushuru, vibali vya ujenzi na mapato mengineyo. Fedha hizi hutumika kuongezea ruzuku iliyotolewa na Serikali Kuu na Washirika wa Maendeleo.

## Tawala za Mikoa

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 Taasisi tano (5) za Tawala za Mikoa zilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 80,140,004 kutoka katika vyanzo vya ndani ikilinganishwa na bajeti ya shilingi 243,476,856 ambapo ilionesha upungufu wa mapato kwa kiasi cha shilingi 163,336,852 sawa na asilimia 67.08 ya upungufu wa bajeti iliyoidhinishwa.

## Mamlaka za Serikali za Mitaa

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya Mamlaka tisa (9) kati ya Mamlaka kumi na mbili (12) za Serikali za Mitaa zilifanikiwa

kukusanya jumla ya shilingi 11,583,299,018.62 kutoka katika vyanzo vya ndani ikilinganishwa na bajeti ya shilingi 15,545,595,450 ambapo ilionesha upungufu wa mapato kwa kiasi cha shilingi 3,962,296,431.38 sawa na asilimia 25.49 ya upungufu wa bajeti iliyoidhinishwa.

Aidha, jumla ya Mamlaka mbili (2) kati ya Mamlaka kumi na mbili (12) za Serikali za Mitaa zilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 2,970,249,713.2 kutoka katika vyanzo vya ndani ikilinganishwa na bajeti ya shilingi 1,925,260,000 ambapo ilionesha ziada ya mapato kwa kiasi cha shilingi 1,044,989,713.2 sawa na asilimia 54.28 ya ziada ya bajeti iliyoidhinishwa.

Kutokana na mchanganuo uliobainishwa hapo juu unamaanisha ya kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja na Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "A" yanaonekana kuwa na ufanisi mkubwa katika usimamizi na ufuatiliaji wa ukusanyaji wa mapato ikilinganishwa na Mamlaka nyengine tisa (9) ambazo zinaonekana kukosa ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.

Aidha, ukaguzi umebaini Taasisi moja ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa haikupangiwa bajeti ya makusanyo yatokanayo na vyanzo vya ndani, hivyo ukaguzi unashauri Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha inalitizama kwa kina suala la uwepo wa bajeti ya makusanyo ili taasisi hiyo iweze kutoa huduma kwa jamii na kuweza kujiendesha wenyewe kwa mujibu wa dhana ya Serikali ya kulianzisha Baraza la Jiji la Zanzibar.

## Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 Taasisi nne (4) za Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zilikusanya jumla ya shilingi 586,243,350 kutoka katika vyanzo vya ndani ikilinganishwa na bajeti ya shilingi 2,385,107,401 ambapo ilionesha kukosekana kwa ufanisi katika ukusanyaji wa mapato jambo ambalo limepelekea kuwepo kwa upungufu mkubwa wa mapato yaliyokusanywa kwa kiasi cha shilingi 1,798,864,051 sawa na asilimia 75.42 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Aidha, ukaguzi umebaini Taasisi moja ya Idara Maalum ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haikupangiwa bajeti ya makusanyo yatokanayo na vyanzo vya ndani, hivyo ukaguzi unashauri Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha inalitizama kwa kina suala la uwepo wa bajeti ya

makusanyo ili taasisi hiyo iweze kutoa huduma ikiwemo huduma za ulinzi na nyenginezo kwa njia ya ukusanyaji wa mapato ili iweze kutekeleza baadhi ya mipango yake iliyojipangia na kuacha kutegemea bajeti ya Serikali kwa asilimia mia moja (100).

## Mwenendo wa Mapato yatokanayo na Vyanzo vya Ndani ikilinganishwa na Ruzuku

Ruzuku ya matumizi ya kawaida inahusisha fedha za uendeshaji wa shughuli za kila siku ikijumuisha malipo ya mishahara kwa watumishi, manunuzi ya vifaa na huduma mbali mbali za uendeshaji wa Taasisi ambapo chanzo kikuu cha fedha ni ruzuku ya matumizi ya kawaida kutoka Serikali Kuu na makusanyo ya ndani.

## Tawala za Mikoa

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 Taasisi tano (5) za Tawala za Mikoa zilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 80,140,004 kutoka katika vyanzo vya ndani ikilinganishwa na matumizi ya kawaida ya shilingi 26,929,673,076 ambapo ilionesha upungufu wa mapato kwa kiasi cha shilingi 26,849,533,072 sawa na asilimia 99.70 ya ruzuku iliyotolewa.

Kutokana na taarifa iliyopo hapo juu inaonesha kwamba Taasisi tano za Tawala za Mikoa zinategemea zaidi ruzuku kutoka Serikalini kwa kiwango cha asilimi 99.7 jambo ambalo linaonesha taasisi hizo hazitoweza kujiendesha pindipo Serikali itakapoziacha mkono wa kuzipa ruzuku.

Ukaguzi unazishauri Taasisi hizo kuongeza umakini wa ukusanyaji wa mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani pamoja na kuibua vyanzo vipya vya ukusanyaji wa mapato ili ziweze kujiendesha bila ya utegemezi wa Serikali. Mchanganuo wa taarifa hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

## Mamlaka za Serikali za Mitaa

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 Mamlaka za Serikali za Mitaa kumi na mbili (12) zilikusanya jumla ya shilingi 14,553,548,731.82 kutoka katika vyanzo vya ndani ikilinganishwa na ruzuku kutoka Serikali ni yenye jumla ya shilingi 16,926,232,594.73 ambapo inaonesha upungufu wa mapato kwa kiasi cha shilingi 2,372,683,862.91 sawa na asilimia 14.02 ya upungufu wa ruzuku iliyotolewa.

Kutokana na Taarifa zilizobainishwa hapo juu zinaonesha kwamba jumla ya Taasisi nne (4) kati ya Taasisi kumi na mbili (12) za Mamlaka ya Serikali za Mitaa hazikuweza kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato yatokanayo na vyanzo vyake vya ndani na kubainika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 taasisi hizo kuwa na wastani wa asilimia 76 na kutegemea ruzuku kutoka Serikali Kuu jambo ambalo linaweza kupelekea uwezekano mkubwa wa kushindwa kutoa huduma kwa jamii pindipo Serikali Kuu ikisita kuzipatia ruzuku Taasisi hizo.

Ukaguzi unazishauri Taasisi hizo kuongeza umakini katika kusimamia vyanzo vyake vya mapato ikiwemo kubuni vyanzo vipya ili kuweza kuleta tija na ufanisi wa kujiendesha kwa Taasisi hizo.

Aidha, ukaguzi umebaini Baraza la Jiji la Zanzibar halikupangiwa bajeti ya makusanyo yatokanayo na vyanzo vya ndani na kupelekea kutegemea ruzuku kutoka Serikalini kwa asilimia mia moja (100) jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya uanzishwaji wa Baraza la Jiji la Zanzibar ikilinganishwa na ufanyaji kazi wa Baraza la Jiji la nchi nyenginezo.

Ukaguzi unaishauri Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha unalitizama kwa kina suala la uwepo wa vyanzo vya mapato vitakavyosimamiwa na Baraza la Jiji la Zanzibar ili Serikali ichukuwe maamuzi ya kulipangia bajeti maalum ya makusanyo yatokanayo na vyanzo hivyo kwa lengo la kuweza kujiendesha na kujitegemea wenyewe kwa baadhi ya huduma inazozitoa.

### Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 Idara Maalum tano (5) za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 586,243,350 kutoka katika vyanzo vya ndani ikilinganishwa na ruzuku ya shilingi 131,145,917,870.55 iliyotolewa kwa Taasisi hizo ambapo ilionesha upungufu wa mapato kwa kiasi cha shilingi 130,559,674,520.55 sawa na asilimia 99.55 ya ruzuku iliyotolewa.

Aidha, ukaguzi umebaini Kikosi cha Valantia hakikupangiwa bajeti ya makusanyo yatokanayo na vyanzo vya ndani, hivyo kuendelea kutegemea ruzuku kutoka Serikalini kwa asilimia mia moja (100%) katika uendeshaji wa shughuli zake za kila siku.

Kutokana na hali hiyo kwa vile Kikosi cha Valantia kina uwezo wa kuanzisha miradi mbali mbali ya kujitegemea ikiwemo miradi ya ushoni, ufugaji, ulinzi, pamoja na miradi mengineyo kwa lengo la kuanzisha vyanzo vya mapato ya ndani ukaguzi unashauri Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuliangalia kwa kina suala la uwepo wa vyanzo vipya vya mapato na kuvibariki kwa Kikosi cha Valantia kuweza kuvisimamia na hatimae kukusanya mapato ili yaweze kusaidia upatikanaji wa huduma nyenginezo bila ya uwepo wa utegemezi wa ruzuku kwa asilimia mia moja (100%) kama ilivyo hivi sasa.

### Tathmini ya Usimamizi wa Matumizi

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023 ukaguzi umebaini kuimarika kwa nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa taasisi mbali mbali na kupelekea kuongezeka kwa hati zinazoridhisha na kuleta faraja na nidhamu juu ya usimamizi wa matumizi ya fedha za umma.

Hata hivyo zipo baadhi ya taasisi zimebainika kuwa na mapungufu mbali mbali katika nidhamu ya usimamizi wa matumizi na kupelekea kutokuzingatia matakwa ya Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016. Miongoni mwa dosari kubwa zilizobainika katika nidhamu ya matumizi ni kufanyika kwa malipo kwa fedha taslim, dosari katika uzuwiaji wa kodi, ucheleweshwaji wa mapato ya Serikali kuwasilishwa benki kwa wakati pamoja na kutokuzingatia maelekezo ya Serikali kuhusiana na kudai stakabadhi za kielektroniki wakati wa ufanyaji wa malipo.

### Tathmini ya Usimamizi wa Manunuzi

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023, ukaguzi ulibaini uwepo wa maboresho katika Taasisi mbali mbali zilizofanya manunuzi kwa kufanya manunuzi kupitia mfumo wa manunuzi pamoja na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zinazohusiana na manunuzi hayo, ingawa zipo baadhi ya Taasisi zilibainika kutokuzingatia Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya 2016 pamoja na Kanuni zake wakati wa kufanya manunuzi.

Aidha, baadhi ya taasisi zimebainika kufanya manunuzi bila ya kuzingatia ushindani wa bei, kufanya manunuzi kwa kutumia rasimu za mikataba, kufanya manunuzi bila ya kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu kupitia rasimu za mkataba walizoziwasilisha, kutokuambatishwa kwa nyaraka muhimu za manunuzi katika hati za malipo, kufanya manunuzi kinyume na mpango wa manunuzi, kutokuwasilishwa kwa mpango wa manunuzi kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali jambo ambalo limepelekea baadhi ya Taasisi kufanya manunuzi nje ya mpango wa manunuzi au kufanya manunuzi yaliyo na gharama kubwa zaidi kuliko uhalisia wa bajeti iliyowekwa kwenye mpango wa manunuzi.

## Tathmini katika Usimamizi wa Mikataba

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023 ukaguzi ulibaini mapungufu mbali mbali yanayotokana na ukiukwaji wa Sheria na taratibu za manunuzi unaotokana na baadhi ya Taasisi kushindwa kuwasilisha rasimu za mikataba yao Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa lengo la kufanyiwa mapitio na kupatiwa ushauri wa kisheria juu ya namna bora ya kufanya maboresho ya dosari zilizobainika katika rasimu za mikataba hiyo.

Hata hivyo zipo baadhi ya taasisi zimebainika kutokutekeleza maagizo na mashauri yanayotolewa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuhusiana na maboresho ya rasimu za mikataba na hatimae kufanya manunuzi na kuingia katika makubaliano ya kimkataba bila ya uwepo wa mikataba yenye tija na maslahi kwa Serikali na hatimae kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma kunakotokana na kutokutekelezwa kwa maagizo ya mikataba inayopitiwa na Mwanasheria Mkuu.

## Tathmini ya Hati za Ukaguzi

Kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023, ukaguzi ulifanyika kwa taasisi mbali mbali kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa. Kutokana na kuzingatiwa kwa vigezo vya ufungaji wa hesabu kwa taasisi za umma kumepelekea kuimarika kwa Hati za ukaguzi zinazoridhisha kwa taasisi mbali mbali zilizokaguliwa. Hata hivyo zipo baadhi ya Taasisi ziliendelea kuwa na dosari kubwa za ufungaji wa hesabu zao na kupelekea kulazimika kufanyiwa marekebisho kwa hesabu hizo.

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, jumla ya hati za ukaguzi Ishirini na Mbili **(22)** zimetolewa katika ripoti hii ambapo kati ya hati hizo, hati Kumi na Tisa **(19)** ni hati zinazoridhisha sawa na asilimia **86.36** ya hati zilizotolewa na hati Tatu **(3)** ni hati zenye shaka sawa na asilimia **13.64** ya hati zilizotolewa na hapakuwa na hati mbaya wala hati ya kushindwa kutoa maoni kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Nichukuwe fursa hii kuwapongeza Maafisa Masuuli kutokana na jitihada walizozichukuwa katika kusimamia ufungaji wa hesabu uliozingatia vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa pamoja na kuwajengea uwezo watendaji wao katika utekelezaji wa majukumu yao.

## Tathmini ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi kwa mwaka uliopita

Tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa mwaka uliopita inaonesha kuwa, kati ya mapendekezo **512** niliyoyatoa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, mapendekezo **380** sawa na asilimia **74.22** yametekelezwa, mapendekezo **44** sawa na asilimia **8.59** yapo kwenye hatua mbali mbali za utekelezaji, mapendekezo **47** sawa na asilimia **9.18** hayajatekelezwa, mapendekezo **23** sawa na asilimia **4.49** yamejirudia na mapendekezo **18** sawa na asilimia **3.52** yamepitwa na wakati

# SURA YA KWANZA



# 1.0 UTANGULIZI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibu wa kukagua hesabu zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ukaguzi huo unafanyika kwa mujibu wa kifungu cha 112 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar unajumuisha hesabu zote za Serikali kuu, Mashirika ya Umma na Taasisi zinazojitegemea, Serikali za Mitaa, Mamlaka na Taasisi mbali mbali pamoja na Miradi mbali mbali ya maendeleo na baadae kutoa taarifa ya ukaguzi wa hesabu hizo kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya Zanzibar.

Kutokana na mamlaka ya kikatiba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibu wa kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar matumizi yake yameidhinishwa kisheria ambapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibu wa kuidhinisha matumizi kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kufanya ukaguzi wa hesabu hizo.

## 1.1 Majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Kwa mujibu wa kifungu nambari 112 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa zake za ukaguzi huo angalau mara moja kila mwaka. Taarifa hizo zitaelezea hali halisi za mapato na matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na utekelezaji wa sheria mbali mbali zikiwemo Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016, Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 pamoja na sheria mbali mbali zilizopitishwa na Baraza la Wawakilishi na kutumiwa ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 112(3) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu anawajibika kufanya yafuatayo:-

a) "Kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, matumizi yake yameidhinishwa kisheria na iwapo atatosheka kwamba masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe.

b) Kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yanatokana na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi, na ambazo zimetumika kwa ajili ya shughuli zilizohusika na matumizi ya fedha hizo na kwamba matumizi hayo yamefanywa kwa kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo; na

c) Angalau mara moja kwa kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu za Mahkama zote za Zanzibar, hesabu za Tume au vyombo vyengine vilivyoanzishwa na Katiba hii na hesabu zozote zinazohusika na Baraza la Wawakilishi. ”

Ukaguzi wa hesabu umefanywa kwa kuzingatia miongozo na vigezo mbali mbali vya ukaguzi ili kukidhi matarajio ya wadau wetu na wananchi kwa ujumla. Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaendelea kufanya uchambuzi wa njia bora zaidi kwa kufanya ukaguzi utakaoleta tija na kuongeza wigo kwa maeneo yanayokaguliwa ili kuweza kuimarisha utendaji na uwajibikaji katika sekta za Umma.

## 1.2 Upeo na Madhumuni ya Ripoti ya Ukaguzi

Ripoti hii imekusanya taarifa za ukaguzi wa hesabu za Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuzingatia taarifa za mapato na matumizi ya kawaida, matumizi ya maendeleo pamoja na michango mbali mbali kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, kwa kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

Ukaguzi ulifanyika kwa mujibu wa viwango vya kitaifa na kimataifa vya ukaguzi na kujiridhisha kwamba taarifa zitakazotolewa zitaonyesha sura halisi ili kutoa uhakika kwamba taarifa za mapato na matumizi zimefuata Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo. Taarifa za hesabu zilizokaguliwa zilijumuisha hesabu za mwisho wa mwaka pamoja na taarifa mbalimbali zinazohusiana na hesabu hizo.

Mabadiliko ya mifumo ya ukaguzi na uhasibu yanayotokea kwa mujibu wa viwango vya kitaifa na kimataifa yamepelekea kuwepo na mafanikio makubwa katika utendaji na uwajibikaji kwenye sekta za Umma katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya rasilimali za umma. Mafanikio hayo yametokana na kuimarika kwa mfumo wa fedha pamoja na utekelezaji wa sheria mbalimbali zikiwemo Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016, Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 pamoja na sheria mbali mbali zilizopitishwa na Baraza la Wawakilishi na kutumiwa ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kupelekea kuimarika kwa uwazi na uwajibikaji katika taasisi za Umma pamoja na utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo na kuleta tija kwa wananchi na kufanikisha lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha dhana nzima ya utawala bora.

## 1.3 Njia zilizotumika katika ukaguzi

Katika kufanya ukaguzi wa hesabu za Serikali mbinu na njia mbali mbali za ukaguzi zilitumika ikiwemo taratibu za ukaguzi zifuatazo: -

i. Kutoa barua za awali za maandalizi ya ukaguzi (Engagement Letter) kwa Taasisi inayokaguliwa.

ii. Kuangalia viashiria vya maeneo hatarishi katika taasisi zinazokaguliwa kwa lengo la kupata uelewa wa mazingira ya taasisi hiyo ikiwemo mfumo wa udhibiti wa ndani na kubaini viashiria vitakavyoathiri udhibiti wa ndani pamoja na utendaji wa taasisi.

iii. Kuandaa mikakati ya ukaguzi kuanzia mpango wa awali hadi mpango mkuu wa ukaguzi (Pre Planning, Strategic Planing and detailed Planning) itakayozingatia muelekeo na upeo wa ukaguzi ambapo utaonyesha dira na dhamira nzima ya ukaguzi huo.

iv. Kufanya kikao cha kuanza kazi za ukaguzi (Entrance Meeting) pamoja na uongozi wa Taasisi zinazokaguliwa.

v. Kupitia na kuhakiki nyaraka mbalimbali pamoja na kupata taarifa kutoka kwa wahusika ili kupata uelewa wa kazi za Taasisi zinazokaguliwa.

vi. Kutumia njia na mbinu mbalimbali za ukaguzi kama ilivyoainishwa kwenye muongozo wa ukaguzi (Compliance Audit Manual & Financial Audit Manual).

vii. Kufanya kikao cha kumaliza ukaguzi (Exit Meeting) na uongozi wa Taasisi inayokaguliwa baada ya kumaliza ukaguzi ambapo katika kikao hicho wakaguzi na uongozi wa taasisi hupitia kwa pamoja hoja zilizojitokeza wakati wa ukaguzi.

viii. Kutoa ripoti ya ukaguzi ya awali (Management letter) kwa uongozi wa taasisi inayokaguliwa itakayoainisha hoja za ukaguzi pamoja na mambo mbalimbali yaliyobainika wakati wa ukaguzi na kutoa nafasi kwa uongozi kutoa majibu na vielelezo kuhusiana na ripoti hiyo kwa muda unaotakiwa kwa mujibu wa sheria.

ix. Kufuatilia majibu ya hoja za ukaguzi yaliyotolewa katika ripoti ya ukaguzi ya awali ili kuweza kujiridhisha na majibu ya hoja hizo.

x. Kutoa Ripoti Kuu ya Mwaka kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

## 1.4 Umuhimu wa ukaguzi katika kuimarisha Utawala Bora

Lengo kuu la kufanya ukaguzi ni kuhakikisha kwamba fedha inayoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa sheria inatumika ipasavyo na kwa malengo yaliyokusudiwa kwa kuleta ufanisi na tija kwa maslahi ya wananchi na taifa kwa ujumla. Aidha, ukaguzi wa hesabu unalenga kuimarisha uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali za umma na kupelekea kuimarika kwa dhana nzima ya Utawala Bora.

Aidha, kuimarika kwa utendaji wa kazi za ukaguzi kunapelekea kuongezeka kwa uwazi na uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha na rasilimali za umma na kuleta tija na ufanisi na kufanikisha kutekeleza malengo yaliyopangwa na Serikali kwa wakati uliopangwa. Aidha, kuimarika kwa utendaji wa kazi za ukaguzi kunapelekea kuimarika kwa hali ya uchumi wa nchi pamoja na kuimarika kwa hali za wananchi kwa jumla.

Katika kufanikisha malengo ya Serikali ya kuimarisha utawala bora nchini, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imejipanga kutekeleza majukumu yake ya kikatiba kwa kuongeza ufanisi wa kazi pamoja na kuendelea na jitihada zake za kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo na mbinu mbalimbali za ukaguzi ili kwenda sambamba na mabadiliko ya mifumo ya uhasibu na ukaguzi pamoja na mabadiliko ya kasi ya teknolojia duniani katika masuala ya udhibiti na ukaguzi wa hesabu za Serikali.

## 1.5 Kamati za Baraza la Wawakilishi

Katika kuleta ufanisi na kufikia malengo ya Serikali iliyojipangia, Baraza la Wawakilishi ni nguzo imara katika kuimarisha uwajibikaji na kusimamia rasilimali za umma kuweza kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa na kuleta tija kwa jamii. Aidha, Kamati za Baraza la Wawakilishi zinatoa mchango mkubwa katika kujenga na kusimamia misingi ya utawala bora na uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali za Umma.

Kwa kuzingatia majukumu na umuhimu wa Kamati za Baraza la Wawakilishi Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imekuwa ikishirikiana na Kamati hizo katika kufuatilia utekelezaji wa bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na kuhakikisha kwamba taasisi za Serikali zinatekeleza malengo waliyojipangia kama yalivyoainishwa katika Bajeti zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi.

Hata hivyo upeo wa mahusiano wa Taasisi za ukaguzi duniani (SAIs) na Mabunge (Baraza la Wawakilishi) unatofautiana baina ya nchi na nchi duniani ambapo kuna baadhi ya nchi taasisi za ukaguzi huwa ni sehemu ya Bunge (Legislative) na baadhi huwa chini ya utawala (Executive) na baadhi ya nchi nyengine Taaisisi za ukaguzi huwa haziko kokote yaani sio (legislative wala Executive). Kwa hivyo taasisi za ukaguzi zina jukumu la kuzijengea uwezo Kamati za Ukaguzi za Bunge (Baraza la Wawakilishi) kwa lengo la kuzisimamia ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kutoa ushauri na mapendekezo yao kwa taasisi za umma pamoja na  Serikali.

SURA YA PILI

MUHTASARI WA MAMBO YALIYOBAINIKA PAMOJA NA UFAFANUZI WA HATI ZA UKAGUZI

# SURA YA PILI



# 2.0 MUHTASARI WA MAMBO YALIYOBAINIKA PAMOJA NA UFAFANUZI WA HATI ZA UKAGUZI

Sura hii inaelezea muhtasari wa mambo yaliyobainika katika ukaguzi wa hesabu pamoja na ufafanuzi wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

## 2.1 Muhtasari wa mambo yaliyobainika katika ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilibainikwa uwepo wa dosari mbali mbali za kiutendaji ambazo hadi ukaguzi unakamilika hazikupatiwa majibu au majibu yake hayakuridhisha hali iliyopelekea kujitokeza kwa hoja za ukaguzi.

## 2.2 Dosari za kiutendaji zilizobainika katika Ukaguzi

Katika ukaguzi wa hesabu wa mwaka wa fedha 2022/2023 kulijitokeza dosari za kiutendaji ambazo zimepelekea kuathiri utendaji wa taasisi zilizokaguliwa pamoja na utekelezaji wa sheria mbali mbali. Dosari hizo ni kama zifuatazo:-

a) Mfumo wa udhibiti wa ndani.

b) Utekelezaji wa Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 na Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016.

c) Usimamizi wa matumizi.

d) Mifumo ya ukusanyaji wa mapato.

e) Usimamizi wa mikataba.

### a) Mfumo wa udhibiti wa ndani

Mfumo wa udhibiti wa ndani ni taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria za usimamizi wa fedha ambazo zinahitajika kuwa imara ili kuweza kusaidia taasisi za umma kuweza kufanya kazi zake kwa weledi na kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria.

Ukaguzi ulibaini dosari katika mfumo wa udhibiti wa ndani kwa baadhi ya Taasisi zilizokaguliwa kutokuwa na Kamati za Ukaguzi pamoja na kutokuwepo kwa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani au kutokufanyakazi kwa kamati hizo. Kutokufanyakazi kwa

kamati za ukaguzi (Audit Committee) kunaweza kupelekea dosari za kiutendaji kushindwa kuchukuliwa hatua za awali pale zinapojitokeza.

Aidha, ukaguzi umebaini vitengo vya ukaguzi wa ndani (Internal Audit Units) kwa baadhi ya Taasisi zilizokaguliwa hazikuwasilisha ripoti za ukaguzi wa hesabu katika kipindi cha ukaguzi pamoja na kushindwa kukutana kwa kamati za ukaguzi kwa lengo la kuzifanyia kazi ripoti za ukaguzi, hesabu za mwisho wa mwaka wa fedha zilizowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na hatimae kubainika uwepo wa dosari mbali mbali katika hesabu hizo.

### b) Utekelezaji wa Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 pamoja na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016

Katika tathmini iliyofanywa ya utekelezaji wa sheria mbali mbali kwa Taasisi za umma imebainika Maafisa Masuuli wamechukuwa jitihada za kusimamia utekelezaji wa sheria, kanuni na miongozo mbali mbali iliyotolewa katika usimamizi wa fedha na rasilimali za umma pamoja na kuwapatia mafunzo watendaji katika utekelezaji wa majukumu yao jambo ambalo limepelekea kuimarika kwa hati za ukaguzi zilizotolewa.

Aidha, pamoja na uwepo wa mafanikio makubwa zipo baadhi ya Taasisi zilibainika kukengeuka utekelezaji na usimamizi wa sheria, kanuni na miongozo mbali mbali iliyotolewa katika usimamizi wa fedha na rasilimali za uma na kupelekea baadhi ya Taasisi kuwa na dosari kubwa za kiutendaji.

### c) Usimamizi wa Matumizi

Kutokana na tathmini iliyofanyika juu ya usimamizi wa matumizi imebainika uwepo wa marekebisho makubwa yaliyofanyika kutokana na mapendekezo yaliyotolewa katika Ripoti ya Ukaguzi ya mwaka wa fedha 2022/2023 na hatimae dosari mbali mbali zilizobainishwa ziliweza kufanyiwa kazi ingawa zipo baadhi ya dosari hazikuweza kufanyiwa kazi kikamilifu kutokana na baadhi ya Taasisi kutokuwa na mfumo mzuri wa matumizi.

Kutokuwepo kwa mfumo mzuri wa usimamizi wa matumizi kunaweza kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma, ukaguzi unachukuwa fursa ya kuzinasihi baadhi ya Taasisi zilizobainishwa katika ripoti hii kuwa na usimamizi usioridhisha wa matumizi kuchukuwa jitihada za makusudi za kuhakikisha wanayafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa katika barua ya dosari za ukaguzi zilizowasilishwa katika uongozi wakati wa kikao cha kukamilika kazi za kaguzi (exit meeting).

### d) Mifumo ya Ukusanyaji wa Mapato

Kutokana na tathmini iliyofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika Mifumo ya Ukusanyaji wa Mapato imeimarishwa na kusimamiwa vizuri jambo ambalo limepelekea kuongezeka kwa ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ukilinganisha na mwaka wa fedha 2021/2022.

Aidha, imebainika uwepo wa baadhi ya Taasisi kuendelea kukusanya mapato nje ya mfumo na kupelekea baadhi ya mapato kutokuwasilishwa kwa wakati, kutokujuulikana mapato sahihi yaliyokusanywa au kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa mapato ya umma unaosababishwa na ukiukwaji wa sheria, taratibu na miongozo iliyowekwa.

### e) Usimamizi wa Mikataba

Ukaguzi umebaini dosari katika usimamizi wa mikataba kwa baadhi ya Taasisi za Serikali ikiwemo kukiuka vipengele muhimu vilivyoainishwa katika mikataba hali iliyopelekea kutokufikiwa kwa malengo yaliyopangwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kuwepo kwa ukiukwaji wa vipengele hivyo kumepelekea kwa baadhi ya miradi kutokamilika kwa wakati na kutofikia malengo yaliyokusudiwa.

Aidha, kujitokeza kwa baadhi ya Taasisi kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kutumia rasimu ya Mkataba jambo ambalo limepelekea kuitia hasara Serikali kwa kufanya malipo ya ziada kutokana na kutokuzingatia masharti ya jumla ya mikataba au kushindwa kutoza tozo ya fidia kulikosababishwa na baadhi ya wazabuni kushindwa kukamilisha kazi kwa wakati, kutokuwasilishwa kwa hati ya dhamana pamoja na baadhi ya Taasisi kushindwa kutekeleza ushauri wa kitaalamu uliotolewa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu uliowataka kufanya marekebisho ya rasimu za mikataba kabla ya utekelezaji.

## 2.3 Uwasilishaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka wa Fedha 2022/2023

Kwa mujibu wa kifungu namba 119(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016, Wizara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinatakiwa zitayarishe na ziwasilishe kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za mwisho wa mwaka ndani ya miezi mitatu baada ya kumalizika mwaka wa fedha ambapo hesabu hizo zitajumuisha taarifa za mapato na matumizi ya Taasisi hizo.

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kwamba uwasilishaji wa taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka umeimarika ingawa zipo baadhi ya Taasisi zilishindwa kuwasilisha hesabu zao kwa wakati kwa mujibu wa Sheria.

Hali ya uwasilishaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2022/2023 ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 1: Orodha ya Taasisi zilizowasilisha taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka

| Nam. | Fungu | Taasisi | Tarehe iliyowasilishwa kwa ukaguzi | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Mwaka wa fedha 2020/2021 | Mwaka wa fedha 2021/2022 | Mwaka wa fedha 2022/2023 |
| **Tawala za Mikoa** | | | | | |
| 1. | D07 | Mkoa wa Mjini Magharibi | 21/09/2021 | 14/09/2022 | 18/09/2023 |
| 2. | D08 | Mkoa wa Kusini Unguja | 20/09/2021 | 29/09/2022 | 18/09/2023 |
| 3. | D09 | Mkoa wa Kaskazini Unguja | 30/09/2021 | 28/09/2022 | 26/09/2023 |
| 4. | D10 | Mkoa wa Kusini Pemba | 28/10/2021 | 28/09/2022 | 25/09/2023 |
| 5. | D11 | Mkoa wa Kaskazini Pemba | 25/10/2021 | 25/09/2022 | 26/09/2023 |
| **Mamlaka za Serikali za Mitaa** | | | | | |
| 1. | 201 | Baraza la Jiji la Zanzibar | 27/09/2021 | 28/09/2022 | 20/09/2023 |
| 2. | 202 | Baraza la Manispaa ya Mjini | 01/09/2021 | 06/09/2022 | 29/09/2023 |
| 3. | 203 | Baraza la Manispaa Magharibi "A" | 27/09/2021 | 28/09/2022 | 29/09/2023 |
| 4. | 204 | Baraza la Manispaa Magharibi "B" | 27/09/2021 | 27/09/2022 | 27/09/2023 |
| 5. | 205 | Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "A" | 30/09/2021 | 29/09/2022 | 26/09/2023 |
| 6. | 206 | Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "B" | 30/09/2021 | 26/09/2022 | 27/09/2023 |
| 7. | 207 | Baraza la Mji Wilaya ya Kati | 22/10/2021 | 29/09/2022 | **04/10/2023** |
| 8. | 208 | Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja | 28/09/2021 | 23/09/2022 | 21/09/2023 |
| 9. | 209 | Baraza la Mji Wete | 08/11/2021 | 27/09/2022 | 29/09/2023 |
| 10. | 210 | Baraza la Manispaa Chake Chake | 30/12/2021 | 26/09/2022 | 27/09/2023 |
| 11. | 211 | Baraza la Mji Mkoani | 26/10/2021 | 27/09/2022 | **09/10/2023** |
| 12. | 212 | Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni | 24/12/2021 | 30/09/2022 | 29/09/2023 |
| **Idara Maalum za SMZ** | | | | | |
| 1. | D02 | Jeshi la Kujenga Uchumi | 30/09/2021 | 04/10/2022 | 26/09/2023 |
| 2. | D03 | Chuo cha Mafunzo | 30/09/2021 | 27/09/2022 | 29/09/2023 |
| 3. | D04 | Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo | 30/09/2021 | 30/09/2022 | 26/09/2023 |
| 4. | D05 | Kikosi cha Zimamoto na Uokozi | 22/09/2021 | 26/09/2022 | 29/09/2023 |
| 5. | D06 | Kikosi cha Valantia | 30/09/2021 | 30/09/2022 | 29/09/2023 |

## 2.4 Hati za Ukaguzi

Hati ya ukaguzi hupatikana kwa kuzingatia tathmini ya hitimisho inayotokana na ushahidi wa ukaguzi uliopatikana, kama taarifa za fedha kwa ujumla wake zimetayarishwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya uhasibu (kama vile IFRS au IPSAS). Hati ya ukaguzi hutolewa kwa mujibu wa Kiwango cha Kimataifa cha Taasisi za Juu za Ukaguzi (ISSAI 1700).

Hili linafanikiwa na kufikiwa kwa kuandaa na kufanya ukaguzi kwa namna ambayo itamuwezesha Mkaguzi kupata uhakika kuhusu tathmini ya matokeo dhidi ya kiwango cha juu kisichohimilika (Materiality) kilichowekwa.

## 2.5 Aina ya Hati za Ukaguzi

### I. Hati Inayoridhisha

Hati hii inatolewa wakati Mkaguzi anaporidhika kuwa hesabu zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu au viwango vingine vya utoaji wa taarifa za fedha vinavyokubalika.

Kama mkaguzi ataona umuhimu wa kuvuta umakini wa wasomaji wa taarifa za fedha kuhusu suala ambalo limeoneshwa au kuainishwa kwenye taarifa za fedha, na ambalo limeonekana kuwa ni muhimu na la msingi kwa ajili ya kuleta uelewa wa taarifa hizo kwa ajili ya kufanya maamuzi yenye tija atatoa **Hati Inayoridhisha Yenye Aya za Msisitizo.**

Aya hii itawekwa tu pale ambapo mkaguzi amepata vielelezo vya kutosha kuwa taarifa za fedha hazijakosewa kwa kiasi kikubwa na inatakiwa itokane na suala ambalo limeoneshwa au kuainishwa kwenye taarifa za hesabu pekee.

Kama mkaguzi ataona ipo haja ya kutoa maelezo ya ziada kwa watumiaji wa taarifa za fedha ili kuwasaidia kuelewa masuala ambayo kwa maoni ya kiweledi ya mkaguzi, yalikuwa na umuhimu mkubwa katika ukaguzi wa taarifa za fedha za taasisi husika atatoa **Aya yenye Masuala Muhimu ya Ukaguzi.**

### II. Hati Isiyoridhisha

Hati hii hutolewa pale ambapo taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka zimeshindwa kuthibitishwa kutokana na athari zilizobainika na hivyo kupelekea taarifa hizo kutoonesha sura sahihi na halisi. Hati hii imegawika katika Makundi matatu (3) ambayo ni Hati Yenye Shaka, Hati Mbaya na Kushindwa Kutoa Maoni ya Ukaguzi.

a) **Hati Yenye Shaka:** Hati hii hutolewa pale taarifa za fedha zinapokuwa zimetayarishwa kwa usahihi isipokuwa:

- Pale ambapo Mkaguzi amepata ushahidi wa kutosha wakati wa ukaguzi, akahitimisha kuwa kulikuwa na dosari ama moja moja au kwa ujumla wake, ambazo ni kubwa lakini hazijaathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha; au
- Pale ambapo Mkaguzi ameshindwa kupata ushahidi wa kutosha kumwezesha kutoa maoni ya ukaguzi, lakini akahitimisha kwamba dosari zilizotokana na kukosa ushahidi ni kubwa lakini hazijaathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha.

b) **Hati Mbaya:** Hati hii hutolewa pale ambapo Mkaguzi amepata ushahidi wa kutosha kuwa dosari moja moja au kwa ujumla zilizobainika wakati wa ukaguzi ni kubwa na zimeathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha hivyo kupelekea taarifa hizo kutokuwa sahihi.

c) **Kushindwa kutoa Maoni:** Hali hii hutokea pale Mkaguzi anaposhindwa kupata ushahidi wa kutosha utakaomuwezesha kutoa maoni ya ukaguzi. Mkaguzi atahitimisha kwamba athari zinazoweza kutokea za dosari zisizogundulika za taarifa za fedha, zinaweza kuwa kubwa na zinaweza kuathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha.

Mkaguzi atashindwa kutoa maoni, katika mazingira nadra sana yaliyohusisha mashaka kwa kiasi kikubwa, atahitimisha kwamba, ingawa amepata ushahidi wa kutosha wa ukaguzi kuhusu kila shaka, haitowezekana kutoa maoni juu ya taarifa za fedha kwa sababu ya mwingiliano wa hayo mashaka na athari zake kwenye taarifa za fedha.

## 2.6 Msingi wa Hati za Ukaguzi

Ili kufikia kwenye hati zilizotolewa, ukaguzi ulizingatia hali halisi ya matokeo ya ukaguzi kwa kila taasisi iliyokaguliwa. Ukaguzi huo ulifanyika kulingana na matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi kwenye Sekta za Umma (ISSAIs). Viwango hivyo vinanitaka kuandaa mpango wa ukaguzi, kufanya ukaguzi, na kutoa ripoti ya matokeo ya ukaguzi huo. Pia, vinanitaka kufuata maadili ya ukaguzi ili kuhakikisha kuwa ukaguzi uliofanyika una ubora unaokubalika kwa hali ya juu. Ukaguzi ulijumuisha uchunguzi wa nyaraka mbalimbali zinazohusiana na kiasi cha fedha kilichoripotiwa kwenye taarifa za fedha.

Aidha, ukaguzi ulijumuisha tathmini ya makadirio na maamuzi yaliyofanywa na uongozi wa Mawizara, Idara na Taasisi wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha, utoshelezi wa mambo yaliyoripotiwa kwenye taarifa za fedha, iwapo

sera za uhasibu zinazotumika zinaendana na mazingira halisi ya utekelezaji wa majukumu ya taasisi inayokaguliwa na kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta za Umma, na kama sera hizo zinajitosheleza na zimekuwa zikitumika mwaka hadi mwaka.

Kaguzi zilizofanyika zilipangwa na kutekelezwa kwa namna ambayo iliwezesha ukusanyaji wa taarifa zote muhimu na maelezo ya uongozi yaliyokuwa yanahitajika ili kuhakikisha upatikanaji wa kutosha wa nyaraka kwa ajili ya kutoa uhakika iwapo taarifa za fedha zilizokaguliwa hazina mapungufu makubwa yaliyosababishwa na ubadhirifu au kwa bahati mbaya.

Nilifanya ukaguzi wangu kwa uhuru na sikuwa na mgongano wa maslahi na taasisi yoyote niliyoikaguwa kwa mujibu wa kanuni za maadili zilizotolewa na Bodi ya Kimataifa ya Viwango vya Maadili kwa Wahasibu pamoja na Kanuni za Maadili zilizotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA) na nilitekeleza wajibu wangu wa kimaadili kwa mujibu wa matakwa hayo.

Ni imani yangu kuwa ushahidi nilioupata ulikuwa sahihi na ulijitosheleza katika kutoa hati za ukaguzi na pale ambapo nilishindwa kupata ushahidi wa kutosha sikutoa hati za ukaguzi.

## 2.7 Hati za Ukaguzi zilizotolewa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, jumla ya hati za ukaguzi Ishirini na Mbili **(22)** zimetolewa katika ripoti hii ambapo kati ya hati hizo, hati Kumi na Tisa **(19)** ni hati zinazoridhisha sawa na asilimia **86.36** ya hati zilizotolewa na hati Tatu **(3)** ni hati zenye shaka sawa na asilimia **13.64** ya hati zilizotolewa na hapakuwa na hati mbaya wala hati ya kushindwa kutoa maoni kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Orodha ya Taasisi zilizokaguliwa pamoja na hati za ukaguzi zilizotolewa zimeoneshwa katika jadweli lifuatalo:-

## Jadweli Nambari 2:Taasisi za Serikali zilizokaguliwa na kupata Hati za ukaguzi

| Nam. | Fungu | Taasisi | Hati za ukaguzi zilizotolewa | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Mwaka wa fedha 2020/2021 | Mwaka wa fedha 2021/2022 | Mwaka wa fedha 2022/2023 |
| **Tawala za Mikoa** | | | | | |
| 1. | D07 | Mkoa wa Mjini Magharibi | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 2. | D08 | Mkoa wa Kusini Unguja | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 3. | D09 | Mkoa wa Kaskazini Unguja | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 4. | D10 | Mkoa wa Kusini Pemba | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 5. | D11 | Mkoa wa Kaskazini Pemba | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| **Mamlaka za Serikali za Mitaa** | | | | | |
| 6. | 201 | Baraza la Jiji la Zanzibar | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 7. | 202 | Baraza la Manispaa ya Mjini | Hati Inayoridhisha | **Hati Yenye Shaka** | **Hati Yenye Shaka** |
| 8. | 203 | Baraza la Manispaa Magharibi "A" | **Hati Isiyoridhisha** | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 9. | 204 | Baraza la Manispaa Magharibi "B" | **Hati Isiyoridhisha** | Hati Inayoridhisha | **Hati Yenye Shaka** |
| 10. | 205 | Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "A" | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 11. | 206 | Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "B" | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 12. | 207 | Baraza la Mji Wilaya ya Kati | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 13. | 208 | Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | **Hati Yenye Shaka** |
| 14. | 209 | Baraza la Mji Wete | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 15. | 210 | Baraza la Manispaa Chake Chake | **Hati Isiyoridhisha** | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 16. | 211 | Baraza la Mji Mkoani | **Hati Isiyoridhisha** | Hati Inayoridhisha | **Hati Inayoridhisha yenye Aya ya Msisitizo** |
| 17. | 212 | Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| **Idara Maalum za SMZ** | | | | | |
| 18. | D02 | Jeshi la Kujenga Uchumi | **Hati Isiyoridhisha** | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 19. | D03 | Chuo cha Mafunzo | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | **Hati Inayoridhisha yenye Aya ya Msisitizo** |
| 20. | D04 | Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo | **Hati Isiyoridhisha** | **Hati Yenye Shaka** | Hati Inayoridhisha |
| 21. | D05 | Kikosi cha Zimamoto na Uokozi | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 22. | D06 | Kikosi cha Valantia | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |

## 2.8 Taarifa ya utekelezaji wa Mapendekezo ya Hoja za Ukaguzi kwa mwaka uliopita

Taarifa ya utekelezaji wa ukaguzi inaeleza kwa muhtasari hali ya utekelezaji na hatua zilizochukuliwa na Maafisa Masuuli katika kusimamia na kufuatilia mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa Taasisi za Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kiujumla hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi imeimarika ambapo baadhi ya Taasisi zimeonekana kupiga hatua katika kufanya marekebisho ya dosari zilizobainika ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 dosari hizo hazikuweza kujirejea na kwa baadhi ya Taasisi zimeweza kupunguza idadi ya hoja zilizobainishwa ukilinganisha na mwaka uliopita.

Tathmini niliyofanya kwenye hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa mwaka uliopita inaonesha kuwa, kati ya mapendekezo 512 niliyoyatoa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, mapendekezo 380 sawa na asilimia 74.22 yametekelezwa, mapendekezo 44 sawa na asilimia 8.59 yapo kwenye hatua mbali mbali za utekelezaji, mapendekezo 47 sawa na asilimia 9.18 hayajatekelezwa, mapendekezo 23 sawa na asilimia 4.49 yamejirudia na mapendekezo 18 sawa na asilimia 3.52 yamepitwa na wakati.

# SURA YA TATU


Control Environment
Control Activities
Information & Communication
Monitoring
Risk Assessment
INTERNAL CONTROL

# 3.0 TATHMINI YA MIFUMO YA UDHIBITI WA NDANI

Sura hii inaelezea tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani inayoendeshwa ndani ya Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Vile vile inaelezea mapungufu yaliyojitokeza katika tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani, pamoja na masuala ya utawala bora, Kamati za Ukaguzi na Kazi za Ukaguzi wa Ndani.

## 3.1 Matokeo ya Tathmini ya Mfumo wa Udhibiti wa Ndani

Ripoti hii inaeleza matokeo ya tathmini ya mfumo wa udhibiti wa ndani na mapendekezo pamoja na njia ambazo zinaweza kutumika katika kudhibiti na kusimamia ambapo mfumo huo unaweza kuboreshwa ili kuongeza ufanisi kwa lengo la kudhibiti vihatarishi vinavyoweza kujitokeza.

Ukaguzi wa udhibiti wa ndani ulikuwa na malengo ya kutambua mapungufu yatokanayo na utekelezaji wa matakwa ya sheria ya Uanzishwaji wa vitengo vya ukaguzi wa ndani, kamati za ukaguzi pamoja na ufanyaji kazi wa vitengo hivyo. Mambo yaliyojitokeza katika taarifa hii ni yale tu yanayotokana na ukaguzi, na ambayo tunaamini kuwa yanatakiwa kuletwa mbele ya umma. Hatuwezi kuwajibika na kuripoti vitu vyote vya vihatarishi vinavyohusiana na udhaifu wa udhibiti wa ndani.

Maafisa Masuuli pamoja na viongozi wa Serikali wanawajibika kwa masuala ya usimamizi na uendeshaji ambapo watalazimika kubainisha viashiria vya upotevu wa fedha za umma pamoja na kuvichukulia hatua za kiutendaji ili visiweze kujitokeza kwa mara nyengine, hata hivyo watakuwa na jukumu la kuhakikisha kunakuwa na udhibiti wa matumizi bora ya fedha za umma katika Taasisi zao.

### 3.1.1 Dosari za ujumla zilizobainika kwa mwaka wa fedha 2022/2023

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika uwepo wa dosari mbali mbali zinazotokana na makosa ya kiutendaji pamoja na ukiukwaji wa sheria ambapo imepelekea uwepo wa dosari hizo kujitokeza mara kwa mara kwa baadhi ya Taasisi za Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kuwepo kwa dosari hizo kunaweza kukapelekea kuharibu mtazamo wa hati za ukaguzi na hatimae taasisi kuweza kupata hati ya ukaguzi isiyoridhisha.

Baadhi ya dosari za ujumla zilizobainika kutoka katika hesabu za Taasisi hizo ni kama inavyobainishwa hapo chini:-

#### 3.1.1.1 Mapungufu katika Mfumo wa Udhibiti wa Ndani

Mifumo ya udhibiti wa ndani ni namna ambavyo rasilimali za umma zinavyopangiliwa, zinavyosimamiwa na kupimwa. Udhibiti wa ndani unatumika kama chombo muhimu katika kudhibiti ubadhirifu na matumizi mabaya ya mali za umma zinazoshikika na zisizoshikika.

Katika Taasisi yoyote lengo la mfumo wa udhibiti wa ndani ni kuhakikisha shughuli za Taasisi husika zinafanywa kwa kuzingatia miongozo na taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria na kanuni.

Ukaguzi umebaini baadhi ya Taasisi bado hazina usimamizi mzuri wa udhibiti wa ndani kwa kutokuanzisha vitengo au kwa kutokufanya kazi kwa vitengo hivyo kwa mujibu wa utaratibu, au kujitokeza dosari mbali mbali za kiutendaji ambazo zinakwaza kamati hizo kufanya kazi zake kwa mujibu wa sheria jambo ambalo linapelekea kamati za ukaguzi (Audit Committee) pamoja na kitengo cha ukaguzi wa ndani (Internal Audit Unit) kutokupitia ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za mwisho wa mwaka pamoja na kushindwa kutoa maoni ya marekebisho ya dosari na kasoro mbali mbali zilizobainishwa katika ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Ukaguzi unawashauri viongozi wa Taasisi za Umma kuhakikisha wanaweka udhibiti mzuri wa ndani ikiwemo kuvijengea uwezo vitengo vya ukaguzi wa ndani pamoja na Kamati za ukaguzi kwa kuvipatia mafunzo ya muda mfupi juu ya namna bora ya kutekeleza kazi zao. Taasisi zilizobainika kuwa na dosari hizo ni kama zinavyoonekana katika jadweli lifuatalo hapo chini:-

**Jadweli Nambari 3:Dosari za kiutendaji zilizobainika kwa vitengo vya usimamizi na udhibiti wa ndani**

| Namba | Jina la Taasisi | Dosari zilizobainika | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Kamati ya Ukaguzi | Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani | Bodi ya Zabuni |
| 1. | Baraza la Manispaa Chake Chake Pemba | -- | Kukosekana kwa Kitengo cha Ukaguzi wa ndani | -- |
| 2. | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja | Kutokufanya kazi kwa mujibu wa kanuni nambari 150(1) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021 | -- | -- |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3. | Kikosi cha Zimamoto na Uokozi | --- | Kukosekana kwa Kitengo cha Ukaguzi wa ndani | --- |
| 4. | Kikosi cha Valantia | --- | --- | Kuchelewa Kuwasilisha Mpango wa Manunuzi |

### 3.1.1.2 Ucheleweshaji wa uwasilishaji wa taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka

Kwa mujibu wa kifungu nambari 119(1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinawataka wakuu wa taasisi kutayarisha taarifa za mapato na matumizi na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya kukamilika kwa mwaka wa fedha.

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya Mashirika na Taasisi zinazojitegemea zimechelewa kuwasilisha hesabu za mapato na matumizi yanayosimamiwa na taasisi hizo kwa ajili ya ukaguzi ambapo ni kinyume na kifungu nambari 119(1) cha sheria niliyoitaja hapo juu. Kuchelewa kuwasilisha taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka kwa wakati kunapelekea kujitokeza ugumu wa kuzifanyia kazi taarifa hizo ikiwemo kuzitolea maoni ya kitaalamu kutokana na kujitokeza kwa uharaka wa kuwahi kuwasilisha taarifa zilizokaguliwa kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mujibu wa matakwa ya kifungu nambari 112(5) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984.

Ukaguzi unawashauri Maafisa Masuuli kuhakikisha wanawasilisha taarifa zao za hesabu za mwisho wa mwaka kwa wakati ili ziweze kutolewa maoni ya kitaalamu na kupelekea kuziwasilisha taarifa hizo kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mujibu wa sheria.

Baadhi ya Taasisi zilizobainika kuchelewesha kuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 4:Taasisi zilizochelewa kuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka**

| Nam. | Jina la Taasisi | Tarehe ya Uwasilishaji | |
|---|---|---|---|
| | | Mwaka wa fedha 2021/2022 | Mwaka wa fedha 2022/2023 |
| 1. | Baraza la Mji Mkoani | 27/09/2022 | 09/10/2023 |
| 2. | Baraza la Mji Wilaya ya Kati | 29/09/2022 | 04/10/2023 |

### 3.1.1.3 Kukosekana Daftari la Kuhifadhia Mali za Kudumu (Fixed Assets Register)

Kwa mujibu wa kifungu nambari 29(1)(a) (2) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kwamba "Afisa Mhasibu wa Taasisi za Umma atahusika na kusimamia mali za Taasisi ya Umma na katika kutimiza majukumu yanayohusina na usimamizi wa mali, Afisa Mhasibu atatunza daftari la mali zote zilizopo chini ya udhibiti wa Taasisi ya Umma".

Aidha, kifungu cha 58(c) cha Sheria namabari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya mwaka 2021 kinaeleza kwamba "Afisa Masuuli wa taasisi ya Umma atakuwa na jukumu la kuhifadhi na kuimarisha kila muda daftari la mali za umma kwa kujumuisha mali mpya za umma zinazopatikana na kuondosha vifaa vilivyoondolewa".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hazina daftari la kuhifadhia mali za kudumu, au kutokufanyiwa maboresho kwa daftari hilo kwa kuwekwa mali mpya na kuondolewa zilizochakaa jambo ambalo linaweza kupelekea kutokujua umiliki wake na hatimaye kupelekea kupotea kwa mali hizo.

Kukosekana daftari la kuhifadhia mali za kudumu au kutokufanyiwa maboresho kunaweza kupelekea mali zilizonunuliwa, zilizochakaa, zilizouzwa pamoja na zilizohamishwa kutokutambuliwa na kusababisha upotevu wa mali hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha unatekeleza matakwa ya Sheria nilizozinakili hapo juu ili kuepusha kujitokeza kwa vitendo vya upotevu wa mali za umma bila ya kuzibaini. Mchanganuo wa taasisi zilizobainika na dosari hizo ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 5:Taasisi zilizobainika kuwa na mapungufu katika daftari la Kuhifadhia Mali za Kudumu**

| Namba | Jina la Taasisi | Hali ya daftari iliyobainika |
|---|---|---|
| 1. | Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba | Haina |
| 2. | Baraza la Mji Wete | Halina |
| 3. | Baraza la Manispaa Chake Chake | Halina |
| 4. | Baraza la Mji Mkoani | Halina |
| 5. | Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) Pemba | Halina |
| 6. | Kikosi cha Zimamoto na Uokozi (KZU) Pemba | Hakina |
| 7. | Baraza la Manispaa ya Mjini | Halina |
| 8. | Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "A" | Halina |
| 9. | Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja | Haina |
| 10. | Kikosi cha Valantia | Halijafanyiwa maboresho |

#### 3.1.1.4 Mapungufu yaliyobainika katika daftari linaloonyesha mienendo ya safari katika vyombo vya moto (log book)

Kanuni nambari 124(2) ya Utumishi wa Umma ya 2014 inaeleza kwamba "Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi atahakikisha vyombo vyote vinavyotumika katika Taasisi yake vinakuwa na daftari linaloonyesha matumizi ya chombo kwa safari husika".

Ukaguzi umebaini kuwa vyombo vya moto vya baadhi ya taasisi za Serikali havijawekewa daftari au kutokujazwa ipaswavyo kwa daftari linaloonyesha mienendo ya safari ya vyombo hivyo hali inayopelekea kushindwa kujiridhisha juu ya matumizi ya mafuta yanayonunuliwa na kutumika jambo ambalo linapelekea kujitokeza kwa ugumu wa kujua muda sahihi wa kuweza kufanyiwa matengenezo ya chombo husika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kanuni ya Utumishi wa umma ya 2014 iliyonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unashauri viongozi wa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha wanaanzisha daftari maalum la kurikodia mwenendo wa vyombo vya moto ili kuepusha hasara inayoweza kujitokeza kutokana na kuchelewa kufanyiwa matengenezo ya vyombo hivyo kunakotokana na kukosekana kwa taarifa za mienendo ya vyombo hivyo. Dosari zilizobainika kwa Wizara na Taasisi za Umma ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 6:Taasisi zilizokosa buku linaloonyesha mienendo ya safari katika vyombo vya moto (log book)**

| Namba | Jina la Taasisi | Hali ya daftari iliyobainika |
|---|---|---|
| 1. | Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba | Haijaanzishwa |
| 2. | Baraza la Mji Wete | Halijaanzishwa |
| 3. | Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "A" | Halijaanzishwa |
| 4. | Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "B" | Halijaanzishwa |
| 5. | Baraza la Mji Wilaya ya Kati | Halijaanzishwa |
| 6. | Kikosi cha Valantia Zanzibar | Hakijaanzisha |

#### 3.1.1.5 Kutokuwepo kwa bajeti ya mapato na matumizi kwa baadhi ya Taasisi za Serikali Pemba

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika baadhi ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa upande wa Pemba zinatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa matakwa ya Sheria, Kanuni na Miongozo zinazosimamia Taasisi hizo.

Ukaguzi umebaini uwepo wa changamoto mbali mbali zinazozikabili taasisi hizo ambazo zinapelekea kutokuwa na ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yao na hatimae kutokufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa kutokana na kukosekana kwa bajeti halisi ya ya mapato na matumizi katika uendeshaji wa shughuli za taasisi hizo.

Miongoni mwa dosari zinazozikumba taasisi hizo ni kama zifuatazo:-

- Kutokuwepo kwa mpango wa utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwa mujibu wa bajeti ya taasisi hizo.
- Kukosa muelekeo wa utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwa mwaka husika kutokana na kutokujuwa thamani halisi ya fedha inayoweza kupatikana katika kusimamia shughuli iliyopangwa.
- Kutumiwa fedha za matumizi ya kazi za kawaida kwa baadhi ya taasisi ikiwemo matumizi ya mafuta, umeme, vifaa vya kuandikia kwa njia ya miamala ya simu (Tigo Pesa, Ezy Pesa, Airtel Money) au kupitia hesabu za watu binafsi jambo ambalo ni kinyume na utaratibu wa miongozo ya fedha za umma.

Kuwepo kwa dosari hizo kunaweza kupelekea kutokufikiwa kwa lengo la utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa ufanisi uliokusudiwa.

Ukaguzi unawashauri Maafisa Masuuli wa Taasisi hizo kuwasiliana na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuchukuwa jitihada za kulitafutia ufumbuzi suala hilo ili kunusuru uwezekano wa kujitokeza kwa upotevu wa fedha za umma kutakakosababishwa na baadhi ya watumishi waliokosa uaminifu. Mchanganuo wa Taasisi zisizokuwa na bajeti ya mapato na matumizi ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 7:Taasisi zisizokuwa na bajeti ya mapato na matumizi**

| Namba | Jina la Taasisi | Hali halisi iliyobainika |
|---|---|---|
| 1. | Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) | Kukosekana kwa bajeti ya mapato na matumizi ya shughuli za uendeshaji. |
| 2. | Kikosi Maalum cha Kuzuwia Magendo (KMKM) | |
| 3. | Chuo cha Mafunzo (MF) | |
| 4. | Kikosi cha Zimamoto na Uokozi (KZU) | |
| 5. | Kikosi cha Valantia (KVZ) | |

### 3.1.1.6 Dosari zilizobainika katika mfumo wa MUTM pamoja na vifaa vya kukusanyia mapato (POS)

Katika kuimarisha usimamizi wa makusanyo wa mapato ya Taasisi za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatumia mfumo wa "MUTM" katika zoezi zima la ukusanyaji mapato yanayotokana na vianzio mbalimbali vilivyoainishwa kwenye Sheria na Kanuni. Aidha, mfumo huo umeanzishwa kwa lengo la kupunguza mianya ya upotevu wa fedha za umma na kutanuwa wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Taasisi za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Kifungu nambari 30(2) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kwamba "Afisa Mhasibu kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha kifungu hiki, atachukua hatua zinazofaa kuhakikisha uanzishaji na uendeshaji mfumo bora na wa ufanisi wa ukusanyaji na uhifadhi wa mapato".

Ukaguzi umebaini dosari katika mfumo ambao unatumika kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato kama ifuatavyo:-

- Mfumo hautoi taarifa za mchanganuo wa kila kianzio cha mapato yaliokusanywa. Hali hii imepelekea ukaguzi kushindwa kujiridhisha na mapato ya kila kianzio yaliokusanywa kupitia mfumo huo.
- Kukosekana kwa ripoti za mfumo zinazoonyesha uhalisia wa fedha zilizokusanywa kwa kutumia "POS" yanayotokana na vianzio vya mapato hayo.
- Kukosekana kwa taarifa ya tathmini inayotokana na mfumo wa ukusanyaji mapato. Taarifa hii itasaidia kufanyika kwa maboresho pale panapoonekana kuwa na mapungufu.
- Kukosekana kwa taarifa za ukusanyaji mapato kutoka kwenye mfumo maalum uliowekwa "MUTM". Hii imepelekea kutopatikana kwa taarifa za mapato ya miezi hiyo kwa ukaguzi.
- Kukosekana kwa kumbukumbu za taarifa "backup" ya stakabadhi zilizotumika katika ving'amuzi (POS) vya ukusanyaji wa mapato.

- Kutowiana kwa fedha za makusanyo baina ya mfumo, madaftari ya mapato na fedha zilizowasilishwa benki.
- Kujiongeza fedha kwa makusanyo ya POS.
- Kutolipika kwa baadhi ya "Control Number".
- Kuwepo kwa utofauti wa "Control Number" zilizolipwa na kusoma hazijalipika.
- Kutojulikana kwa idadi halisi ya stakabadhi zinazotolewa na POS badala ya kuingizwa kwa karatasi za "Roller".
- Kukosekana kwa uhalisia wa mapato yaliokusanywa kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023.

Kwa mujibu wa dosari zilizoainishwa hapo juu, ukaguzi umebaini kwamba Taasisi za Mamlaka za Serikali za Mitaa hazina mfumo bora na wa ufanisi wa ukusanyaji na uhifadhi wa kumbukumbu zinazohusiana na mapato kama Sheria ilivyoelekeza.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuchukua hatua za kufanya maboresho ya mfumo pamoja na POS kwa lengo la kuziba mianya ya upotevu wa mapato ili kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya Taasisi za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mchanganuo wa taasisi zilizobainika kuwa na dosari hizo ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 8:Taasisi zilizobainika na dosari katika mfumo wa MUTM pamoja na vifaa vya kukusanyia mapato (POS)**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Baraza la Mji Wete |
| 2. | Baraza la Manispaa Chake Chake |
| 3. | Baraza la Mji Mkoani |
| 4. | Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni |
| 5. | Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "A" |
| 6. | Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "B" |

### 3.1.1.7 Kutokuwepo kwa Daftari la Kuwekea Kumbu Kumbu za Mikataba (Contract Register)

Kanuni ya 47 ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaeleza kwamba "Afisa Mhasibu anatakiwa aweke daftari la mkataba lenye kufanyiwa marekebisho kwa mikataba yote walioingia kwa mwaka wa fedha husika".

Ukaguzi umebaini kwamba kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kuwepo kwa dosari

kwa baadhi ya Taasisi kutokuwepo/kutokufanyiwa maboresho kwa daftari la kuwekea kumbukumbu za mikataba kwa ajili ya kutekeleza shughuli za miradi jambo ambalo linaweza kupelekea uwezekano wa kupotea kwa kumbu kumbu muhimu za miradi au shughuli za Afisi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kuhakikisha kwamba zinaanzisha daftari la kuwekea kumbu kumbu za mikataba kwa mujibu wa matakwa ya kisheria. Mchanganuo wa Taasisi hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 9:Dosari za kutokuwepo/kutokufanyiwa maboresho kwa daftari la kumbukumbu za mikataba**

| Namba | Jina la Taasisi | Kutokufanyiwa Maboresho | Kutokuwepo kwa Daftari |
|---|---|---|---|
| 1. | Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba | | ✓ |
| 2. | Baraza la Mji Wete | | ✓ |
| 3. | Baraza la Manispaa Chake Chake Pemba | | ✓ |
| 4. | Baraza la Mji Mkoani | | ✓ |
| 5. | Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni | | ✓ |
| 6. | Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "B" | | ✓ |

### 3.1.1.8 Dosari katika Kamati ya Ukaguzi

Kwa mujibu wa kifungu nambari 118(1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kuwa Kila Taasisi inayohusika na bajeti ya Serikali itakuwa na kamati ya ukaguzi wa ndani itakayoteuliwa na Afisa Mhasibu kwa kushauriana na Mlipaji Mkuu wa Serikali. Aidha, kanuni ya 149 ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021 inaelezea majukumu ya Kamati.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa dosari mbali mbali katika Kamati ya Ukaguzi kwa baadhi ya Taasisi. Dosari wenyewe ni kama zifuatazo:-

a) Kukosekana kwa barua za uteuzi wa wajumbe wa kamati.

b) Kamati za ukaguzi hazikupitia ripoti za ukaguzi zilizotolewa na Mkaguzi wa Ndani pamoja na wakaguzi wa nje kinyume na kanuni ya 149(2)(b) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za mwaka 2021.

c) Afisi haikuwapatia mafunzo ya awali wajumbe wake wapya wa kamati za ukaguzi ili kuwa na uelewa juu ya majukumu yao ikiwemo mafunzo ya maeneo muhimu kama vile usimamizi wa ununuzi, usimamizi wa vihatarishi n.k.

d) Kamati hazikufanya tathmini ya vihatarishi kwenye shughuli za uendeshaji wa kila siku za Afisi kinyume na kanuni ya 149(2)(i) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za mwaka 2021.

e) Kamati hazikuandaa na kuwasilisha taarifa za mwaka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama inavyoelezwa chini ya kanuni ya 149(2)(n) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma za mwaka 2021.

f) Kutokufanyika kwa vikao vya kamati za ukaguzi kinyume na kanuni ya 150(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za mwaka 2021.

g) Kamati za Ukaguzi hazikujifanyia tathmini ya kazi zake jambo ambalo ni kinyume na kifungu nambari 120(3)(h) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Kuwepo kwa dosari hizi kunaweza kupelekea malengo ya kuundwa kwa kamati za ukaguzi kutokufikiwa ambapo pia ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu pamoja na Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2021 nilizozinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kuhakikisha kamati za ukaguzi zinatekeleza majukumu yake kwa ufanisi ikiwemo kupatiwa mafunzo stahiki pamoja na kutengewa bajeti ya utekelezaji wa majukumu yao kwa mujibu wa sheria na kanuni zinavyoelekeza. Mchanganuo wa Taasisi zilizokuwa na dosari hizo ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 10:Taasisi zenye dosari za kiutendaji za Kamati za Ukaguzi**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba |
| 2. | Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba |
| 3. | Baraza la Manispaa ya Chake Chake Pemba |
| 4. | Baraza la Mji Mkoani |
| 5. | Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni |
| 6. | Jeshi la Kujenga Uchumi |

### 3.1.1.9 Kutokukamilika kwa taratibu za kuwaombea ajira ya kudumu watumishi wa kutwa

Kwa mujibu wa kanuni ya 135 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014, inaeleza kuwa hakutakiwi kuwepo kwa wafanyakazi wa kutwa katika Utumishi wa Umma na kama kuna ulazima wa kuwepo Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi atalazimika kuomba kibali kwa Tume ya Utumishi husika na kumjazisha mkataba, ambapo mtumishi wa utumishi wa kutwa hatozidi miezi sita.

Ukaguzi umebaini katika mwaka wa fedha 2022/2023 baadhi ya Taasisi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa na watumishi wa kutwa ambao wanatumika katika shughuli mbali mbali za Mamlaka hizo zikiwemo za ulinzi wa vituo vya afya katika maeneo tofauti pamoja na kufanya usafi wa mji. Baadhi ya wafanyakazi hao wametumikia kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitano (5) na wamekuwa ni chachu katika kuzilinda na kuzitunza rasilimali za Taasisi. Ukaguzi ulishindwa kupata ithibati ya kuwepo kwa kibali cha uajiri kutoka Tume ya Utumishi Serikalini kwa ajili ya kupata idhini. Hali hii inaweza ikapelekea kujitokeza kwa migogoro isiyo ya lazima pindipo mtumishi wa kutwa atakapokosa sifa za uajiri wa kudumu au kujitokeza kwa uajiri wa mtumishi asiyekuwa na maadili mema.

Kuwatumia watumishi wa ajira za kutwa kwa muda mrefu ni kwenda kinyume na Kanuni za utumishi wa Umma za mwaka 2014 kama nilivyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kufuatilia vibali vya ajira ili kuweza kuwaajiri katika ajira ya kudumu wale wote wanaoweza kuajirika kisheria. Mchanganuo wa watumishi wa kutwa walioajiriwa bila kibali ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 11:Watumishi wa kutwa walioajiriwa bila ya Kibali**

| Namba | Jina | Nafasi ya kazi |
|---|---|---|
| **Baraza la Mji Wete** | | |
| 1. | Ashura Khamis Ali | Wasafishaji Baraza la Mji Wete. |
| 2. | Khadija Ali Hamad | |
| 3. | Abdalla Ali Hamad | |
| 4. | Hamad Khamis Omar | |
| 5. | Ali Shaib Ali | |
| 6. | Sharif Ali Omar | |
| 7. | Sada Moh’d Salum | |

| | | |
|---|---|---|
| 8. | Omar Suleiman Omar | Walinzi katika vituo vya Afya. |
| 9. | Ali Abas Jecha | |
| 10. | Yunus Swaleh Rashid | |
| 11. | Amour Khamis Salim | |
| 12. | Abdulsattar Massoud Hamad | |
| 13. | Said Shaaban Rashid | |
| 14. | Mbarouk Khamis Makame | |
| 15. | Seif Talib Bakar | |
| 16. | Khamis Omar Khamis | |
| 17. | Khalfan Salim Khamis | |
| **Baraza la Mji Mkoani** | | |
| 18. | Khamis Silima Ali | Mlinzi Kituo cha Afya Mwambe Shamiani |
| 19. | Abdulrahman Salum Ali | Mlinzi Kituo cha Afya Kisiwa Panza |
| 20. | Moh'd Salim Ali | Mlinzi Kituo cha Afya Makoongwe |

### 3.1.1.10 Kutokuwepo kwa nyaraka zinazothibitisha umiliki wa mali

Kifungu namba 64(1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba "Taasisi ya umma itahifadhi nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali".

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya Taasisi za Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinamiliki mali za aina mbali mbali zikiwemo Masoko, Chinjio, Diko pamoja na Jengo la Afisi bila ya kuwa na nyaraka zinazothibitisha umiliki halali wa mali hizo.

Kutokuwepo kwa nyaraka zinazothibitisha umiliki halali wa mali kunaweza kupelekea kutokea kwa migogoro baina ya Taasisi hizo na wananchi, upotevu, wizi na matumizi mabaya ya mali za umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kwamba mali zote wanazomiliki wanazipatia nyaraka za umiliki. Mchanganuo wa mali za Taasisi hizo ambazo zimekosa nyaraka zinazothibitisha umiliki halali ni kama unavyoonekana katika jadweli lifuatalo: -

## Jadweli Nambari 12: Mali za Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizokosa nyaraka za umiliki

| Namba | Aina ya Mali | Idadi | Mahali Ilipo |
|---|---|---|---|
| **Baraza la Mji Wete** | | | |
| 1. | Jengo la Afisi Ndogo Bahanasa | 1 | Bahanasa |
| 2. | Soko la Matunda Wete | 1 | Wete Sokoni |
| 3. | Ukumbi wa Jamhuri | 1 | Wete Line |
| 4. | Chinjio | 1 | Selemu |
| 5. | Diko | 1 | Selemu |
| 6. | Jengo la Afisi | 1 | Kitutia Wete |
| 7. | Soko la Samaki Gando | 1 | Gando |
| 8. | Soko la Samaki Mtemani | 1 | Mtemani - Wete |
| 9. | Milango ya Maduka | 45 | Sokoni - Wete |
| **Baraza la Manispaa Chake Chake** | | | |
| 10. | Soko la Tibirinzi | 1 | Tibirinzi - Chake Chake |
| 11. | Soko la Matunda | 1 | Chake Mjini |
| 12. | Soko la Ole Kianga | 1 | Ole Kianga |
| 13. | Chinjio | 1 | Wesha |
| 14. | Diko | 1 | Ndagoni na Kichuani |
| 15. | Maduka | 36 | Chake Chake Sokoni |
| **Baraza la Mji Mkoani** | | | |
| 16 | Soko la Samaki na Matunda | 1 | Mbuyuni Mkoani |
| 17. | | 1 | Kangani |
| 18. | | 1 | Mkanyageni |
| 19. | Chinjio | 1 | Jaalani Mkoani |
| 20. | Ukumbi wa Umoja ni Nguvu | 1 | Wilayani Mkoani |
| 21. | Jengo la Afisi | 1 | Makadara Mkoani |
| 22. | Soko Kongwe | 1 | Msikiti wa Ijumaa Kengeja |
| 23. | Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani | 1 | Mtambile |
| **Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni** | | | |
| 24. | Soko la mboga mboga Micheweni | 1 | Micheweni |
| 25. | Soko la samaki Wingwi | 1 | Wingwi |
| 26. | Soko la Wajasiri amali | 1 | Tumbe |
| 27. | Kiwanja | 1 | Wingwi Mapofu |
| 28. | Stand ya daladala | 1 | Kinowe Konde |
| 29. | Diko la Msuka | 1 | Msuka |
| 30. | Diko la Kiuyu Mbuyuni | 1 | Kiuyu Mbuyuni |
| 31. | Diko la Shumba Mjini | 1 | Shumba Mjini |

### 3.1.1.11 Kutokukatiwa Bima kwa Vyombo vya Usafiri

Kwa mujibu wa kanuni 124(5) ya kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2014, Mkuu wa Taasisi anatakiwa kuhakikisha kuwa vyombo vya usafiri vya Serikali vilivyo chini ya mamlaka yake vinapasishwa na kukatiwa bima.

Ukaguzi umebaini kuwa baadhi ya Taasisi zinamiliki vyombo mbalimbali vya usafiri ikiwemo gari, piki piki na vespa ambapo baadhi ya vyombo hivyo vinatumika bila ya kukatiwa bima. Hali hii imetokana na Taasisi hizo kutoweka kipaombele cha ukataji wa bima kwa vyombo vya usafiri. Kutokukatiwa bima kwa vyombo vya usafiri kunaweza kuisababishia Serikali kupata hasara ya utumiaji wa fedha kwa matengenezo pindipo vyombo hivyo vikipata ajali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kuhakikisha kwamba inaweka kipaombele cha ukataji wa bima kwa vyombo vya usafiri ili kunusuru kujitokeza kwa gharama zisizokuwa za lazima pale chombo kinapopata ajali. Mchanganuo wa vyombo hivyo ni kama unavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 13:Vyombo vya usafiri ambavyo havijakatiwa Bima**

| Namba | Aina ya Chombo | Mahali Ilipo | Nambari ya Chombo |
|---|---|---|---|
| **Afisi ya Mkuu wa Mkoa Kaskazini Pemba** | | | |
| 1. | Gari ya Hilux | Afisi ya Mkuu wa Wilaya Micheweni | SMZ 1027C |
| 2. | Vespa | Afisi Kuu ya Mkoa wa Kaskazini Pemba | SMZ 1174C |
| 3. | | | SMZ 1534C |
| 4. | | | SMZ 210C |
| 5. | | Afisi ya Mkuu wa Wilaya Micheweni | SMZ 1205C |
| 6. | | | SMZ 1437 |
| 7. | | Afisi ya Wilaya ndogo Kojani | SMZ 297C |
| 8. | Pikipiki Boxer | Afisi Kuu ya Mkoa wa Kaskazini Pemba | SMZ 1788C |
| 9. | | Afisi ya Mkuu wa Wilaya Wete | SMZ 1789C |
| **Afisi ya Baraza la Manispaa Chake Chake** | | | |
| 10. | Prado | Afisi ya Baraza la Manispaa Chake Chake | SMZ 943 A |
| 11. | Pick Up | | SMZ 362 B |
| 12. | Fuso | | SMZ 490 B |
| 13. | Vespa | | SMZ 382 C |
| 14. | | | SMZ 383 C |
| 15. | | | SMZ 565 C |
| 16. | | | SMZ 712 C |
| **Afisi ya Baraza la Mji Mkoani** | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 17. | Prado Land Cruiser | Afisi ya Baraza la Mji Mkoani | SMZ 819 A |
| 18. | Mitsubishi Fuso | | SMZ 452 B |
| 19. | Vespa | | SMZ 196 C |
| 20. | | | SMZ 195 C |
| 21. | Pikipiki TVS | | SMZ 2102 C |
| 22. | | | SMZ 2103 C |
| **Afisi ya Halmashauri ya Wilaya Micheweni** | | | |
| 23. | Prado | Afisi ya Halmashauri ya Wilaya Micheweni | SMZ 971 A |
| 24. | Vespa | | SMZ 993 C |
| 25. | | | SMZ 1447 C |
| 26. | | | SMZ 707 C |
| 27. | | | SMZ 1348 C |
| 28. | Pikipiki | | SMZ 1938 C |
| **Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) Zoni ya Pemba** | | | |
| 29. | Trector | JKU Pemba | JKU 069 |
| 30. | NISSAN SAFAR | | JKU 079 |
| 31. | TATA | | JKU 084 |
| 32. | TATA | | JKU 085 |
| 33. | Toyota RAV4 | | JKU 089 |
| 34. | TRECTOR | | JKU 109 |
| 35. | Land Cruser Prado | | JKU 140 |
| 36. | Mazda | | JKU 141 |
| 37. | Suzuki Carry | | JKU 142 |
| 38. | Toyota Coaster | | JKU 150 |
| **Chuo cha Mafunzo** | | | |
| 39. | FUSO | Chuo cha Mafunzo Pemba | MF.1024 |
| 40. | Toyota Hiace | | MF.1009 |
| 41. | | | MF.1021 |
| 42. | | | MF.1022 |
| 43. | Landrover | | MF.1014 |
| **Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM)** | | | |
| 44. | Land Cruiser | Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Pemba | KM 083 |
| 45. | Fuso Refu | | KM 084 |
| 46. | Fuso Fupi | | KM 089 |
| 47. | Hilux | | KM 098 |
| 48. | Toyota Rav4 | | KM 151 |
| 49. | Prado | | KM 560 |
| **Kikosi cha Zimamoto na Uokozi (KZU)** | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 50. | Toyota | Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Pemba | KZU 240 |
| 51. | Pickup | | KZU 217 |
| 52. | Canter | | KZU 218 |
| 53. | ISUZU | | KZU 223 |
| 54. | Armarok | | KZU 280 |
| 55. | ISUZU | | KZU 246 |
| 56. | Nissan | | KZU 248 |
| 57. | Canter | | KZU 261 |
| 58. | Scania | | KZU 265 |
| 59. | Man | | KZU 278 |
| 60. | Nissan | | KZU 230 |
| 61. | ISUZU | | KZU 260 |
| **Kikosi cha Valantia (KVZ)** | | | |
| 62. | Prado | Kikosi cha Valantia (KVZ) Pemba | KVZ 128 |
| 63. | Canter | | KVZ 108 |
| 64. | Nissan | | KVZ 114 |
| 65. | Toyota Rav 4 | | KVZ 112 |
| 66. | Vespa | | KVZ 121 |
| 67. | Honda Boxer | | KVZ 122 |
| 68. | | | KVZ 123 |
| 69. | | | KVZ 124 |
| **Baraza la Manispaa ya Magharibi "B"** | | | |
| 70. | Faw | Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" | SMZ 435 B |
| 71. | Faw | | SMZ 434 B |
| 72. | Fuso | | SMZ 140 B |
| 73. | Fuso | | SMZ 472 B |
| 74. | Compactor | | SMZ 573 B |
| 75. | Canter | | SMZ 151 B |
| 76. | Wheel Loader | | SMZ 163 B |
| 77. | Trekta | | T 472 DPJ |
| 78. | Harrier | | SMZ 725 A |
| 79. | Pick Up | | SMZ 699 B |
| 80. | Town Ace | | SMZ 973 B |
| 81. | Pick Up | | SMZ 116 B |
| 82. | Pick Up | | SMZ 447 B |
| 83. | Pick Up | | SMZ 413 B |
| 84. | Corolla | | Z 347 FC |
| **Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "A"** | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 85. | Toyota Prado | Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "A" | SMZ 9822A |
| 86. | Suzuki Escudo | | SMZ 899A |
| 87. | Pickup | | SMZ 601 A |
| 88. | Fuso | | SMZ 489 B |
| 89. | Hiace | | SMZ 985 A |
| 90. | Mitsubishi | | SMZ 403 B |
| 91. | Honda | | SMZ 1900 C |
| 92. | Honda | | SMZ 1999 C |
| 93. | Vespa | | SMZ 708 C |
| **Baraza la Mji Wilaya ya Kati** | | | |
| 94. | Canter | Baraza la Mji Wilaya ya Kati | SMZ 494 A |
| 95. | Canter | | SMZ 380 B |
| 96. | Coaster | | SMZ 5892 |
| 97. | Canter | | SMZ 455 B |
| **Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja** | | | |
| 98. | Toyota Prado 2009 | Katibu Tawala Mkoa | SMZ 470 A |
| 99. | Toyota Prado TX 2008 | Mkuu wa Mkoa | SMZ 858A |
| 100. | Toyota Prado 2007 | Mkuu wa Wilaya ya Kati | SMZ 928A |
| 101. | Toyota Landcruiser 2006 | Mkuu wa Wilaya ya Kusini | SMZ 926A |
| 102. | Vespa Star 2011 | Mkoa – Mwanasheria | SMZ 745C |
| 103. | | Mkoa – Katibu wa RC | SMZ 334C |
| 104. | | Mkoa – Dereva wa RC | SMZ 1177C |
| 105. | Honda TVS 2019 | Mkoa – Tarishi | SMZ 1885C |
| 106. | Vespa | Wilaya ya Kati Afisa Mipango | SMZ 1019C |
| 107. | | Wilaya ya Kati Mshika fedha | SMZ 562C |
| 108. | | Wilaya ya Kati Msaidizi wa Katibu Tawala | SMZ796C |
| 109. | | Wilaya ya Kusini | SMZ 417C |
| **Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja** | | | |
| 110. | Basi Toyota Coaster | Afisi Kuu ya Mkoa wa Kaskazini | Z 1072 A |
| 111. | Suzuki Escudo | | SMZ 743 A |
| 112. | Vespa | | SMZ 1519 C |
| 113. | Nissan | Afisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini 'B' | SLS 139 A |
| 114. | Nissan | Afisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini 'A' | SMZ 126 A |
| 115. | Vespa | | SMZ 1520 C |
| 116. | Hyundai | | SMZ 138 A |
| 117. | Boti Fiber | Wilaya ndogo Tumbatu | -- |
| **Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi** | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 118. | Land Cruiser | Makao makuu – Mkoa | SMZ 991 A |
| 119. | | Wilaya ya Mjini | SMZ 993 A |
| 120. | Land Cruiser Prado | Makao makuu – Mkoa | SMZ 1148 A |
| 121. | | Wilaya ya Magharibi 'A' | SMZ 1060 A |
| 122. | Vespa | Wilaya ya Mjini | SMZ 1427 C |
| 123. | | | SMZ 1479 C |
| 124. | | Wilaya ya Magharibi 'A' | SMZ 1304 C |
| 125. | | | SMZ 1480 C |
| 126. | | Mkoa | SMZ 437 C |
| 127. | Honda Click | Wilaya ya Magharibi 'A' | SMZ 1887 C |
| 128. | | Mkoa | SMZ 1614 C |
| 129. | Pikipiki | | SMZ 1776 C |
| 130. | Hyundai | Wilaya ya Mjini | SMZ 451 A |
| 131. | Toyota Rav 4 | | SMZ 707 A |

### 3.1.1.12 Ununuzi wa vifaa vya kuandikia kwa watoa huduma mbali mbali bila ya kupata idhini kutoka Wakala wa Uchapaji shilingi 20,971,998

Kifungu nambari 35(1) cha Sheria ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar ya mwaka 2018 kinazitaka taasisi za Umma kufanya ununuzi wa vifaa vya kuandikia kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika jumla ya shilingi 20,971,998 zilitumiwa kwa ajili ya huduma kwa baadhi ya Taasisi za Umma, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokufanyika kwa manunuzi ya vifaa vya kuandikia kutoka kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji, aidha imebainika kwamba ununuzi wa vifaa hivyo umefanywa kwa watoa huduma wengine bila ya kupatiwa idhini na Wakala wa Serikali wa Uchapaji (ZAGPA).

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuidumaza Wakala na kushindwa kuendelea kutoa huduma zinazostahiki, aidha ni kwenda kinyume na Sheria ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar ya mwaka 2018.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kununua vifaa vya kuandikia kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar au kuomba ridhaa ya kufanya manunuzi kwa watoa huduma wengine ikiwa hawatokuwa na uwezo wa kusambaza vifaa husika. Mchanganuo wa vifaa hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 14: Ununuzi wa vifaa vya kuandikia kwa watoa huduma wengine**

| Hati Namba | Hundi Namba | Thamani (Tsh.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| **Afisi ya Baraza la Manispaa Chake Chake** | | | | |
| 12/09 ya 08/09/2022 | TT | 1,485,739 | Pemba Digital Printing. | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia kwa matumizi ya Afisi ya Baraza la Manispaa Chake Chake. |
| 19/11 ya 02/11/2022 | | 5,686,528 | | |
| 42/01 ya 24/01/2023 | | 109,486 | | |
| 44/01 ya 24/01/2023 | | 513,814 | | |
| 7/05 ya 08/05/2023 | | 1,846,628 | | |
| 18/06 ya 6/6/2023 | | 345,882 | | |
| 21/06 ya 6/6/2023 | | 345,882 | | |
| **Jumla Ndogo (A)** | | **10,333,959** | | |
| **Afisi ya Baraza la Mji Mkoani** | | | | |
| 036 ya 14/08/2022 | TISS | 2,756,348 | Pemba Digital Printing | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia kwa matumizi ya Afisi ya Baraza la Mji Mkoani. |
| 033 ya 14/8/2022 | | 3,366,800 | Africom Limited | |
| 211PV23000140 ya 26/10/2022 | | 1,397,432 | FAA Stationary | |
| 161 ya 14/11/2022 | | 3,117,459 | Malinge Enterprise Pemba | |
| **Jumla Ndogo (B)** | | **10,638,039** | | |
| **Jumla Kuu (A+B)** | | **20,971,998** | | |

*Chanzo: Ukaguzi wa Hati za malipo*

### 3.1.1.13 Kukosekana kwa Mkataba wa Huduma kwa Umma

Kwa mujibu wa kanuni nambari 37(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014 inaelezea kwamba "Kila taasisi italazimika kuandaa mkataba wa huduma kwa umma".

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya Taasisi za Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinatoa huduma mbali mbali bila ya kuwepo kwa mkataba wa huduma kwa umma unaoelezea ni kwa namna gani Mamlaka zinatoa huduma kwa wateja wake.

Kutokuwepo kwa mkataba wa huduma kwa umma kunapelekea kuwanyima wataka huduma taarifa za kina zinazohusiana na Mamlaka, kutojulikana kwa huduma zinazotolewa na Mamlaka pamoja na kuwepo kwa ugumu wa mawasiliano

ya upatikanaji wa taarifa za Mamlaka. Hali hii imesababishwa na kutokuzingatiwa kwa Sheria na Kanuni mbali mbali za Serikali.

Kutokuwepo kwa mkataba wa huduma kunapelekea kuwanyima wataka huduma taarifa za kina zinazohusiana na Mamlaka, kutojulikana kwa huduma zinazotolewa pamoja na kupelekea ugumu wa mawasiliano ya upatikanaji wa taarifa za Taasisi husika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha unaandaa mkataba wa huduma kwa umma ili kurahisisha mawasiliano katika jamii katika kuzijua na kupata huduma zilizo bora na kwa urahisi zaidi. Mchanganuo wa Taasisi hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 15:Taasisi ambazo hazikuandaa Mkataba wa Huduma kwa Umma**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Baraza la Mji Wete |
| 2. | Baraza la Mji Mkoani |
| 3. | Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni |

### 3.1.1.14 Kutokuwepo kwa Kitengo cha usimamizi wa mali pamoja na Mpango wa matengenezo wa Mali za Taasisi za Umma

Kwa mujibu wa kifungu 59(1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba "Kutakua na kitengo cha usimamizi wa mali katika kila taasisi ya Umma".

Aidha, kwa mujibu wa kifungu nambari 66 cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba "Kutakuwa na mpango wa matengenezo wa mali utakaoandaliwa na Taasisi ya Umma unaohakikisha kwamba mali zinabaki katika ubora kwa matumizi yaliyokusudiwa.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kutokuwepo kwa kitengo cha Usimamizi wa Mali pamoja na mpango wa matengenezo wa mali ambao unaoonesha utaratibu mzima wa kuzifanyia matengenezo mali/vifaa vinavyomilikiwa na kutumika kwa shughuli za Taasisi jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa uharibifu mkubwa wa mali na hatimae kupelekea kutumia gharama kubwa ya matengenezo au kuwepo kwa upotevu wa mali za Taasisi husika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kuanzisha Kitengo cha Usimamizi wa Mali pamoja na uandaaji wa mpango wa matengenezo wa mali hizo ili kuepusha uwezekano wa kutokea kwa

uharibifu wa mali za Taasisi. Mchanganuo wa Taasisi zenye dosari hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 16:Taasisi zisizokuwa na Kitengo cha Usimamizi wa Mali pamoja na Mpango wa matengenezo wa Mali zinazomilikiwa na Afisi**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Baraza la Manispaa ya Mjini |
| 2. | Baraza la Manispaa ya Magharibi "A" |
| 3. | Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" |
| 4. | Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "A" |
| 5. | Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "B" |
| 6. | Baraza la Mji Wilaya ya Kati |
| 7. | Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja |
| 8. | Baraza la Manispaa Chake Chake |
| 9. | Baraza la Mji Mkoani |
| 10. | Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni |

### 3.1.1.15 Dosari katika matengenezo ya gari shilingi 55,389,580

Kwa mujibu wa kanuni ya 124(3) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inaeleza kuwa 'Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi atahakikisha vyombo vyote vilivyomo katika taasisi yake vinafanyiwa matengenezo katika Karakana Kuu ya Serikali au sehemu (gereji) zitakazothibitishwa na Serikali".

Ukaguzi umebaini kuwa jumla ya shilingi 55,389,580 zimetumiwa na Taasisi mbali mbali za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya matengenezo ya vyombo vya moto katika gereji binafsi bila ya kupatiwa idhini kutoka kwa Wakala wa Karakana Kuu ya Serikali. Hali hii imetokana na kutokufuatwa ipaswavyo kwa Sheria na kanuni za Serikali pamoja na afisa manunuzi kutokuwa na uwelewa wa kutosha juu ya utaratibu huu jambo ambalo linaweza kupelekea kufanyika kwa matengenezo ya vyombo vya moto bila ya kuzingatiwa vigezo na pia uwezekano wa kutokea kwa matengenezo hewa ya magari pamoja na ununuzi wa vipuri vya magari visivyohitajika na pasipo kuzingatia thamani halisi ya fedha au kukidhi vigezo vinavyostahiki. Aidha, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Kanuni ya Utumishi wa Umma niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mpango maalum utakaohakikisha vyombo vyote vya moto vya Taasisi hizo vinakaguliwa na Wakala wa Karakana Kuu ya Serikali kabla ya kufanyiwa matengenezo ili kupata idhini iwapo matengenezo hayo yako nje ya uwezo wa Karakana.

Mchanganuo wa gharama za ununuzi wa vipuri pamoja na utengenezaji wa gari katika gereji binafsi ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 17:Malipo ya matengenezo ya magari katika gereji binafsi

| Hati Namba | Hundi Namba | Thamani (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| **Baraza la Manispaa Chake Chake** | | | | |
| 26/7 ya 27/07/2022 | TT | 1,349,362 | Nourbhai Auto Services | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya matengenezo ya gari SMZ 362B. |
| 27/7 ya 27/07/2022 | | 273,750 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya Today SMZ 1675C. |
| 28/7 ya 27/07/2022 | | 4,014,472 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya gari SMZ 570B. |
| 29/7 ya 27/07/2022 | | 504,210 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya gari SMZ 944A. |
| 5/9 ya 08/09/2022 | | 370,714 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa wa vifaa vya gari SMZ 943A. |
| 18/9 ya 13/09/2022 | | 793,800 | Tahfif Auto Work | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufanyia matengenezo ya gari SMZ 944A. |
| 20/9 ya 13/09/2022 | | 1,509,200 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufanyia matengenezo ya gari SMZ 362B. |
| 22/9 ya 13/09/2022 | | 332,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa betri kwa matengenezo ya gari SMZ 944A. |
| 8/10 ya 17/10/2022 | | 2,381,400 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufanyia matengenezo ya gari SMZ 570B. |
| 14/11 ya 02/11/2022 | | 1,499,400 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa kava za viti za magari. |
| 6/12 ya 8/12/2022 | | 2,006,870 | | Malipo ya fedha kwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya magari kwa matengenezo ya gari SMZ 362B, SMZ 944A na SMZ 570B. |

| Hati Namba | Hundi Namba | Thamani (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 43/01 ya 24/1/2023 | | 579,479 | Vista Auto Parts | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya magari kwa matengenezo ya gari SMZ 570B. |
| 45/01 ya 24/01/2023 | | 1,022,609 | Tahfif Auto Parts | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya magari kwa matengenezo ya gari SMZ 570B. |
| 46/01 ya 24/01/2023 | | 166,149 | Nourbhai Auto Services | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya Piki piki SMZ 2013C. |
| 47/01 ya 24/01/2023 | | 707,305 | Tahfif Auto Work | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya matenegenezo ya Gari SMZ 943A. |
| 48/01 ya 24/01/2023 | | 230,496 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa kioo cha gari SMZ 362B. |
| 49/01 ya 24/01/2023 | | 850,434 | Nourbhai Auto Services | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya matengenezo ya gari SMZ 490B. |
| 45/03 ya 28/03/2023 | TT | 1,597,827 | Tahfif Auto Work | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya matenegenezo ya gari SMZ 362B. |
| 47/03 ya 28/03/2023 | | 409,044 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa ball joint kwa matengenezo ya gari SMZ 943A. |
| 52/03 ya 28/03/2023 | | 1,448,696 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya matengenezo ya gari SMZ 570B SINO TRUCK. |
| 3/05 ya 08/05/2023 | | 2,454,262 | Tahfif Auto Work | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya matengenezo ya gari SMZ 943A. |
| 7/06 ya 13/06/2023 | | 2,859,044 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya magari kwa matengenezo ya gari SMZ 570B na SMZ 362B. |
| 10/06 ya 13/06/2023 | | 824,478 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya gari SMZ 362B. |
| 11/06 ya 13/06/2023 | | 524,939 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya services kwa gari SMZ 570B. |
| **Jumla Ndogo (A)** | | **28,709,940** | | |
| **Baraza la Mji Mkoani** | | | | |

| Hati Namba | Hundi Namba | Thamani (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 032 ya 14/08/2022 | TISS | 897,974 | Nourbhai Auto Services | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na matengenezo ya gari za Ofisi ya Baraza la Mji Mkoani. |
| 042 ya 14/08/2022 | | 1,392,580 | Muhammed Mfaume Abdalla | |
| 031 ya 17/08/2022 | | 196,000 | Tahfif Alluminium and Glass Workshop. | |
| 067 ya 09/09/2022 | | 2,151,296 | Muhammed Mfaume Abdalla. | |
| 187 ya 24/11/2022 | | 377,349 | Tahfif Alluminium and Glass Workshop. | |
| 188 ya 24/11/2022 | | 4,921,600 | | |
| 224 ya 22/12/2022 | | 4,417,840 | Mohammed Mfaume Abdalla. | |
| 277 ya 20/02/2023 | | 1,498,224 | | |
| 327 ya 23/03/2023 | | 2,160,900 | Nourbhai Auto Services. | |
| 383 ya 11/05/2023 | | 2,028,364 | | |
| **Jumla Ndogo (B)** | | **20,042,127** | | |
| **Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni** | | | | |
| 9/8 ya 16/8/2022 | TISS | 378,240 | Ngoto Auto Accessories | Malipo ya ununuzi wa vifaa vya kufanyia service ya Gari SMZ 917A |
| 18/9 ya 19/9/2022 | | 1,723,200 | | Malipo ya ununuzi wa vifaa vya kufanyia service ya gari kwa ajili ya matumizi ya Ofisi |
| 2/12 ya 14/12/2022 | | 1,152,942 | | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa mipira |
| 2/3 ya 2/3/2023 | | 2,897,391.56 | Nourbhai Auto Service | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa pikipiki |
| 1/6 ya 01/06/2023 | | 485,739.13 | Ngoto Auto Accessories | Malipo ya fedha kwa ajili ya matengenezo ya gari DFPA 7030 |
| **Jumla Ndogo (C)** | | **6,637,513** | | |
| **Jumla Kuu (A+B+ C)** | | **55,389,580** | | |

*Chanzo: Hati za malipo*

#### 3.1.1.16 Kutokuondolewa au kufanyiwa matengenezo kwa Gari chakavu

Kifungu nambari 69(1)(2) cha Sheria namba 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya mwaka 2021 kinaeleza kwamba "Kutakuwa na Mpango wa uondoaji wa mali wa mwaka utakaoandaliwa na kila taasisi ya Umma na kuwasilishwa katika Ofisi ya Msajili wa Hazina. Taasisi ya Umma itaomba ruhusa kutoka katika ofisi kwa ajili ya kuondoa mali za Umma".

Ukaguzi uliofanyika umebaini kuwa baadhi ya mali za kudumu zinazomilikiwa na baadhi ya Taasisi za Idara Maalum za SMZ kama vile magari hayatumiki, yametelekezwa na pia hayajafanyiwa matengenezo kwa muda mrefu. Hali hii imetokana na kukosekana kwa mpango rasmi wa matengenezo wa magari pamoja na uhaba wa fedha zinazotengwa kwa ajili ya matengenezo ya magari hayo jambo ambalo linaweza kupelekea gari hizo kushuka thamani na kutia hasara Serikali.

Kutokuzifanyia matengenezo au kuomba ruhusa ya kuziondoa gari chakavu ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi za Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutayarisha mpango rasmi wa matengenezo wa magari pamoja na kutenga fedha za kutosha katika bajeti zao za mwaka. Mchanganuo wa gari chakavu ambazo hazijafanyiwa matengenezo au kuondolewa ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 18:Gari ambazo hazijafanyiwa matengenezo kwa muda mrefu**

| Namba | Aina ya Gari | Nambari ya Usajili | Kipindi kilichokaa | Mahala Ilipo |
|---|---|---|---|---|
| **Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU)** | | | | |
| 1. | Suzuki Escudo | JKU 143 | Miezi 6 | Afisi Kuu Pemba |
| 2. | Land Rover | JKU 104 | Miaka 04 | |
| 3. | Isuzu | JKU 073 | Miaka 13 | |
| 4. | Nissan Safari | Z 290 | | |
| **Chuo cha Mafunzo (MF)** | | | | |
| 5. | TATA | MF.6735 | Mwaka 1 | Afisi Kuu Pemba |
| 6. | Prado | MF | Miezi 8 | |
| 7. | Toyota Hilux | MF.1027 | Miezi 6 | |
| 8. | Toyota Rav4 | MF.6804 | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM)** | | | | |
| 1. | TATA Refu | KM 134 | Muda Mrefu | Afisi Kuu Pemba |
| 2. | TATA Fupi | KM 149 | | |
| 3. | Toyota Rav4 | KM 151 | | |
| 4. | Land Rover | KM 154 | | |
| **Kikosi cha Zimamoto na Uokozi (KZU)** | | | | |
| 1. | TATA | KZU 196 | Muda mrefu | Chanjaani Pemba |
| 2. | Columbus | KZU 222 | | |
| 3. | TATA | KZU 195 | | |
| 4. | Ditroity | SMZ 6923 | | |
| **Kikosi cha Valantia (KVZ)** | | | | |
| 1. | TATA | KVZ 107 | Miaka 7 | Afisi Kuu Pemba |
| 2. | Rav4 | KVZ 112 | Miaka 2 | |
| 3. | Toyota Hilux | KVZ 125 | Mwaka 1 | |
| 4. | Vespa | KVZ 121 | | |
| **Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi** | | | | |
| 1. | Land Cruiser | SMZ 992 A | Muda Mrefu | Wilaya ya Magharibi 'B' |
| 2. | Hyundai | SMZ 452 A | | |
| 3. | Prado | SMZ 742 A | | |
| 4. | Hyundai | SMZ 181 A | | Mkoa |
| 5. | Prado Land Cruiser | T 243 DJT | | |

*Chanzo: Ripoti ya Afisa Usafiri*

### 3.1.1.17 Kutokufikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa mapato

Kifungu nambari 30 (1-4) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 kinamtaka "Afisa masuuli kuwajibika kwa uwezo wake wote katika suala la usimamizi katika ukusanyaji wa mapato"

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba baadhi ya Taasisi za Umma hazikufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kuligana na bajeti jambo ambalo limepelekea kuathiri utekelezaji wa kazi walizojipangia.

Kutokufikiwa kwa ukusanyaji wa mapato wa vyanzo vya ndani kumetokana na baadhi ya Taasisi kuwa na mifumo duni ya ukusanyaji wa mapato au kutokutoa kipaombele cha uhamasishaji wa malipo yatokanayo na vyanzo vyao vya mapato au kuwa na ubunifu duni wa uanzishwaji wa vyanzo vipya vya ukusanyaji wa mapato pamoja na kushindwa kuvisimamia vyanzo hivyo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi za umma kuongeza umakini katika ukusanyaji wa mapato ikiwemo kuwapatia elimu watumishi wanaoshughulikia ukusanyaji wa mapato pamoja na kuhamasisha wananchi njia bora ya kuchangia mapato ya Serikali ikiwemo kubuni njia bora zaidi zitakazohakikisha kuwa mapato yanakusanywa kikamilifu na kuibua vyanzo vipya vya mapato ili kuhakikisha zinafikia malengo yaliyowekwa. Miongoni mwa taasisi hizo ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 19: Taasisi ambazo hazikufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato ya vyanzo vya ndani kwa mwaka wa fedha 2022/2023**

| Namba | Jina la Taasisi | Makadirio ya Makusanyo (Tsh.) | Makusanyo Halisi (Tsh.) | Asilimia ya Makusanyo (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Baraza la Manispaa ya Mjini | 5,252,940,000 | 3,738,771,962.00 | 71.17 |
| 2. | Baraza la Mji Wete | 500,000,000 | 362,914,156 | 72.58 |
| 3. | Baraza la Manispaa Chake Chake | 847,705,450 | 596,419,420 | 70 |
| 4. | Baraza la Mji Mkoani | 566,650,000 | 371,474,665 | 65.66 |
| 5. | Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni | 420,000,000 | 265,166,330 | 63.1 |
| 6. | Baraza la Manispaa ya Magharibi “A” | 1,900,000,000 | 1,477,405,381.62 | 77.76 |
| 7. | Baraza la Manispaa ya Magharibi “B” | 2,640,000,000 | 1,954,953,000 | 74.05 |
| 8. | Baraza la Mji Wilaya ya Kati | 1,600,000,000 | 1,137,246,362 | 71 |
| 9. | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja | 45,248,000 | 21,391,002 | 47.28 |
| 10. | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja | 37,859,123 | 9,320,000 | 24.62 |
| 11. | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi | 75,800,767 | 26,803,602 | 35.36 |
| 12. | Kikosi cha Zimamoto na Uokozi | 113,200,000.00 | 73,450,000.00 | 64.89 |

### 3.1.1.18 Kukosekana kwa hatimiliki za mali za Taasisi

Kifungu nambari 64(1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba “Taasisi ya Umma itahifadhi nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali”.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa mali nyingi kwa baadhi ya Taasisi za Umma ambazo hazina hati miliki, miongoni mwa mali hizo ni baadhi ya majengo ya Ofisi, vyombo vya moto pamoja na viwanja jambo ambalo linaweza kupelekea upotevu wa mali hizo kutokana na Taasisi hizo kutokuwa na umiliki halali, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi za Umma kuongeza juhudi za kufanya ufuatiliaji wa upatikanaji wa hatimiliki zinazohusiana na mali hizo ili kuepusha kuingia katika migogoro isiyokuwa ya lazima. Mchanganuo wa mali hizo kwa baadhi ya Taasisi za Umma ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 20:Mali za Taasisi ambazo hazina hati miliki**

| Namba | Aina ya Mali | Mahala ilipo |
|---|---|---|
| **Baraza la Manispaa ya Mjini** | | |
| 1. | Soko la Kuku | Darajani |
| 2. | Soko la Kibandamaiti | Kibandamaiti |
| 3. | Soko la Samaki | Malindi |
| 4. | Jengo la Manispaa | Malindi |
| 5. | Saaten Workshop | Saateni |
| 6. | Soko Kuu la Biashara | Darajani |
| 7. | Choo cha Africa house | Hurumzi |
| 8. | Choo cha Mnazi Mmoja | Mnazi Mmoja |
| 9. | Maduka 12 ya Biashara | Darajani |
| **Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja** | | |
| 10. | Ardhi | Kitogani |
| 11. | Ardhi | Kitogani |
| 12. | Ardhi | Kitogani |
| 13. | Ardhi | Kibuteni |
| 14. | Ardhi | Makunduchi |
| 15. | Kiwanja cha Kufurahishia Watoto | Mtule |
| 16. | Stendi ya Gari | Michamvi |
| 17. | Soko la Mboga Mboga | Muyuni |
| **Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi** | | |
| 18. | Rav 4 - SMZ 323 A | Wilaya ya Magharibi 'A' |
| 19. | Land Cruiser Prado - SMZ 927 A | |
| 20. | Land Cruiser - SMZ 992 A | Wilaya ya Magharibi 'B' |
| 21. | Hyundai - SMZ 452 A | |
| 22. | Rav 4 - SMZ 6781 A | |
| 23. | Prado - SMZ 742 A | |

| | | |
|---|---|---|
| 24. | Prado Land Cruiser - T 243 DJT | Mkoa |
| 25. | Hyundai - SMZ 181 A | |
| 26. | Vespa - SMZ 1374 C | |

### 3.1.1.19 Kukosekana kwa vifaa vya huduma ya kwanza

Kanuni ya 125(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inaeleza kuwa Kila Mkuu wa Taasisi atalazimika kuhakikisha ndani ya Taasisi yake kunakuwa na upatikanaji wa huduma ya kwanza ya afya na vifaa vya huduma ya kwanza kwa watumishi. Aidha, kifungu nambari 85 cha Sheria nambari 8 ya Afya na Usalama Kazini ya 2005 kinazitaka Taasisi "Kuweka vifaa vya zimamoto pindi janga litakapotokea".

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya Taasisi za Umma zimeshindwa kuandaa utaratibu wa upatikanaji wa vifaa vya huduma ya kwanza (First Aid) pamoja na vifaa vya kuzimia moto (Fire extinguisher) pindi inapotokea dharura kwa watumishi na mali za Ofisi. Hali hii inaweza kusababisha kutokea kwa hasara kubwa pindipo pakitokea janga la moto au mtumishi kupata ajali akiwa kazini.

Kutokuweka vifaa vya huduma ya kuzimia moto na huduma ya kwanza ndani ya majengo ya Afisi ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kufanya jitihada za kuandaa utaratibu wa upatikanaji wa vifaa vya huduma ya kwanza kwa lengo la kulinda usalama wa wafanyakazi kwa kufuata utarabibu wa Sheria na Kanuni zilizoekwa.

Orodha ya Taasisi zilizokosa vifaa vya huduma ya kwanza ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 21:Taasisi ambazo hazina vifaa vya huduma ya kwanza**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "A" |
| 2. | Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "B" |
| 3. | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja |
| 4. | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi |

#### 3.1.1.20 Kukosekana kwa Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi (Risk Management Framework)

Kwa mujibu wa kanuni nambari 154, 155 na 156 za Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021, Afisa Masuuli wa Taasisi ya Umma anapaswa kutengeneza, kutekeleza na kuimarisha Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi (Risk Management Framework). Aidha, Afisa Masuuli anapaswa kuhakikisha kuwa ripoti za usimamizi wa vihatarishi (risk management reports) zinawasilishwa katika kamati ya ukaguzi angalau mara nne (4) kwa mwaka.

Ukaguzi umebaini kuwa baadhi ya Taasisi za Umma bado hazina Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi (Risk management Framework) sambamba na kukosa kuwasilishwa ripoti za usimamizi wa vihatarishi katika kamati ya ukaguzi. Hali hii inaweza kupelekea Taasisi kushindwa kutambua na kuingiza katika mikakati na mipango ya Taasisi vihatarishi vilivyopo na vinavyoweza kuwepo katika utendaji kazi wa Taasisi hizo ikiwemo vihatarishi vya kisheria (legal risks), vihatarishi vya uhalifu mitandaoni (cyber security risks), na vihatarishi vya mazingira ya utendaji kazi (operational risks).

Kutokuanzisha, kutekeleza na kuimarisha Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi ni kwenda kinyume na kanuni nambari 154, 155 na 156 za Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kuhakikisha unaanzisha, unatekeleza na kuimarisha Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi (Risk Management Framework) kwa mujibu wa Kanuni kama zilivyonakiliwa hapo juu. Orodha ya Taasisi ambazo hazina Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 22:Taasisi ambazo hazina Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Baraza la Manispaa ya Mjini |
| 2. | Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "A" |
| 3. | Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "B" |
| 4. | Baraza la Mji Wilaya ya Kati |
| 5. | Mkoa wa Kusini Unguja |

### 3.1.1.21 Kutokuandaliwa au kutokufanyiwa maboresho kwa Mpango Mkakati (Strategic Planning)

Mpango Mkakati ni mfumo wa maandishi unaonyesha kazi zinazotakiwa kufanywa na hatua mbalimbali za kufikia malengo ya muda mrefu yaliyowekwa kwa muda wa kipindi cha miaka mitatu au miaka mitano kwa lengo la kuleta ufanisi katika taasisi husika. Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya Taasisi za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 zimeshindwa kufanya maboresho kwa mpango Mkakati wa taasisi zao na baadhi ya taasisi kuonekana kutokuandaa kabisa Mpango Mkakati (strategic plan).

Kwa mujibu wa kanuni nambari 11(c) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaeleza ya kwamba utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayosimamiwa na Taasisi za Umma inapaswa kuendana na Mpango Mkakati wa Taasisi husika.

Kutokuandaliwa au kufanyiwa maboresho ya mara kwa mara kwa Mpango Mkakati wa Taasisi kunaweza kupelekea kutopatikana kwa udhibiti na ufuatiliaji wa vipaumbele vinavyohitajika kufanywa na Taasisi jambo ambalo linaweza kupelekea kutekelezwa miradi ambayo haiendani sambamba na Mpango Mkuu wa Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Taasisi hizo kusimamia kwa karibu uandaaji na uboreshaji wa Mpango Mkakati kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kazi kutokana na malengo yaliyokusudiwa. Mchanganuo wa Taasisi zilizoshindwa kuaandaa au kuboresha Mpango Mkakati ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 23:Taasisi za Serikali zilizoshindwa kuandaa au kuboresha Mpango Mkakati**

| Namba | Jina la Taasisi | Hali halisi ya Mpango Mkakati |
|---|---|---|
| 1. | Baraza la Mji Wilaya ya Kati | Haujafanyiwa Maboresho |
| 2. | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja | Haujaandaliwa |

### 3.1.1.22 Kutokuwepo kwa Mpango Mkakati wa Kukabiliana na Maafa

Kanuni nambari 120(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inamtaka "Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi kuhakikisha kwamba kunakuwepo kwa vifaa vya awali vya kukabiliana na maafa na pia kunakuwepo kwa Mpango Mkakati wa Kukabiliana na Maafa kwa kila taasisi au Wizara".

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya Taasisi za Umma hazijaandaa Mpango Mkakati ambao utasimamia na kutoa muongozo wa jinsi ya kukabiliana na Maafa pindipo yatakapotokea. Aidha, ukaguzi umebaini kuwepo kwa baadhi ya dosari kama zifuatazo:-

- Taasisi hazijateua maafisa maalum ambao watasimamia utekelezaji na ufuatiliaji wa udhibiti wa maafa. Hii ni kwenda kinyume na kanuni nambari 120(3) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inayoeleza kwamba "Taasisi zote za umma zitaanzisha na kuweka Afisa maalum kwa madhumuni ya kuhakikisha utekelezaji na ufuatiliaji wa udhibiti wa maafa katika taasisi zao".
- Taasisi hazijatenga fungu maalum la fedha ambalo litatumika kwa ajili ya kukabiliana na maafa pale yatakapotokea. Hii ni kukiukwa kwa kanuni nambari 120(4) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inayoeleza kwamba "Katika kuhakikisha kwamba mpango wa Taifa wa kukabiliana na maafa unatekelezwa kila taasisi itahakikisha kwamba katika mipango yake kunatengwa fungu maalum kwa ajili ya kukabiliana na maafa".
- Watendaji wa Taasisi kutokupatiwa mafunzo ya jinsi ya kukabiliana na maafa pale yatakapotokea. Hii ni kwenda kinyume na kanuni nambari 120(5) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inayoeleza kwamba "Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi atahakikisha kuwa watumishi wote wa taasisi yake wanafahamu mpango na taratibu zote za kukabiliana na maafa na wanapata fursa ya kuhudhuria mafunzo ya kukabiliana na maafa".

Kutokuwepo kwa mpango Mkakati wa Kukabiliana na Maafa kunapelekea:

- Ukiukwaji wa Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014.
- Kuwepo kwa ugumu wa kujinusuru na kukabiliana na maafa pale yatakapotokea.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Taasisi hizo kuhakikisha kwamba unachukua hatua za haraka za kuanzisha Mpango Mkuu wa Kukabiliana na Maafa ambao utasaidia katika kurekebisha changamoto mbalimbali zinazotokana na maafa hayo pamoja na kuwapatia mafunzo na elimu watendaji juu ya kukabiliana na maafa kwa lengo la kupata uwelewa na kujua hatua za kuchukua pindipo maafa yakitokea ili kupunguza madhara yatokanayo na maafa hayo.

Mchanganuo wa Taasisi zilizokuwa hazina Mpango wa Kukabiliana na Maafa ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 24:Taasisi ambazo hazina Mpango wa Kukabiliana na Maafa**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Baraza la Manispaa ya Mjini |
| 2. | Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" |
| 3. | Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "A" |
| 4. | Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja |

### 3.1.1.23 Kukosekana kwa Mpango wa likizo (leave roaster)

Kwa mujibu wa kanuni ya 58(1)(a) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inaeleza kuwa 'Mtumishi wa umma atastahiki kupewa likizo la siku ishirini na nane za kazi ndani ya miezi kumi na mbili na atastahiki posho la likizo kila baada ya miaka mitatu au kama itakavyofafanuliwa katika matoleo kutoka Afisi Kuu ya Utumishi wa Umma.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba baadhi ya Taasisi za Umma hazikuandaa Mpango wa likizo wa mwaka ambao utasaidia katika kutoa dira kwa maofisa na wapiganaji kuweza kutambua siku wanayopaswa kwenda likizo ili waweze kujipanga katika kuweka sawa majukumu ya kazi pamoja na kukabidhi majukumu hayo kwa watendaji wengine, aidha kutokuwepo kwa mpango wa likizo kunarejesha nyuma mipango ya taasisi katika kuweza kutambua idadi ya watumishi wanaopaswa kwenda likizo kwa mwaka husika sambamba na kujua watumishi ambao watapatiwa huduma za malipo ya likizo kwa mujibu wa kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kuhakikisha unasimamia na kutekeleza matakwa ya sheria juu ya uandaaji wa mpango wa likizo kwa maofisa na wapiganaji wa Kikosi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao na hatimae kupatikana kwa tija iliyokusudiwa. Mchanganuo wa Taasisi ambazo hazijaandaa mpango wa likizo ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 25:Taasisi ambazo hazijaandaa Mpango wa likizo**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar |
| 2. | Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar |

SURA YA NNE

MAANDALIZI YA BAJETI NA UTEKELEZAJI WAKE

# SURA YA NNE



# 4.0 MAANDALIZI YA BAJETI NA UTEKELEZAJI WAKE

Sura hii inaelezea utekelezaji wa mipango na bajeti za Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ukusanyaji na matumizi yenye ufanisi wa fedha zlizopatikana kutokana na mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani, ruzuku kutoka Serikali Kuu pamoja na misaada kutoka kwa wadau wa maendeleo.

## 4.1 Mtizamo wa Jumla wa Bajeti

Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinatakiwa kuandaa taarifa za kibajeti zinazoonesha kiasi cha mapato kinachotarajiwa kupokelewa, kiasi cha mapato kinachotarajiwa kutolewa katika mwaka wa fedha husika na kukiwa na ulazima Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaweza kupitisha bajeti za ziada katika mwaka husika.

Kwa mujibu wa kitabu cha bajeti (MTEF) kwa kawaida huandaliwa kila mwaka kwa kulinganisha miaka miwili inayofuatana ili kuona kama inaendana na mpango wa maendeleo wa miaka mitano, sera pamoja na mikakati ya kitaifa. Ukaguzi wa bajeti katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umeonesha mapungufu mbali mbali kama ilivyoelezwa hapo chini:-

### 4.1.1 Mwenendo wa Mapato ya Ndani ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa

Mapato ya ndani yanajumuisha kodi za ndani, ada, tozo, ushuru, vibali vya ujenzi na mapato mengineyo. Fedha hizi hutumika kuongezea ruzuku iliyotolewa na Serikali Kuu na Washirika wa Maendeleo.

#### (a) Tawala za Mikoa

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 Taasisi tano (5) za Tawala za Mikoa zilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 80,140,004 kutoka katika vyanzo vya ndani ikilinganishwa na bajeti ya shilingi 243,476,856 ambapo ilionesha upungufu wa mapato kwa kiasi cha shilingi 163,336,852 sawa na asilimia 67.08 ya upungufu wa bajeti iliyoidhinishwa.

#### (b) Mamlaka za Serikali za Mitaa

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya Mamlaka tisa (9) kati ya Mamlaka kumi na mbili (12) za Serikali za Mitaa zilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 11,583,299,018.62 kutoka katika vyanzo vya ndani ikilinganishwa na

bajeti ya shilingi 15,545,595,450 ambapo ilionesha upungufu wa mapato kwa kiasi cha shilingi 3,962,296,431.38 sawa na asilimia 25.49 ya upungufu wa bajeti iliyoidhinishwa.

Aidha, jumla ya Mamlaka mbili (2) kati ya Mamlaka kumi na mbili (12) za Serikali za Mitaa zilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 2,970,249,713.2 kutoka katika vyanzo vya ndani ikilinganishwa na bajeti ya shilingi 1,925,260,000 ambapo ilionesha ziada ya mapato kwa kiasi cha shilingi 1,044,989,713.2 sawa na asilimia 54.28 ya ziada ya bajeti iliyoidhinishwa.

Kutokana na mchanganuo uliobainishwa hapo juu unamaanisha ya kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja na Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "A" yanaonekana kuwa na ufanisi mkubwa katika usimamizi na ufuatiliaji wa ukusanyaji wa mapato ikilinganishwa na Mamlaka nyengine tisa (9) ambazo zinaonekana kukosa ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.

Aidha, ukaguzi umebaini Taasisi moja ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa haikupangiwa bajeti ya makusanyo yatokanayo na vyanzo vya ndani, hivyo ukaguzi unashauri Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha inalitizama kwa kina suala la uwepo wa bajeti ya makusanyo ili taasisi hiyo iweze kutoa huduma kwa jamii na kuweza kujiendesha wenyewe kwa mujibu wa dhana ya Serikali ya kulianzisha Baraza la Jiji la Zanzibar.

### (c) Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 Taasisi nne (4) za Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zilikusanya jumla ya shilingi 586,243,350 kutoka katika vyanzo vya ndani ikilinganishwa na bajeti ya shilingi 2,385,107,401 ambapo ilionesha kukosekana kwa ufanisi katika ukusanyaji wa mapato jambo ambalo limepelekea kuwepo kwa upungufu mkubwa wa mapato yaliyokusanywa kwa kiasi cha shilingi 1,798,864,051 sawa na asilimia 75.42 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Aidha, ukaguzi umebaini Taasisi moja ya Idara Maalum ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haikupangiwa bajeti ya makusanyo yatokanayo na vyanzo vya ndani, hivyo ukaguzi unashauri Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha inalitizama kwa kina suala la uwepo wa bajeti ya makusanyo ili taasisi hiyo iweze kutoa huduma ikiwemo huduma za ulinzi na nyenginezo kwa njia ya ukusanyaji wa mapato ili iweze kutekeleza baadhi ya mipango yake iliyojipangia na kuacha kutegemea bajeti ya Serikali kwa asilimia mia moja (100). Mchanganuo wa taarifa hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

## Jadweli Nambari 26:Mtazamo wa Jumla wa Bajeti

| Namba | Fungu | Jina la Taasisi | Makadirio ya Makusanyo (Tshs) | Makusanyo Halisi (Tshs) | (Upungufu)/ Ongezeko (Tshs) | Asilimia ya (Up-ungufu)/ Ongezeko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Tawala za Mikoa** | | | | | | |
| 1. | D07 | Mkoa wa Mjini Magharibi | 75,800,767 | 26,803,602 | (48,997,165) | 64.64 |
| 2. | D08 | Mkoa wa Kusini Unguja | 45,248,000 | 21,391,002 | (23,856,998) | 52.72 |
| 3. | D09 | Mkoa wa Kaskazini Unguja | 37,859,123 | 9,320,000 | (28,539,123) | 75.38 |
| 4. | D10 | Mkoa wa Kusini Pemba | 40,595,292 | 18,240,400 | (22,354,892) | 55.07 |
| 5. | D11 | Mkoa wa Kaskazini Pemba | 43,973,674 | 4,385,000 | (39,588,674) | 90.03 |
| | | **Jumla Ndogo** | **243,476,856** | **80,140,004** | **(163,336,852)** | **67.08** |
| **Mamlaka za Serikali za Mitaa** | | | | | | |
| 6. | 201 | Baraza la Jiji la Zanzibar | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 7. | 202 | Baraza la Manispaa ya Mjini | 5,252,940,000 | 3,738,771,962 | (1,514,168,038) | 28.83 |
| 8. | 203 | Baraza la Manispaa Magharibi "A | 1,900,000,000 | 1,477,405,381.62 | (422,594,618.38) | 22.24 |
| 9. | 204 | Baraza la Manispaa Magharibi "B" | 2,640,000,000 | 1,954,953,000 | (685,047,000) | 25.95 |
| 10. | 205 | Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "A" | 1,071,100,000 | 1,561,390,454.20 | 490,290,454 | 45.77 |
| 11. | 206 | Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "B" | 1,818,300,000 | 1,678,947,752 | (139,052,248) | 7.65 |
| 12. | 207 | Baraza la Mji Wilaya ya Kati | 1,600,000,000 | 1,137,246,362 | (462,753,638) | 28.92 |

| Namba | Fungu | Jina la Taasisi | Makadirio ya Makusanyo (Tshs) | Makusanyo Halisi (Tshs) | (Upungufu)/ Ongezeko (Tshs) | Asilimia ya (Up-ungufu)/ Ongezeko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 13. | 208 | Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja | 1,003,640,000 | 1,408,859,259 | 405,219,259 | 40.37 |
| 14. | 209 | Baraza la Mji Wete | 500,000,000 | 362,914,156 | (137,085,844) | 27.42 |
| 15. | 210 | Baraza la Manispaa Chake Chake | 847,705,450 | 596,419,420 | (251,286,030) | 29.64 |
| 16. | 211 | Baraza la Mji Mkoani | 566,650,000 | 371,474,655 | (195,175,345) | 34.44 |
| 17. | 212 | Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni | 420,000,000 | 265,166,330 | (154,833,670) | 36.87 |
| | | **Jumla Ndogo** | **17,620,335,450** | **14,553,548,731.82** | **(3,066,786,718)** | **17.4** |
| **Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar** | | | | | | |
| 16. | D02 | Jeshi la Kujenga Uchumi | 2,058,234,338 | 337,910,000 | (1,720,324,338) | 83.58 |
| 17. | D03 | Chuo cha Mafunzo | 125,690,855 | 102,551,500 | (23,139,355) | 18.41 |
| 18. | D04 | Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo | 87,982,208 | 72,331,850 | (15,650,358) | 17.79 |
| 19. | D05 | Kikosi cha Zimamoto na Uokozi | 113,200,000 | 73,450,000 | (39,750,000) | 35.11 |
| 20. | D06 | Kikosi cha Valantia | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | | **Jumla Ndogo** | **2,385,107,401** | **586,243,350** | **(1,798,864,051)** | **75.42** |
| | | **JUMLA KUU** | **20,248,919,707** | **15,219,932,085.82** | **5,028,987,621.18** | **24.84** |

### 4.1.2 Mwenendo wa Mapato yatokanayo na Vyanzo vya Ndani ikilinganishwa na Ruzuku

Ruzuku ya matumizi ya kawaida inahusisha fedha za uendeshaji wa shughuli za kila siku ikijumuisha malipo ya mishahara kwa watumishi, manunuzi ya vifaa na huduma mbali mbali za uendeshaji wa Taasisi ambapo chanzo kikuu cha fedha ni ruzuku ya matumizi ya kawaida kutoka Serikali Kuu na makusanyo ya ndani.

#### (a) Tawala za Mikoa

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 Taasisi tano (5) za Tawala za Mikoa zilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 80,140,004 kutoka katika vyanzo vya ndani na kuwa na matumizi ya kawaida ya shilingi 26,929,673,076 ambapo ilionesha upungufu wa mapato kwa kiasi cha shilingi 26,849,533,072 sawa na asilimia 99.70 ya ruzuku iliyotolewa.

Kutokana na taarifa iliyopo hapo juu inaonesha kwamba Taasisi tano (5) za Tawala za Mikoa zinategemea zaidi ruzuku kutoka Serikalini kwa kiwango cha asilimia 99.70 jambo ambalo linaonesha taasisi hizo hazitoweza kujiendesha pindipo Serikali itakapoziacha Mkono wa kuzipa ruzuku.

Ukaguzi unazishauri Taasisi hizo kuongeza umakini wa ukusanyaji wa mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani pamoja na kuibua vyanzo vipya vya ukusanyaji wa mapato ili ziweze kujiendesha bila ya utegemezi wa Serikali. Mchanganuo wa taarifa hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli nambari 27 hapo chini:-

#### (b) Mamlaka za Serikali za Mitaa

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 Mamlaka za Serikali za Mitaa kumi na mbili (12) zilikusanya jumla ya shilingi 14,553,548,731.82 kutoka katika vyanzo vya ndani ikilinganishwa na ruzuku kutoka Serikali ni yenye jumla ya shilingi 16,926,232,594.73 ambapo inaonesha upungufu wa mapato kwa kiasi cha shilingi 2,372,683,862.91 sawa na asilimia 14.02 ya upungufu wa ruzuku iliyotolewa.

Kutokana na Taarifa zilizobainishwa hapo juu zinaonesha kwamba jumla ya Taasisi nne (4) kati ya Taasisi kumi na mbili (12) za Mamlaka ya Serikali za Mitaa hazikuweza kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato yatokanayo na vyanzo vyake vya ndani na kubainika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 taasisi hizo kuwa na wastani wa asilimia 76 na kutegemea ruzuku kutoka Serikali Kuu jambo ambalo linaweza kupelekea uwezekano mkubwa wa kushindwa kutoa huduma kwa jamii pindipo Serikali Kuu ikisita kuzipatia ruzuku Taasisi hizo.

Ukaguzi unazishauri Taasisi hizo kuongeza umakini katika kusimamia vyanzo vyake vya mapato ikiwemo kubuni vyanzo vipya ili kuweza kuleta tija na ufanisi wa kujiendesha kwa Taasisi hizo.

Aidha, ukaguzi umebaini Baraza la Jiji la Zanzibar halikupangiwa bajeti ya makusanyo yatokanayo na vyanzo vya ndani na kupelekea kutegemea ruzuku kutoka Serikalini kwa asilimia mia moja jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya uanzishwaji wa Baraza la Jiji la Zanzibar ikilinganishwa na ufanyaji kazi wa Baraza la Jiji la nchi nyenginezo.

Ukaguzi unaishauri Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha unalitizama kwa kina suala la uwepo wa vyanzo vya mapato vitakavyosimamiwa na Baraza la Jiji la Zanzibar ili Serikali ichukuwe maamuzi ya kulipangia bajeti maalum ya makusanyo yatokanayo na vyanzo hivyo kwa lengo la kuweza kujiendesha na kujitegemea wenyewe kwa baadhi ya huduma inazozitoa. Mchanganuo wa taarifa hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli nambari 27 hapo chini:-

### (c) Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 Idara tano (5) Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 586,243,350 kutoka katika vyanzo vya ndani ikilinganishwa na ruzuku ya shilingi 131,145,917,870.55 iliyotolewa kwa Taasisi hizo ambapo ilionesha upungufu wa mapato kwa kiasi cha shilingi 130,559,674,520.55 sawa na asilimia 99.55 ya ruzuku iliyotolewa.

Aidha, ukaguzi umebaini Kikosi cha Valantia hakikupangiwa bajeti ya makusanyo yatokanayo na vyanzo vya ndani, hivyo kuendelea kutegemea ruzuku kutoka Serikalini kwa asilimia mia moja (100%) katika uendeshaji wa shughuli zake za kila siku.

Kutokana na hali hiyo kwa vile Kikosi cha Valantia kina uwezo wa kuanzisha miradi mbali mbali ya kujitegemea ikiwemo miradi ya ushoni, ufugaji, ulinzi, pamoja na miradi mengineyo kwa lengo la kuanzisha vyanzo vya mapato ya ndani ukaguzi unashauri Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuliangalia kwa kina suala la uwepo wa vyanzo vipya vya mapato na kuvibariki kwa Kikosi cha Valantia kuweza kuvisimamia na hatimae kukusanya mapato ili yaweze kusaidia upatikanaji wa huduma nyenginezo bila ya uwepo wa utegemezi wa ruzuku kwa asilimia mia moja (100%) kama ilivyo hivi sasa. Mchanganuo wa taarifa hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli nambari 27 hapo chini:-

## Jadweli Nambari 27: Taarifa ya Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ikilinganishwa na Ruzuku

| Namba | Fungu | Jina la Taasisi | Kiasi cha Ruzuku (Tshs) | Makusanyo Halisi (Tshs) | Tofauti (Tshs) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Tawala za Mikoa** | | | | | | |
| 1. | D07 | Mkoa wa Mjini Magharibi | 10,192,615,050 | 26,803,602 | 10,165,811,448 | 99.74 |
| 2. | D08 | Mkoa wa Kusini Unguja | 3,867,545,365 | 21,391,002 | 3,846,154,363 | 99.4 |
| 3. | D09 | Mkoa wa Kaskazini Unguja | 4,291,700,695 | 9,320,000 | 4,282,380,695 | 99.78 |
| 4. | D10 | Mkoa wa Kusini Pemba | 4,689,719,516 | 18,240,400 | 4,671,479,116 | 99.61 |
| 5. | D11 | Mkoa wa Kaskazini Pemba | 3,888,092,450 | 4,385,000 | 3,883,707,450 | 99.8 |
| **Jumla Ndogo** | | | **26,929,673,076** | **80,140,004** | **26,849,533,072** | **99.70** |
| **Mamlaka za Serikali za Mitaa** | | | | | | |
| 6. | 201 | Baraza la Jiji la Zanzibar | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 7. | 202 | Baraza la Manispaa ya Mjini | 3,572,538,784.09 | 3,738,771,962 | (166,233,177.91) | 4.65 |
| 8. | 203 | Baraza la Manispaa Magharibi "A" | 1,206,268,690 | 1,477,405,381.62 | (271,136,691.62) | 22.48 |
| 9. | 204 | Baraza la Manispaa Magharibi "B" | 1,564,928,065 | 1,954,953,000 | (390,024,935) | 24.92 |
| 10. | 205 | Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "A" | 1,018,079,500 | 1,561,390,454.20 | (543,310,954.20) | 53.37 |
| 11. | 206 | Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "B" | 1,018,079,500 | 1,678,947,752 | (660,868,252) | 64.91 |
| 12. | 207 | Baraza la Mji Wilaya ya Kati | 940,965,045 | 1,137,246,362 | (196,281,317) | 20.86 |
| 13. | 208 | Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja | 692,521,455 | 1,408,859,259 | (716,337,804) | 103.44 |
| 14. | 209 | Baraza la Mji Wete | 1,808,172,204.64 | 362,914,156 | 1,445,258,048.64 | 79.93 |
| 15. | 210 | Baraza la Manispaa Chake Chake | 1,780,831,208 | 596,419,420 | 1,184,411,788 | 66.51 |
| 16. | 211 | Baraza la Mji Mkoani | 1,552,273,293 | 371,474,655 | 1,180,798,638 | 76.07 |
| 17. | 212 | Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni | 1,771,574,850 | 265,166,330 | 1,506,408,520 | 85.03 |
| **Jumla Ndogo** | | | **16,926,232,594.73** | **14,553,548,731.82** | **2,372,683,862.91** | **14.02** |

| Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 16. | D02 | Jeshi la Kujenga Uchumi | 35,325,855,495 | 337,910,000 | 34,987,945,495 | 99.04 |
| 17. | D03 | Chuo cha Mafunzo | 22,503,476,150 | 102,551,500 | 22,400,924,650 | 99.54 |
| 18. | D04 | Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo | 34,440,104,449.55 | 72,331,850 | 34,367,772,599.55 | 99.79 |
| 19. | D05 | Kikosi cha Zimamoto na Uokozi | 16,881,005,386 | 73,450,000 | 16,807,555,386 | 99.56 |
| 20. | D06 | Kikosi cha Valantia | 21,995,476,390 | 0 | 21,995,476,390 | 100 |
| | | **Jumla Ndogo** | **131,145,917,870.55** | **586,243,350** | **130,559,674,520.55** | **99.55** |
| | | **JUMLA KUU** | **175,001,823,541.28** | **15,219,932,085.82** | **159,781,891,455.46** | **91.30** |

# SURA YA TANO



# 5.0 MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Katika ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kwamba mfumo wa uwekaji wa kumbukumbu na taarifa mbali mbali za hesabu ikiwemo fedha na rasilimali za umma pamoja na mfumo wa udhibiti wa ndani umekuwa ukiimarika ingawa kumejitokeza dosari za kiutendaji mbali mbali.

Katika ukaguzi huo kulijitokeza dosari za kiutendaji kwa baadhi ya Taasisi za Serikali ambapo baadhi ya dosari ziliweza kurekebishwa na kupatiwa ufafanuzi wakati wa ukaguzi, aidha baadhi ya dosari za ukaguzi hazikuweza kupatiwa ufafanuzi hadi ukaguzi unakamilika na kupelekea kujitokeza kwa hoja za ukaguzi. Matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:-

## 5.1 TAARIFA ZA UKAGUZI WA HESABU ZA TAWALA ZA MIKOA

Sura hii inaelezea matokeo ya ukaguzi wa Tawala za Mikoa ambapo jumla ya Mikoa mitano (5) ilikaguliwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023. Sura hii inaonyesha masuala muhimu yanayohitaji kushughulikiwa na Serikali, Baraza la Wawakilishi pamoja na Uongozi wa taasisi husika ili kuhakikisha ufanisi katika utendaji wa shughuli za taasisi hizo. Yafuatayo ni matokeo ya ukaguzi kwenye ukaguzi wa Tawala za Mikoa kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

### 5.1.1 FUNGU D 07 - MKOA WA MJINI MAGHARIBI

Ukaguzi wa hesabu za Mkoa wa Mjini Magharibi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.1.1.1 Kutokuwasilishwa katika Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Taarifa za fedha za Washirika wa Maendeleo shilingi 88,280,000

Muongozo namba 2 wa kufunga hesabu uliotolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa maafisa wahasibu wote (Accounting officers) umetoa maelekezo juu ya ufungaji wa hesabu za mwaka wa fedha 2022/2023.

Kipengele nambari tatu cha 'mazingatio' kwenye muongozo huo kinazitaka Taasisi zote za kibajeti (Votes na Subvotes) zinazopokea fedha kutoka kwa wahisani wa maendeleo moja kwa moja kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kupitia hesabu za Taasisi zilizopo katika Benki za Kibiashara (Commercial Banks) Taarifa za fedha zote za miradi yote zilizopokelewa katika mwaka wa fedha 2022/2023 ziwasilishwe Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kupitia Idara ya Fedha za Nje na kwa fedha zilizotumika ziwasilishwe Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kupitia Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuingizwa katika mfumo wa matumizi (EPICOR) kwa ajili ya kupitishiwa DUMMY, taarifa zote hizi ziwasilishwe kabla ya tarehe ya mwisho ya ufungaji wa mwaka wa fedha 2022/2023.

Ukaguzi umebaini kuwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi imepokea jumla ya shilingi 88,280,000 kutoka UNICEF kwa ajili ya mradi wa ulinzi wa watoto "Children Protection Program".

Dosari iliyobainika ni kutowasilishwa kwa taarifa hizo Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ambapo ni kwenda kinyume na muongozo uliotolewa na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Kutopelekwa kwa taarifa za fedha za wahisani Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kutapelekea Serikali kutojua takwimu sahihi ya fedha ilizopata kupitia wahisani wa maendeleo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi kufuata maelekezo ya ufungaji wa hesabu yanayotolewa na Serikali kupitia Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ili kuiwezesha Serikali kupata taarifa za takwimu muhimu upande wa hesabu.

### 5.1.2 FUNGU D 08 - MKOA WA KUSINI UNGUJA

Ukaguzi wa hesabu za Mkoa wa Kusini Unguja kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.1.2.1 Kukosekana kwa hatimiliki za Mali za Ofisi

Kifungu nambari 64(1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba "Taasisi ya Umma itahifadhi nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa mali nyingi za Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja ambazo hazina hati miliki, miongoni mwa mali hizo ni baadhi ya majengo ya afisi na vyombo vya moto jambo ambalo linaweza

kupelekea upotevu wa mali hizo kutokana na Ofisi kutokuwa na umiliki halali, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja kuongeza juhudi za kufanya ufuatiliaji wa upatikanaji wa hatimiliki zinazohusiana na mali hizo ili kuepusha Ofisi kuingia katika migogoro isiyokuwa ya lazima. Mchanganuo wa mali hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli nambari 28:Mali za Taasisi ambazo hazina hati miliki**

| Namba | Aina ya Mali | Mahala lilipo |
|---|---|---|
| 1. | Jengo la Afisi Kuu ya Mkuu wa Wilaya ya Kati | Mwera |
| 2. | Jengo la Afisi ya Wilaya linalotumika na Sekta mbali mbali | |
| 3. | Afisi mpya ya Mkuu wa Wilaya | |
| 4. | Jengo la Makaazi | Binguni |
| 5. | Nyumba ya wafanyakazi | Kidimni |
| 6. | Nyumba ya Makaazi ya familia Mbili | |
| 7. | Nyumba ya Makaazi ya familia Moja | |
| 8. | Afisi kuu ya Mkuu wa Wilaya ya Kusini | Makunduchi |
| 9. | Jengo jipya la makaazi ya Mkuu wa Wilaya | |

### 5.1.2.2 Kutokutumika kwa Mfumo wa ZanMalipo katika ukusanyaji wa mapato

Kwa mujibu wa kifungu nambari 30(1)(2) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016, kinaelezea "Afisa Mhasibu, kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atachukua hatua zinazofaa kuhakikisha uanzishaji na uendeshaji wa mfumo bora na wa ufanisi wa ukusanyaji na uhifadhi wa mapato. Aidha, toleo la barua yenye kumb.No.CA.319/398/01/02/19 ya tarehe 14/02/2022 kutoka kwa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar inafafanua kwamba matumizi yote ya Taasisi za Umma yafanyike kupitia Mfumo wa ZAN MALIPO".

Ukaguzi umebaini kuwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kusini Unguja haitumii mfumo wa ZanMalipo kwa kukusanya mapato kupitia vyanzo vyake mbalimbali jambo ambalo ni kwenda kinyume na sera na miongozo ya Serikali juu ya viwango bora vinavyokubalika katika utekelezaji na mifumo ya kielektroniki ili kuhakikisha kwamba mifumo hiyo inakidhi mahitaji ya watumiaji na inaongeza tija kwenye taasisi za Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja kuongeza umakini katika kusimamia sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kukusanya mapato kupitia mfumo wa ZanMalipo.

#### 5.1.2.3 Matumizi ya mafuta kwa gari za Viongozi wateule wa Rais lita 2,238

Kwa mujibu wa Muongozo wa utumiaji wa mafuta kwa magari ya viongozi wateule wa Mhe. Rais kwa kazi mbali mbali uliotolewa kwa kumbukumbu nambari CAB. 40/158/01/41 wa tarehe 25 Oktoba, 2013 umeeleza kwamba Viongozi wateule wa ngazi ya Mhe. Rais kulipwa posho la mafuta moja kwa moja katika vocha za mishahara za kila Taasisi kupitia nambari ya hesabu ya muhusika (Personal Account Number) na si katika matumizi mengineyo (Other Charge) ya Wizara/ Taasisi. Hivyo, viongozi waliotajwa katika toleo hapo juu ni wale Wateuliwa wa Mhe. Rais tu na si kwa wale waliopata uteuzi wa ndani wa Wizara au Taasisi. Kwa mnasaba huo hakuna kiongozi aliyeruhusiwa kutumia mafuta ya ofisi kwa matumizi binafsi au ya kazi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa viongozo waliotajwa katika toleo la hapo juu ambao waliteuliwa kwa nafasi ya Mhe. Rais kubainika magari yao yanatumia mafuta ya Taasisi yanayolipiwa kwa gharama za matumizi mengineyo (Other Charges) na kuendelea kutumika kwa shughuli mbali mbali zinazofahamika na Taasisi zao kinyume na matakwa ya Muongozo huo.

Aidha, licha ya wateule hao kulipwa stahiki za mafuta ndani ya mishahara yao ukaguzi umebaini jumla ya lita 2,238 zilitumika kinyume na utaratibu kwa viongozi mbali mbali kama ilivyobainishwa katika jadweli hapo chini.

Ukaguzi unawashauri viongozi hao kuepuka kutumia mafuta yanayonunuliwa kwa fedha za uendeshaji kwani kufanya hivyo ni kwenda kinyume na miongozo ya utumishi sambamba na kuibebesha mzigo Serikali na hatimae kupelekea kukosekana kwa tija iliyokusudiwa katika shughuli zote za uendeshaji wa Taasisi za Umma. Mchanganuo wa matumizi ya mafuta hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

## Jadweli Nambari 29:Matumizi ya mafuta kwa Viongozi wateule wa Rais

| Tarehe | Nambari ya Koponi | Idadi ya lita | | Tarehe | Nambari ya Koponi | Idadi ya lita |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mafuta ya Petroli yaliyotumika kwa gari ya Mkuu wa Mkoa SMZ 885 C** | | | | **Mafuta ya Petroli yaliyotumika kwa Gari ya Mkuu wa Wilaya Kusini SMZ 926 A** | | |
| 06.07.2022 | 2715 | 60 | | 27/09/2022 | 661662 | 34 |
| 14.07.2022 | 2724 | 60 | | 30/09/2022 | 661664 | 20 |
| 03.08.2022 | 2780 | 60 | | 03/10/2222 | 661665 | 20 |
| 03.07.2022 | 2780 | 60 | | 17/10/2022 | 661670 | 34 |
| 18.01.2023 | 1676 | 50 | | 17/10/2022 | 661672 | 34 |
| 10.11.2022 | 1615 | 30 | | 19/10/2022 | 661673 | 34 |
| 08.12.2022 | 1620 | 30 | | 22/10/2022 | 661675 | 34 |
| 11.12.2022 | 1622 | 40 | | 02/11/2022 | 661676 | 40 |
| 13.12.2022 | 1625 | 30 | | 22/11/2022 | 661680 | 20 |
| 30.12.2022 | 1646 | 50 | | 23/11/2022 | 661683 | 20 |
| 04.01.2022 | 1669 | 40 | | 25/11/2022 | 661684 | 40 |
| 13.01.2023 | 1668 | 50 | | 29/11/2022 | 661685 | 20 |
| 06.01.2022 | 1663 | 50 | | 01/12/2022 | 661687 | 15 |
| 28.01.2022 | 1686 | 50 | | 13/12/2022 | 661697 | 20 |
| 03.02.2023 | 1683 | 60 | | 31/12/2022 | 662171 | 40 |
| 06.02.2023 | 1686 | 50 | | 16/02/2023 | 682198 | 20 |
| 16.02.2023 | 1698 | 60 | | 24/02/2023 | 694102 | 15 |
| 22.02.2023 | 2503 | 40 | | 01/03/2023 | 694107 | 20 |
| 20.03.2023 | 2511 | 30 | | 03/03/2023 | 694115 | 30 |
| 27.03.2023 | 2522 | 30 | | 07/03/2023 | 694121 | 10 |
| 14.04.2023 | 2530 | 30 | | 17/03/2023 | 694125 | 6 |
| 20.04.2023 | 2531 | 20 | | 19/04/2023 | 694128 | 50 |
| | **Jumla** | **980** | | 19/04/2023 | 694129 | 40 |
| | | | | 21/04/2023 | 694130 | 25 |
| **Mafuta ya Diseli yaliyotumika na Katibu Tawala Wilaya Kusini SMZ 307 A** | | | | 25/04/2023 | 694131 | 20 |
| 27/12/2022 | 662169 | 10 | | 27/04/2023 | 694132 | 30 |
| 11/02/2023 | 692191 | 30 | | 03/05/2023 | 694135 | 30 |
| 14/02/2023 | 692193 | 10 | | 08/05/2023 | 694138 | 10 |
| 16/02/2023 | 682198 | 10 | | 10/05/2023 | 694143 | 20 |
| 23/02/2023 | 682200 | 30 | | 15/05/2023 | 694146 | 20 |
| 27/02/2023 | 694106 | 10 | | 16/05/2023 | 694148 | 10 |

| Tarehe | Nambari ya Koponi | Idadi ya lita | | Tarehe | Nambari ya Koponi | Idadi ya lita |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 01/03/2023 | 694108 | 10 | | 18/05/2023 | 694150 | 30 |
| 03/03/2023 | 694114 | 10 | | 19/05/2023 | 705651 | 22 |
| 06/03/2023 | 694118 | 10 | | 22/05/2023 | 705653 | 15 |
| 08/03/2023 | 694120 | 10 | | 01/06/2023 | 705687 | 50 |
| 14/04/2023 | 694126 | 10 | | 03/06/2023 | 705693 | 30 |
| 08/05/2023 | 694137 | 10 | | 05/06/2023 | 705694 | 20 |
| 10/05/2023 | 694141 | 15 | | 05/05/2023 | 705695 | 10 |
| 18/05/2023 | 694147 | 15 | | 10/06/2023 | 705697 | 20 |
| 03/06/2023 | 705692 | 40 | | 20/06/2023 | 705700 | 20 |
| 12/06/2023 | 705698 | 10 | | **Jumla** | | **998** |
| 13/06/2023 | 705699 | 10 | | | | |
| 30/06/2023 | 664604 | 10 | | | | |
| **Jumla** | | **260** | | | | |

### 5.1.2.4 Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu shilingi 17,731,326

Kifungu nambari 29(1)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa "Afisa Mhasibu wa Taasisi ya Umma atahusika na kusimamia madeni ya Taasisi ya Umma."

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja inadaiwa jumla ya shilingi 17,731,326 yatokanayo na kupatiwa huduma kutoka kwa watoa huduma mbali mbali, ambapo madeni hayo ni ya muda mrefu na hakuna hatua zilizochukuliwa na Ofisi katika kuyalipa madeni hayo.

Hii imesababishwa na kutokuongeza umakini kwa watendaji wenye dhamana ya kusimamia na kufanya malipo ya madeni hayo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja kuongeza umakini katika kufuata Sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kuchukua hatua stahiki za kuyalipa madeni hayo. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 30:Madeni ya muda mrefu ya Ofisi**

| Namba | Wanaodai | Thamani (Tsh.) |
|---|---|---|
| 1. | Watoa huduma | 14,685,100 |
| 2. | Wafanyakazi | 2,799,726 |
| 3. | Taasisi za Serikali | 246,500 |
| **Jumla** | | **17,731,326** |

*Chanzo: Uchambuzi wa Taarifa ya fedha mwaka 2022/2023*

### 5.1.3 FUNGU D 09 - MKOA WA KASKAZINI UNGUJA

Ukaguzi wa hesabu za Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.1.3.1 Deni la fidia ya vipando vya wananchi shilingi 7,146,975

Ukaguzi umebaini kwamba Mkoa wa Kaskazini Unguja umeingia makubaliano na wananchi wa Shehia ya Pale Kiongele Wilaya ya Kaskazini 'A' kulipa fidia ya vipando vyao ili kupisha ujenzi wa kituo cha wajasiriamali.

Tathmini ya vipando hivyo ilifanywa mwezi wa Februari, 2022 na mwezi wa Agosti, 2022 wananchi hao walianza kulipwa. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwepo kwa malipo pungufu kwa wananchi kumi (10) yaliyopelekea uwepo wa bakaa ya deni la shilingi 7,146,975 ambalo hawakulipwa wananchi hao.

Kutolipwa kwa bakaa ya fidia kwa wananchi kwa muda mrefu kunaweza kusababisha kujitokeza kwa kero na manung'uniko kwa wananchi dhidi ya Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kaskazini Unguja kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha bakaa ya deni la fidia ya wananchi inalipwa. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana kwenye jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 31:Deni la fidia ya vipando vya wananchi**

| Namba | Hati Namba | Aliyelipwa | Jumla ya madai (Tsh) | Kiasi alicholipwa (Tsh.) | Kiasi cha Deni (Tsh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 13/8 ya 28/8/2022 | Juma Abdul Haji | 3,300,000 | 2,650,500 | 650,000 |
| 2. | 2/8 ya 22/8/2022 | Abdul Haji Haji | 7,279,000 | 5,482,025 | 1,796,975 |
| 3. | 3/8 ya 22/8/2022 | Tatu Faki Hassan | 2,415,000 | 2,165,000 | 250,000 |
| 4. | 4/8 ya 28/8/2022 | Zuwena Faki Hassan | 2,625,000 | 2,375,000 | 250,000 |
| 5. | 5/8 ya 28/8/2022 | Makame Iddi Chota | 3,241,000 | 2,591,000 | 650,000 |
| 6. | 6/8 ya 28/8/2022 | Mgeni Moh'd Sharif | 4,427,500 | 3,627,500 | 800,000 |
| 7. | 7/8 ya 28/8/2022 | Moh'd Ali Hamdu | 4,501,000 | 3,701,000 | 800,000 |
| 8. | 8/8 ya 28/8/2022 | Moh'd Juma Ussi | 3,780,000 | 3,130,000 | 650,000 |
| 9. | 10/8 ya 28/8/2022 | Khamis Ali Hamdu | 3,489,500 | 2,839,500 | 650,000 |
| 10. | 1/89 ya 14/9/2022 | Faki Khamis Yahya | 3,720,500 | 3,070,500 | 650,000 |
| **Jumla** | | | **38,778,500** | **31,632,025** | **7,146,975** |

### 5.1.3.2 Kutokulipwa kwa fidia ya vipando kwa Wananchi waliopisha ujenzi wa maegesho ya magari shilingi 27,368,500

Kufuatia muendelezo wa ujenzi wa miradi inayotekelezwa na Serikali, Mkoa wa Kaskazini Unguja ni miongoni mwa taasisi zilizobahatika kupata sehemu ya miradi hiyo ambapo Wilaya ya Kaskazini 'A' Shehia ya Pale – Kiongele kumejengwa kituo cha wajasiriamali.

Katika kuimarisha ujenzi wa kituo hicho Serikali ililazimika kuondoa vipando vya wananchi watatu ambao walikua wakijishuhulisha na kilimo katika eneo hilo na hatimae Serikali kuamuru kulitumia eneo hilo kwa ajili ya ujenzi wa maegesho ya gari.

Kwa mujibu wa tathmini iliyofanywa tarehe 17/03/2023 waathirika hao walitakiwa kulipwa fidia ya shilingi 15,548,500 ambapo hadi ukaguzi unakamilika bado hatua ya kufanyika kwa malipo ya fidia hizo hazijachukuliwa.

Aidha, ukaguzi umebaini uwepo wa deni la Ndugu Machano Jamali Machano lenye thamani ya shilingi 11,820,000 kuwa ni deni linalotokana na fidia ya vipando kwa

ajili ya kupisha ujenzi wa eneo la wajasiriamali liliopo Shehia ya Pale Wilaya ya Kaskazini "A". Hadi ukaguzi unakamilika, ndugu Machano Jamali Machano hajalipwa stahiki zake.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kaskazini Unguja kuchukua jitihada za makusudi za kuwatambua waathirika hao ikiwemo kuwaombea stahiki zao ili kuwapunguzia ukali wa maisha. Mchanganuo wa fidia kwa mujibu wa tathmini ni kama inavyoonekana kwenye jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 32:Kutokulipwa kwa fidia ya vipando kwa Wananchi**

| Namba | Aina ya Mazao | Idadi | Class | Gharama kwa kila shina | Jumla ya Gharama |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | **KHAMIS ALI KHAMIS** | | | | |
| | Muhogo mashina | 2,496 | 111 | 3,500 | 8,736,000 |
| | Migomba mashina | 2 | 11 | 10,000 | 20,000 |
| **Jumla ndogo (A)** | | | | | **8,756,000** |
| 2. | **OTHMAN FADHIL KHAMIS** | | | | |
| | Migomba Mashina | 1,228 | 11 | 3,500 | 1,780,000 |
| | Migomba Mashina | 73 | 11 | 2,000 | 1,000,000 |
| | Mihogo Mashina | 61 | 1 | 1,000 | 61,000 |
| **Jumla ndogo (B)** | | | | | **2,841,000** |
| 3. | **HIJA JUMA KHAMIS** | | | | |
| | Muhogo Mashina | 1,179 | 111 | 3,500 | |
| **Jumla ndogo (C)** | | | | | **3,951,500** |
| **MACHANO JAMALI MACHANO** | | | | | |
| 4. | Miembe | 111 | 6 | 1,500,000 | 9,000,000 |
| | Minazi | 111 | 7 | 300,000 | 2,100,000 |
| | Mikeshia | 111 | 12 | 60,000 | 720,000 |
| **Jumla Ndogo (D)** | | | | | **11,820,000** |
| **Jumla Kuu (A+B+C+D)** | | | | | **27,368,500** |

### 5.1.3.3 Kutokuwasilishwa katika Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Taarifa za fedha za Washirika wa Maendeleo shilingi 19,780,000

Muongozo namba 2 wa kufunga hesabu uliotolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa maafisa wahasibu wote (Accounting officers) umetoa maelekezo juu ya ufungaji wa hesabu za mwaka wa fedha 2022/2023.

Kipengele nambari tatu cha 'mazingatio' kwenye muongozo huo kinazitaka Taasisi

zote za kibajeti (Votes na Subvotes) zinazopokea fedha kutoka kwa wahisani wa maendeleo moja kwa moja kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kupitia hesabu za Taasisi zilizopo katika Benki za Kibiashara (Commercial Banks) Taarifa za fedha zote za miradi yote zilizopokelewa katika mwaka wa fedha 2022/2023 ziwasilishwe Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kupitia Idara ya Fedha za Nje na kwa fedha zilizotumika ziwasilishwe Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kupitia Idara ya Mhasibu Mkuu wa wa Serikali kwa ajili ya Kuingizwa katika mfumo wa matumizi (EPICOR) kwa ajili ya kupitishiwa DUMMY, taarifa zote hizi ziwasilishwe kabla ya tarehe ya mwisho wa Ufungaji wa mwaka wa fedha 2022/2023.

Ukaguzi umebaini kua Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kaskazini Unguja imepokea jumla ya shilingi 19,780,000 kutoka UNICEF ambazo ni kwa ajili ya mradi wa ulinzi wa watoto "Children Protection Program".

Dosari iliyobainika ni kutowasilishwa kwa taarifa hizo Ofisi ya Raisi Fedha na Mipango ambapo ni kwenda kinyume na muongozo uliotolewa na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Kutopelekwa kwa taarifa za fedha za wahisani Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kutapelekea Serikali kutojua takwimu sahihi ya fedha ilizopata kupitia wahisani wa maendeleo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kaskazini Unguja kufuata maelekezo ya ufungaji wa hesabu yanayotolewa na Serikali kupitia Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ili kuiwezesha Serikali kupata taarifa za takwimu muhimu upande wa hesabu.

### 5.1.4 FUNGU D10 - MKOA WA KUSINI PEMBA

Ukaguzi wa hesabu za mwaka 2022/2023 kwa Mkoa wa Kusini Pemba umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.1.4.1 Kutokupatiwa Mafunzo ya Awali kwa Waajiriwa Wapya

Kwa mujibu wa kanuni nambari 5(1)(b) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014 inamtaka Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi kuhakikisha kuwa watumishi wanaoingia katika ajira ya utumishi wa umma kwa mara ya kwanza wanapatiwa mafunzo ya awali ya kazi ndani ya muda wa majaribio.

Ukaguzi umebaini kuwa baadhi ya waajiriwa katika Afisi ya Mkuu wa Mkoa Kusini Pemba walioajiriwa kati ya mwaka 2019 hadi sasa hawajapatiwa mafunzo ya

awali (induction course). Hali hii inaweza kupelekea watumishi kukosa uzalendo, kutokujua vyema miiko na maadili ya utumishi wao na hivyo kushindwa kutekeleza kikamilifu majukumu yao ya kazi.

Kutokuwapatia mafunzo ya awali waajiriwa wapya ndani ya muda wa majaribio ni kwenda kinyume na kanuni nambari 5(1)(b) na kanuni nambari 9(2)(c) za Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi ya Mkuu wa Mkoa Kusini Pemba kuhakikisha wanatenga fedha za kutosha katika bajeti zao za mwaka ili kuwezesha waajiriwa wapya kupatiwa mafunzo ya awali. Mchanganuo wa watumishi ambao hawajapatiwa mafunzo ya awali (induction course) ni kama unavyoonekana katika jadweli lifuatalo: -

**Jadweli Nambari 33:Watumishi Ambao Hawajapatiwa Mafunzo ya Awali**

| Namba | Jina | Tarehe ya Ajira | Muda wa Kutokupata Mafunzo (Miezi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Salama Mrisho Ali | 03/10/2020 | 36 |
| 2. | Khadija Juma Mgeni | 03/10/2020 | 36 |
| 3. | Sharifu Hussein Ayoub | 03/09/2019 | 49 |
| 4. | Mshenga Mahmoud Mshenga | 03/09/2019 | 49 |

## 5.1.5 FUNGU D 11 - MKOA WA KASKAZINI PEMBA

Ukaguzi wa hesabu za mwaka 2022/2023 kwa Mkoa wa Kaskazini Pemba umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

### 5.1.5.1 Malipo yaliyokosekana kwa ukaguzi shilingi 5,600,000

Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba imefanya malipo ya vifungu mbali mbali kwa kutumia hati moja ya mtandao ambayo huambatanishwa na hati ndogo ndogo za matumizi ili kuweza kutofautisha malipo ya vifungu husika.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Afisi ya Mkuu wa Mkoa imelipa jumla ya shilingi 17,015,000 kupitia hati ya malipo namba 01/05 ya tarehe 15/05/2023 yenye hundi namba 035223 alizolipwa meneja wa PBZ kwa ajili ya malipo mbali mbali ya Afisi ya Mkuu wa Mkoa Kaskazini Pemba.

Dosari iliyobainika ni kuwa malipo ya shilingi 5,600,000 yalikosekana kwa ajili ya ukaguzi na kupelekea kushindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa matumizi hayo.

Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa baadhi ya hati ndogo ndogo za matumizi jambo ambalo linaweza likapelekea matumizi ya fedha yasiyo na tija kwa Serikali.

Kutokukamilika kwa nyaraka za malipo katika hati ya malipo husika ni kwenda kinyume na kanuni ya 57(1)(2) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kuambatanisha vielelezo vyote husika vya malipo katika hati za malipo kwa wakati.

### 5.1.5.2 Kukosekana kwa nyaraka muhimu za watumishi katika majalada binafsi (Personal File)

Baada ya kupitia baadhi ya majalada binafsi ya watumishi ukaguzi umebaini kutokuwekwa kwa nyaraka muhimu za watumishi katika majalada yao binafsi kama vile kibali cha ajira, barua ya kuthibitishwa kazi, fomu ya uchunguzi wa afya n.k. Hali hii imetokana na maafisa utumishi kutokuwa makini katika kutekeleza majukumu yao jambo ambalo linaweza kusababisha ucheleweshwaji wa upatikanaji wa stahiki mbali mbali za wafanyakazi hasa wakati wa kustaafu kazi.

Kukosekana kwa kibali cha ajira, barua ya kuthibitishwa kazi, fomu ya uchunguzi wa afya pamoja na vielelezo vyengine muhimu vya mtumishi katika jalada binafsi ni kwenda kinyume na kanuni namba 5(1)(a) ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2014.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi ya Mkuu wa Mkoa Kaskazini Pemba kuhakikisha kuwa watumishi wote wanawekewa nyaraka zote muhimu katika majalada yao binafsi. Mchanganuo wa watumishi ambao majalada yao yamekosa baadhi ya nyaraka muhimu ni kama wanavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 34: Nyaraka zilizokosekana katika Majalada binafsi ya Watumishi**

| Namba | Jina la Mtumishi | Kibali cha Ajira | Fomu ya Uchunguzi wa Afya | Mkataba wa Ajira | Barua ya Kuthibitishwa Kazi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mwanaisha | X | ✓ | X | ✓ |
| 2. | Sabri Mohamed Said | ✓ | ✓ | X | X |
| 3. | Fatma Saleh Salim | ✓ | ✓ | X | X |
| 4. | Mudrik Ali Hamad | ✓ | ✓ | ✓ | X |
| 5. | Bakar Mbuki Juma | X | X | X | ✓ |
| 6. | Siti Hamad Othman | X | ✓ | X | X |
| 7. | Sada Khamis Juma | ✓ | ✓ | X | X |
| 8. | Fadhila Khamis Salum | X | ✓ | X | ✓ |

*Chanzo: Majalada binafsi ya watumishi*

***Tanbihi:***

✓ : *Inamaanisha uwepo wa nyaraka iliyoainishwa hapo juu.*

X : *Inamaanisha kutokuwepo kwa nyaraka iliyoainishwa hapo juu.*

TAARIFA ZA UKAGUZI WA HESABU ZA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

# SURA YA SITA



# 6.0 TAARIFA ZA UKAGUZI WA HESABU ZA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

Sura hii inaelezea matokeo ya ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mtaa ambayo inaonyesha masuala muhimu yanayohitaji kushughulikiwa na Serikali, Baraza la Wawakilishi, pamoja na uongozi wa Mamlaka husika ili kuhakikisha ufanisi katika utendaji wa shughuli za taasisi hizo.

## 6.1 Uanzishwaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa

Mamlaka za Serikali za Mitaa imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria nambari 7 ya Uanzishwaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2014. Katika kutekeleza majukumu yake Serikali za Mitaa zinawajibika kufanya kazi zake kwa kufuata sheria mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zikiwemo Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016, Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 pamoja na Sheria nambari 2 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011.

## 6.2 Lengo la Kuanzishwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa

Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeanzishwa kwa madhumuni ya kusogeza huduma karibu na wananchi ili kuleta ufanisi wa utoaji huduma za Serikali, katika kutekeleza majukumu yake Mamlaka za Serikali za Mitaa zinasimamiwa na Mabaraza ya Madiwani ambao ndio wanaoidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya mamlaka hizo. Uendeshwaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa unasimamiwa na Wakurugenzi ambao ndio Maafisa Wahasibu na ndio wenye jukumu la kusimamia ukusanyaji wa mapato na kuidhinisha matumizi ya fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

## 6.3 Ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa

Ukaguzi wa hesabu ulifanyika kwa mujibu wa viwango vya kitaifa na kimataifa vya Ukaguzi na kujiridhisha kwamba taarifa za fedha zitakazotayarishwa zitaonyesha sura sahihi na halisi ili kutoa uhakika kwamba taarifa za mapato na matumizi zimefuata Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo. Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ulifanywa kwa kuangalia utekelezaji wa Sheria ya Uanzishwaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa nambari 7 ya mwaka 2014, Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016, Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016, Sheria Nambari 2 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011 pamoja na Sheria nyenginezo.

Aidha, ukaguzi uliangalia ufanisi wa mfumo wa udhibiti wa ndani, ufanisi katika ukusanyaji wa mapato, usimamizi wa matumizi, usimamizi wa mali za umma, usimamizi wa miradi ya maendeleo pamoja na mifumo ya utendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa kiwango cha wastani katika mfumo wa udhibiti wa ndani wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo kiwango hicho kimepelekea kubainika dosari mbali mbali ambazo zimewasilishwa kwa Maafisa Wahasibu kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi na kufanyiwa marekebisho kwa hoja za ukaguzi zilizobainika. Aidha, baadhi ya hoja za ukaguzi hazikuweza kurekebishwa kutokana na kutokupatikana kwa vielelezo vinavyohusiana na hoja hizo.

Yafuatayo ni matokeo ya ukaguzi kwenye ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2022/2023:-

### 6.3.1 FUNGU 201 - BARAZA LA JIJI LA ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Baraza la Jiji la Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 6.3.1.1 Kutokamilika kwa ujenzi wa kizimba namba 3 katika Jaa la Kibele

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Meneja wa Jaa la kibele Zanzibar aliandika barua yenye kumb. No. CC/SLF-K/VOL.1/63 kwenda kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ ikieleza kuwa baada ya kufanyika kwa tathmini katika eneo la Jaa la Kibele imebainika kuwa sehemu iliyobakia ya kutupia taka katika eneo hilo inaweza kuchukua muda usiozidi mwaka mmoja na nusu kujaa.

Aidha, kwa mujibu wa tathmini, muda wa matumizi ya Jaa hilo umekadiriwa kuwa ni miaka kumi (10) ambapo ukaguzi umebaini uwepo wa vizimba vitatu vya kutupia taka ambapo Kizimba namba 1 kimejaa, Kizimba namba 2 kinakaribia kujaa na Kizimba namba 3 ujenzi wake hadi sasa haujakamilika.

Licha ya jitihada zinazochukuliwa na wasimamizi wa Jaa hilo dosari iliyobainika ni kwamba hakuna jitihada zinazoendelea kuchukuliwa kukamilisha ujenzi wa Kizimba kilichobakia ili kunusuru kuzagaa kwa taka au kutokufanya kazi kabisa kwa jaa hilo pindipo muda wa makadirio wa matumizi ya jaa utakapokamilika na kushindwa kufanya kazi kabisa.

Katika kupima ufanisi wa matumizi ya jaa ukaguzi umeweza kubaini uwepo wa dosari nyengine za kiutendaji ambazo zilipaswa kuchukuliwa hatua za haraka ili kuwezesha matumizi ya jaa hilo kujiendesha kwa ufanisi, miongoni mwa dosari hizo ni kama ifuatavyo:-

- Kukosekana kwa mmiliki halali wa jaa kwa mujibu wa utaratibu ambae atakuwa na uwezo wa kusimamia mazingira yote yanayohusu uwekaji mzuri wa taka, ushughulikiaji wa miundombinu, uendeshaji wa taratibu za upokeaji, ubaguaji na uchakataji wa taka ili kuweza kuzitumia kwa matumizi mengineyo ambayo yataleta faida ikiwemo uzalishaji wa mbolea ambayo itaingiza kipato kwa Taasisi husika.
- Kukosekana kwa mapato yatokanayo na uwepo wa usimamizi wa taka zinazoingia kutoka mahotelini pamoja na makampuni mbali mbali yanayotumia huduma itolewayo na sehemu hiyo ya uhifadhi wa taka.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuhakikisha inachukuwa juhudi za makusudi kuifanyia kazi barua iliyowasilishwa ambayo imeonesha tathmini ya ukomo wa matumizi ya jaa kwa kufanya mambo yafuatayo:-

- Kuchukua hatua za kimkakati kuweza kukamilisha ujenzi wa kizimba namba 3 ili kuweza kunusuru hali ya kuzagaa kwa taka njiani na kusababisha kutuama kwa maji machafu yanayotokana na taka hizo.
- Kufanya ukarabati wa vizimba hivyo ili viweze kutoa huduma kwa muda uliopangwa na kupata tija kama ilivyokusudiwa.
- Kuwepo uwazi wa umiliki wa jaa hilo ili kupatikana kwa uwajibikaji katika usimamizi, uendelezaji na utekelezaji wa shughuli za Jaa Kuu la Kibele ikiwemo kufanya ukarabati na utengenezaji wa vyombo vinavyotumika.
- Kuweko kwa ubinafsishaji wa jaa ili liweze kujiendesha kwa faida.

### 6.3.2 FUNGU 202 - BARAZA LA MANISPAA YA MJINI

Ukaguzi wa hesabu za Baraza la Manispaa ya Mjini kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

### 6.3.2.1 Kutokuwepo Taarifa za Kuhesabu Mali (Stock Taking)

Kifungu cha 71(1) cha Sheria namba 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba Taasisi kufanya zoezi la utambuzi wa vifaa vya taasisi kwa lengo la kujua idadi, thamani na hali halisi ya vifaa hivyo.

Ukaguzi umebaini Baraza la Manispaa ya Mjini kwa mwaka wa fedha 2022/2023 halikufanya zoezi hili licha ya kuwa Baraza lina bakaa ya vifaa mbali mbali ambavyo havikutumika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina pamoja na Kanuni na miongozo inayotolewa na Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kuhakikisha miongozo inafuatwa ili kuendana na mfumo sahihi wa ufungaji wa hesabu ya mwisho wa mwaka ambao umetolewa na Mhasibu Mkuu.

### 6.3.2.2 Kutokuwepo kwa mfumo maalum wa kuhifadhi taarifa za vianzio vya ukusanyaji wa mapato

Kifungu nambari 70 cha Sheria namba 7 ya Serikali za Mitaa ya 2014 kimelipa fursa Baraza kukusanya mapato mbalimbali yatokanayo na kodi, vianzio mbalimbali pamoja na fedha zinazotokana na vitega uchumi, miradi n.k.

Kanuni nambari 27(3) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2021 inaeleza kwamba Mamlaka ya Serikali za Mitaa itakuwa na uwezo wa kuweka malengo ya mapato.

Ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Manispaa ya Mjini hawana mfumo maalum wa kuhifadhia kumbukumbu zinazotokana na vianzio mbalimbali vya mapato kama vile fomu za leseni za biashara, mabango, ada ya usajili wa wafanya biashara ndogo ndogo, n.k jambo ambalo linapelekea Baraza kushindwa kuweka na kufikia malengo halisi ya ukusanyaji wa mapato kutokana na kutojulikanwa kwa idadi halisi ya vianzio hivyo.

Aidha, ukaguzi umeshindwa kujiridhisha na uhalisia wa makusanyo ya mapato yanayotokana na vianzio hivyo kutokana na Baraza hilo kutojuwa idadi halisi ya vianzio vyake.

Kukosekana kwa mifumo ya kuhifadhia kumbumbuku zilizoainishwa hapo juu kunapelekea:

- Kutojuwa uhalisia na mtiririko mzima wa fedha zilizokusanywa.

- Kutojulikana kwa takwimu halisi za vianzio vya mapato kama vile idadi ya mabango ya matangazo yanayotakiwa kulipiwa mapato, leseni, maduka yanayokusanywa taka, mahoteli yanayokusanywa taka, maskuli na taasisi zikiwemo makanisa na miskiti, idadi ya fomu za leseni zilizopokelewa na Baraza n.k.
- Kuwepo kwa ugumu wa ufuatiliaji wa mapato hayo hali ambayo imepelekea kuchukua muda mrefu kwa ajili ya kufuatilia kumbukumbu kwenye mafaili hususan kumbukumbu za miaka ya nyuma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza kuhakikisha kwamba unachukua hatua za makusudi za kuanzisha mfumo wa kuhifadhia taarifa mbalimbali ili uweze kuwasaidia watendaji katika kutekeleza majukumu yao kwa urahisi.

### 6.3.2.3 Kutokuwepo kwa mchanganuo wa vyanzo vya mapato katika mfumo wa makusanyo wa MUTM

Kwa mujibu wa kifungu nambari 27(2)(a) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 pamoja na kanuni nambari 25(1-2) na kanuni nambari 122(1)(a-d) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021, zinahimiza usahihi na uwazi wa taarifa za mapato/fedha za Taasisi.

Ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Manispaa ya Mjini lina vianzio vya makusanyo ya mapato visivyopungua 19 vya ukusanyaji wa mapato ambayo yanasaidia katika utekelezaji wa majukumu ya Baraza kama vile mapato yatokanayo na huduma za ada ya usafi, leseni, fomu, masoko n.k.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kwamba mapato yote yanaingizwa katika mfumo wa MUTM kupitia hesabu ya mapato yenye nambari 0404007000 bila ya kuwepo mchanganuo au kutofautisha aina na kiwango cha kila chanzo cha mapato kilichokusanywa kwa kipindi husika jambo ambalo limepelekea ukaguzi kushindwa kutathmini na kujua hali halisi ya ukusanyaji wa mapato kwa kila chanzo kulingana na makadirio yaliyowekwa.

Aidha, ukaguzi umeshindwa kujiridhisha na kuthibitisha taarifa za mapato zilizoainishwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka kutokana na kukosekana kwa uwazi wa taarifa za kila kianzio husika.

Kukosekana kwa mchanganuo wa vyanzo mbalimbali vya mapato katika mfumo wa makusanyo unaotumiwa na Baraza kunaweza kupelekea kujitokeza kwa mambo yafuatayo:-

- Kukosekana kwa uwazi na takwimu sahihi za mapato kulingana na vyanzo husika.

- Kushindwa kufanya tathmini juu ya mwenendo mzima wa ukusanyaji wa mapato.
- Kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa mapato ya Serikali kutokana na kutokujulikana kima halisi cha fedha kinachokusanywa kwa kila chanzo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kuweka alama za utambulisho "code" ambazo zitaainisha na kutofautisha aina na kiwango halisi cha mapato yaliyokusanywa kwa kila chanzo kwa mwaka husika.

#### 6.3.2.4 Tofauti ya bakaa ya fedha ya kufunga na kufungulia mwaka shilingi 178,446,089

Ukaguzi umekagua kumbukumbu mbalimbali za kurikodia taarifa za fedha zikiwemo daftari la kurikodia fedha taslim, taarifa za benki pamoja na hesabu ya mwisho wa mwaka na kubaini kwamba bakaa ya fedha zilizowasilishwa kwenye hesabu ya kufungia mwaka imetofautiana na bakaa ya kufungulia mwaka ambapo hesabu ya mwisho wa mwaka 2022/2023 inaonyesha bakaa ya kufungia mwaka 2021/2022 ilikuwa ni shilingi 383,292,684.38 na bakaa ya kufungulia mwaka 2022/2023 ni shilingi 561,738,773.29 hivyo kupelekea tofauti ya shilingi 178,446,089 baina ya bakaa ya kufungia na kufungulia mwaka.

Aidha, ukaguzi umebaini kuwa bakaa ya kufungulia mwaka iliyoainishwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka shilingi 561,738,773.29 inakwenda sambamba na bakaa ya fedha iliopo benki katika hesabu ya mapato jambo ambalo linaashiria kukosekana kwa usahihi wa bakaa ya fedha ya mwisho wa mwaka iliyoainishwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kutokana na kutokuzingatiwa misingi ya uandaaji wa usuluhisho wa kibenki.

Kutokuwepo kwa usawa wa bakaa ya fedha baina ya hesabu ya mwisho wa mwaka pamoja na taarifa za benki kunaweza kupelekea kukosekana kwa ithibati ya taarifa za hesabu ya mwisho wa mwaka iliyowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kuhakikisha unarekebisha mapungufu yaliyobainika kwenye hesabu za mwaka 2021/2022 kupitia taarifa za mfumo ili kuweka bakaa sahihi kwa taarifa za hesabu za mwaka 2022/2023.

#### 6.3.2.5 Kutokufanyika kwa usuluhishi wa kibenki

Kanuni nambari 105(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2021 inamtaka Afisa Masuuli kufanya usuluhishi wa kibenki kila mwezi au mara kwa mara kutegemea na miongozo ya Hazina au matoleo mengine yaliyotolewa na Mhasibu Mkuu wa Serikali.

Ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Manispaa ya Mjini halifanyi usuluhishi wa kibenki kama kanuni zinavyoelekeza jambo ambalo limepelekea Baraza kushidwa kugundua sababu zilizopelekea kutowiana kwa taarifa zilizorikodiwa katika mabuku ya kurikodia fedha taslim na taarifa za fedha zilizopo katika taarifa za benki (Bank statements).

Kutofanyika kwa usuluhishi wa kibenki kwa mujibu wa Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma kumepelekea kutopatikana kwa usahihi wa taarifa za fedha zilizoainishwa katika vitabu vya kumbukumbu, taarifa zililoingizwa kwenye mfumo pamoja na taarifa zilizopo benki.

Aidha,Taasisi kushindwa kugundua makosa katika hatua za awali na kupelekea kuendelea kufanya makosa hayo kwa muda mrefu jambo ambalo linapelekea ugumu katika utatuzi wake.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kufanya usuluhishi wa kibenki kila wiki ili kuweza kugundua mapema, kupunguza au kuzuia matatizo yanayopelekea kutopatikana kwa usahihi wa taarifa za mapato pamoja na matumizi zinazorikodiwa katika vitabu vya hesabu za Taasisi.

### 6.3.3 FUNGU 204 - BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI "B"

Ukaguzi wa hesabu za Baraza la Manispaa Magharibi "B" kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 6.3.3.1 Tofauti ya Bakaa ya fedha kwenye hesabu ya mwisho wa mwaka na bakaa iliopo benki shilingi 106,839,247.01

Ukaguzi umepitia taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka 2022/2023 na kubaini uwepo wa bakaa ya fedha ya shilingi 396,947,799 iliyoainishwa katika hesabu hiyo ikilinganishwa na bakaa ya fedha ya shilingi 290,108,551.99 iliyoainishwa katika taarifa za benki ambapo imepelekea uwepo wa tofauti ya shilingi 106,839,247.01 baina ya hesabu za mwisho wa mwaka na taarifa za benki.

Kutokuwepo kwa usawa baina ya hesabu ya mwisho wa mwaka pamoja na taarifa za hesabu za benki kunapelekea kukosekana kwa ithibati ya taarifa za hesabu ya mwisho wa mwaka na hatimae kutokuonyesha sura sahihi na halisi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" kuhakikisha unaandaa taarifa za hesabu kwa mujibu wa misingi iliyowekwa ya utayarishaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kulingana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na

kimataifa. Aidha, uongozi unashauriwa kuipeleka hesabu ya mwisho wa mwaka katika kitengo cha ukaguzi wa ndani ili Kamati ya Ukaguzi iweze kufanyia mapitio na marekebisho kabla ya kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

### 6.3.3.2 Kutokufanyika kwa usuluhishi wa kibenki

Kanuni nambari 105(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2021 inamtaka Afisa Masuuli kufanya usuluhishi wa kibenki kila mwezi au mara kwa mara kutegemea na miongozo ya Hazina au matoleo mengine yaliyotolewa na Mhasibu Mkuu wa Serikali.

Ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" halifanyi usuluhishi wa kibenki kama kanuni zinavyoelekeza jambo ambalo limepelekea Baraza kushindwa kugundua sababu zilizopelekea kutowiana kwa taarifa zilizorikodiwa katika mabuku ya kurikodia fedha taslim na taarifa za fedha zilizopo katika taarifa za benki (Bank statements).

Kutofanyika kwa usuluhishi wa kibenki kwa mujibu wa Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma kumepelekea kutopatikana kwa usahihi wa taarifa za fedha zilizoainishwa katika vitabu vya kumbukumbu, taarifa zililoingizwa kwenye mfumo pamoja na taarifa zilizopo benki.

Aidha,Taasisi kushindwa kugundua makosa katika hatua za awali na kupelekea kuendelea kufanya makosa hayo kwa muda mrefu jambo ambalo linapelekea ugumu katika utatuzi wake.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" kufanya usuluhishi wa kibenki kila wiki ili kuweza kugundua mapema, kupunguza au kuzuia matatizo yanayopelekea kutopatikana kwa usahihi wa taarifa za mapato pamoja na matumizi ya fedha zilizorikodiwa katika vitabu vya hesabu za Taasisi.

### 6.3.3.3 Kukosekana kwa mapato ya Minara yanayokusanywa na ZICTIA

Kifungu nambari 27(1)(a) cha Sheria nambari 7 ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya 2014 kinaeleza kwamba "Baraza la Manispaa, Baraza la Jiji, Baraza la Mji, Halmashauri zinauwezo wa kuingia mikataba na upande wowote ikihitajika".

Ukaguzi umebaini uwepo wa wakala wa ukusanyaji wa mapato yatokanayo na tozo za minara na matangazo ZICTIA ambaye amefunga mkataba na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa dhamana ya ukusanyaji wa mapato hayo pasi na Baraza kutambua makubaliano hayo.

Kufanya hivyo kumepelekea ukaguzi kushindwa kubaini na kuthibitisha kiwango halisi cha fedha kinachokusanywa na kiwango kinachopaswa kupewa Baraza.

Pamoja na kuwasilisha Wizarani mradi ambao utatumika kama ni kigezo cha kupewa fedha hizo, Baraza la Manispaa Magharibi “B” limeshindwa kuthibitisha taratibu zilizotumika katika uombaji wa fedha hizo.

Aidha, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kipindi cha miaka mitatu sasa bado haijawasilisha gawio la fedha zinazotokana na mapato ya minara katika Baraza jambo ambalo limepelekea kupungua kwa mapato ya Baraza na kupelekea kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuwa mapato yote yaliokusanywa kwa niaba ya Baraza la Manispaa Magharib “B” yanayotokana na minara yanawasilishwa kwenye Baraza kwa wakati kwa ajili ya kusaidia kukuza mapato ya Baraza na kuweka taarifa sahihi ya mapato yaliyokusanywa na kubainishwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka.

#### 6.3.3.4 Kutofanyika kwa wakati matengenezo ya vyombo vya Moto

Kifungu namba 58(b) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba “Afisa Masuuli wa Taasisi ya umma atakuwa na jukumu la kuhakikisha mifumo ya udhibiti wa ndani kwa ajili ya utaratibu wa uhifadhi na matengenezo ya mali za umma inawekwa”.

Ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Manispaa Magharibi “B” halina mfumo wa udhibiti wa ndani ambao unasimamia utaratibu wa kuhifadhi na kutengeneza mali zao ambazo zipo katika hali ya uchakavu. Hii imepelekea kuwepo kwa magari ambayo yanahitaji matengenezo lakini mpaka ukaguzi unakamilika Baraza hilo lilikuwa bado halijafanya matengenezo hayo.

Kutofanyika kwa matengenezo ya Mali kwa wakati kunaweza kupelekea:

- Kuharibika zaidi kwa mali hizo.
- Kutumika kwa fedha nyingi wakati wa kufanyika kwa matengenezo ya mali hizo.
- Upotevu wa fedha za Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Magharibi “B” kuhakikisha kwamba unachukua hatua za makusudi za kufanya matengenezo ya mapema mali zilizo chini ya Baraza ili kupunguza utumiaji wa fedha nyingi za Serikali zinazotokana na kuchelewa kufanyika kwa matengenezo.

### 6.3.4 FUNGU 205 - BARAZA LA MJI WILAYA YA KASKAZINI "A"

Ukaguzi wa hesabu za Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini ''A" kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 6.3.4.1 Kutokuwasilishwa kwa Rasimu ya Mkataba wa Ukusanyaji Taka kwa Mwanasheria Mkuu

Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "A" limesaini hati ya makubaliano yenye kumbukumbu namba SMZ/D0905/NCS/OQ/2023/2024 na mtoa huduma Zanrec Plastic Company Limited kwa ajili ya ukusanyaji wa ada ya taka kwa kipindi cha miaka minne (4) kuanzia tarehe 27/11/2023 hadi tarehe 26/11/2027 kwa thamani ya asilimia kumi na tano (15%) kwa kila mwezi kutokana na fedha itakayokusanywa kwenye ada ya uzoaji wa taka.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokuwasilishwa kwa rasimu ya mkataba huo Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kupitiwa na kupata ushauri wa kisheria kabla ya kuanza kutumika jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 27(3) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza kuhakikisha mikataba yote inayoingia inawasilishwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa mujibiu wa sheria ili kuepusha kujitokeza kwa mikataba isiyo na tija na Serikali na hatimae kupelekea kuingiza hasara Serikali.

#### 6.3.4.2 Kutokufanyiwa kazi kwa ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "A" liliandaa rasimu za mikataba ya ujenzi wa Soko la Chaani na Soko la Mkwajuni Wilaya ya Kaskazini "A" na kuziwasilisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata ushauri wa kisheria kabla ya kusainiwa kwa rasimu hizo.

Pamoja na mambo mengineyo Afisi ya Mwanasheria Mkuu ilitoa ushauri ufuatao kutokana na rasimu zilizowasilishwa:-

- Kwa kuzingatia tangazo la Sheria nambari 50 la mwaka 2017 ya Wakala wa Majengo Zanzibar (Zanzibar Building Agency Legal Notice no. 50 of 2017) ambayo imetoa mamlaka kwa Wakala wa Majengo Zanzibar kusimamia,

kuratibu, kujenga na kufanyia matenegezo majengo ya Serikali, Afisi inashauri kwamba, ni vyema kwa Taasisi yako kuwasilisha Rasimu husika ZBA kwa hatua za kupata ushauri wa kitaalamu.

- Kwamba, Hati ya Kupinga Hongo na Ufisadi inayokataza malipo au zawadi kwa maafisa wa Serikali au mtu mwengine aliye na cheo kikubwa ili kupata manufaa yoyote yasiofaa ya biashara (Anti-Bribery Memorandum Policy) ambayo ni sehemu ya mkataba huu haijaambatanishwa, hivyo Afisi inashauri hati hiyo iambatanishwe na iwe ni sehemu ya Rasimu ya mkataba.
- Kwamba, katika kusimamia na kutekeleza kazi husika Afisi yako inashauriwa kushirikiana na wataalam kutoka Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) ili kuleta tija na ufanisi wa kazi tajwa hapo juu.
- Kwamba, Afisi imebaini hakuna taarifa za kibenki za mkandarasi (Bank Guarantee) hivyo ni vyema Rasimu ikasomeka taarifa kamili za kibenki za mkandarasi. Pamoja na mambo mengine taarifa hizo zijumuishe jina la Benki, Nambari za Hesabu (account number) na jina la Tawi la Benki.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokufanyiwa kazi ushauri uliotolewa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu jambo ambalo limepelekea uwepo wa ukiukwaji wa kisheria kwa mujibu wa kifungu nambari 27(3) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "A" kuhakikisha unatekeleza ushauri wa kitaalamu unaotolewa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu ili kuepuka kujitokeza kwa uingiaji wa mikataba kiholela ambayo haitakuwa na tija na Serikali na hatimae kuibebesha Serikali mzigo wa gharama pindipo Mzabuni atakaposhindwa kutekeleza matakwa ya makubaliano ya mkataba huo.

### 6.3.5 FUNGU 206 - BARAZA LA MJI WILAYA YA KASKAZINI "B"

Ukaguzi wa hesabu za Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "B" kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

### 6.3.5.1 Kutokuwasilishwa kwa Rasimu ya Mkataba wa Ukusanyaji Taka kwa Mwanasheria Mkuu

Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "B" limesaini hati ya makubaliano yenye kumbukumbu namba BMK'B'/MKTB/DEV/NCQ/2022-2023/01 na mtoa huduma Ali Vuai Khamis kwa ajili ya ukusanyaji wa ada ya taka kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia tarehe 30/06/2022 hadi tarehe 01/07/2023 kwa thamani ya malipo ya asilimia Ishirini (20%) kwa kila mwezi kutokana na fedha itakayokusanywa kwenye ada ya uzoaji wa taka.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokuwasilishwa kwa rasimu ya mkataba huo Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kupitiwa na kupata ushauri wa kisheria kabla ya kuanza kutumika jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 27(3) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza kuhakikisha mikataba yote inayoingia inawasilishwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa mujibu wa sheria ili kuepusha kujitokeza kwa mikataba isiyo na tija na Serikali na hatimae kupelekea kuingiza hasara Serikali.

## 6.3.6 FUNGU 207 - BARAZA LA MJI WILAYA YA KATI

Ukaguzi wa hesabu za Baraza la Mji Wilaya ya Kati kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

### 6.3.6.1 Kutokufanyika kwa usuluhishi wa kibenki

Kanuni nambari 105(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2021 inamtaka Afisa Masuuli kufanya usuluhishi wa kibenki kila mwezi au mara kwa mara kutegemea na miongozo ya Hazina au matoleo mengine yaliyotolewa na Mhasibu Mkuu wa Serikali.

Ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Mji Wilaya ya Kati halifanyi usuluhishi wa kibenki kama kanuni zinavyoelekeza jambo ambalo limepelekea Baraza kushidwa kugundua sababu zilizopelekea kutowiana kwa taarifa zilizorikodiwa katika mabuku ya kurikodia fedha taslim na taarifa za fedha zilizopo katika taarifa za benki (Bank statements).

Kutofanyika kwa usuluhishi wa kibenki kwa mujibu wa Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma kumepelekea kutopatikana kwa usahihi wa taarifa za fedha zilizoainishwa katika vitabu vya kumbukumbu, taarifa zililoingizwa kwenye mfumo pamoja na taarifa zilizopo benki.

Aidha,Taasisi kushindwa kugundua makosa katika hatua za awali na kupelekea kuendelea kufanya makosa hayo kwa muda mrefu jambo ambalo linapelekea ugumu katika utatuzi wake.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji Wilaya ya Kati kufanya usuluhishi wa kibenki kila wiki ili kuweza kugundua mapema, kupunguza au kuzuia matatizo yanayopelekea kutopatikana kwa usahihi wa taarifa za mapato pamoja na matumizi zinazorikodiwa katika vitabu vya hesabu za Taasisi.

### 6.3.6.2 Kutokukusanywa kwa Mapato ya ada ya taka za Hoteli shilingi 85,200,000

Kifungu nambari 69(1) cha Sheria nambari 7 ya Uanzishwaji wa Serikali za Mitaa ya 2014 kimelipa fursa Baraza kukusanya mapato mbalimbali yatokanayo na kodi, vianzio mbalimbali pamoja na fedha zinazotokana na vitega uchumi, miradi n.k.

Ukaguzi umepitia nyaraka na taarifa mbalimbali zinazohusiana na mapato yatokanayo na ada ya ukusanywaji wa taka za Mahoteli na kubaini kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Baraza la Mji Wilaya ya Kati limeshindwa kukusanya mapato ya shilingi 85,200,000 yanayohusiana na ada za taka katika mahoteli.

Kutokukusanywa kwa mapato yatokanayo na ada ya taka za Mahoteli ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria kilichonakiliwa hapo juu jambo ambalo linapelekea kutokufikiwa kwa malengo yaliyopangwa na kuikosesha Serikali mapato.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji Wilaya ya Kati kuhakikisha unapanga mbinu na mikakati imara ya kuweza kuyafikia mahoteli, kuhamasisha ulipaji wa hiari pamoja na kusimamia misingi ya sheria na kanuni zilizopo ili kuleta ufanisi wa kiutendaji. Orodha ya hoteli ambazo hazikulipa ada ya taka ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 35:Mapato ya ada ya taka za Mahoteli ambayo hayakuweza kukusanywa**

| Namba | Jina la Hoteli | Kiwango cha Ada ya Makusanyo kwa mwezi (Tsh.) | Kiwango cha Ada ya Makusanyo kwa mwaka (Tsh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | Pongwe Beach Hotel | 500,000 | 6,000,000 |
| 2. | Tulia Zanzibar Unique Resort | 500,000 | 6,000,000 |
| 3. | Roa Hotel | 1,250,000 | 15,000,000 |
| 4. | White Paradise Zanzibar | 500,000 | 6,000,000 |
| 5. | Santa Maria | 300,000 | 3,600,000 |
| 6. | Pongwe Bay Resort | 500,000 | 6,000,000 |
| 7. | Uroa Bay | 1,250,000 | 15,000,000 |
| 8. | Azao Resort and Spa Co.Ltd | 500,000 | 6,000,000 |
| 9. | Palumbo Reef Resort | 500,000 | 6,000,000 |
| 10. | Nautilis Lodge | 300,000 | 3,600,000 |
| 11. | F-Zeen Hotel | 500,000 | 6,000,000 |
| 12. | The Island | 500,000 | 6,000,000 |
| **Jumla** | | **7,100,000** | **85,200,000** |

### 6.3.6.3 Dosari katika makabidhiano ya utekelezaji wa Majukumu

Kwa mujibu wa utaratibu wa utumishi wa umma, Mtumishi wa umma atalazimika kuandika barua ya makabidhiano wakati anapoondoka katika wadhifa wake kwa sababu yeyote ile. Aidha, kanuni nambari 116(3) ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya 2014 inaeleza kwamba "Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi atalazimika kuandaa fomu ya makabidhiano inayoonyesha orodha ya vifaa au nyaraka alizozitumia wakati wa kutekeleza majukumu yake".

Katika utekelezaji wa kazi za ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi umebaini uwepo wa dosari za kiutendaji zinazotokana na kutokuwepo kwa makabidhiano ya kazi kwa baadhi ya watumishi waliopata uhamisho, waliokwenda masomoni au waliomaliza muda wa utumishi katika Baraza la Mji Wilaya ya Kati jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa usumbufu kwa watendaji waliokabidhiwa dhamana hizo kuzitekeleza kinyume na utaratibu wa kisheria.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji Wilaya ya Kati kuhakikisha dhamana zinazotolewa zinafuata msingi wa kisheria ili kuweka uwazi na uwajibikaji wa majukumu ikiwemo kutoa fursa ya uchukuwaji wa hatua kwa mtumishi atakeshindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

#### 6.3.6.4 Kukosekana kwa mkataba wa ununuzi wa mafuta shilingi 64,215,000

Kwa mujibu wa kifungu nambari 42(2) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kwamba "Taasisi ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma itapanga mpango wake wa ununuzi na uondoshaji kwa kutumia vigezo vinavyokubalika na hususan utazingatia kutumia mfumo wa mikataba maalumu kwa namna inavyohitajika kutoa huduma bora, zenye gharama nafuu na kwa njia inayoweza kubadilika kwa bidhaa zinazohitajika kila mara au zinazojirudia kila baada ya muda".

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi umefanya tathmini ya matumizi ya mafuta yanayotumiwa na Baraza la Mji Wilaya ya Kati na kubaini jumla ya shilingi 64,215,000 zimetumika kununua mafuta kwa shughuli mbali mbali za uendeshaji. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokuwepo kwa Mkataba wa mauziano baina ya Baraza la Mji Wilaya ya Kati na Kampuni ya Zanzibar Petroleum Limited.

Kutokuwepo kwa mafungamano ya maandishi kunaweza kupelekea kujitokeza kwa changamoto pale ambapo taasisi moja itakaposhindwa kutekeleza makubaliano ya awali waliyokubaliana jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji Wilaya ya Kati kuhakikisha wanafunga mikataba kwa ununuzi wa bidhaa zote wanazotumia kila mara au zinazojirudia kila baada ya muda kama Sheria inavyoolekeza.

### 6.3.7 FUNGU 208 - HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI UNGUJA

Ukaguzi wa hesabu za Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 6.3.7.1 Tofauti ya Bakaa ya fedha kwenye hesabu ya mwisho wa mwaka na bakaa iliopo benki shilingi 44,622,028.94

Ukaguzi umepitia taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka 2022/2023 za Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja na kubaini uwepo wa bakaa ya fedha ya shilingi 721,660,979.13 iliyoainishwa katika hesabu hiyo ikilinganishwa na bakaa ya fedha ya shilingi 766,283,008.07 iliyoainishwa katika taarifa za benki ambapo imepelekea uwepo wa tofauti ya shilingi 44,622,028.94 baina ya hesabu za mwisho wa mwaka na taarifa za benki.

Kutokuwepo kwa usawa baina ya hesabu ya mwisho wa mwaka pamoja na taarifa za hesabu za benki kunapelekea kukosekana kwa ithibati ya taarifa za hesabu ya mwisho wa mwaka na hatimae kutokuonyesha sura sahihi na halisi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja kuhakikisha unaandaa taarifa za hesabu kwa mujibu wa misingi iliyowekwa ya utayarishaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kulingana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa. Aidha, uongozi unashauriwa kuipeleka hesabu ya mwisho wa mwaka katika kitengo cha ukaguzi wa ndani ili Kamati ya Ukaguzi iweze kufanyia mapitio na marekebisho kabla ya kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

#### 6.3.7.2 Kukosekana kwa mapato ya leseni za skuli binafsi shilingi 1,500,000

Kwa mujibu wa kifungu nambari 70(b)(ii) cha Sheria nambari 7 ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya 2014 pamoja na kanuni nambari 31(2) na 32 za Kanuni ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa za 2020 vinaelezea juu ya namna ya kufanya biashara na ukataji wa leseni za biashara.

Ukaguzi umefanya mapitio na tathmini ya mapato yatokanayo na ukataji wa leseni zitokanazo na uwepo wa skuli binafsi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja na kubaini mara baada ya wamiliki wa skuli binafsi kupata kibali cha usajili wa skuli kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wanatakiwa kulipia mapato ya leseni kwa viwango vifuatavyo:-

- Skuli za Maandalizi (Nursery) 100,000
- Skuli ya Msingi na Mandalizi 250,000
- Skuli ya Maandalizi, Msingi na Secondary 500,000

Dosari iliyobanika katika ukaguzi ni uwepo wa skuli nne (4) ambazo zimeshindwa kutekeleza agizo la kukata leseni kwa mujibu wa muongozo uliotolewa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kupelekea kuikosesha Serikali jumla ya shilingi 1,500,000 ikiwa ni ada ya mapato ya ukataji wa leseni.

Aidha, kutokukatwa kwa leseni ya biashara kunapelekea kuikosesha mapato Halmashauri na hatimae kushindwa kutekeleza majukumu waliyojipangia.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja kuongeza mikakati imara ya kusimamia vyanzo vya mapato ikiwemo kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kuweza kujiendesha kiufanisi pindipo baadhi ya vyanzo vya mapato vitakaposhindwa kukidhi makusanyo halisi kwa mujibu wa makadirio ya bajeti.

Orodha ya Skuli hizo na kima kinachodaiwa ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 36:Skuli ambazo hazijakata leseni ya biashara**

| Namba | Jina la Skuli | Malipo ya Leseni |
|---|---|---|
| 1. | Bwejuu Charity School | 500,000 |
| 2. | Assalaam International School | 250,000 |
| 3. | South East Cost | 250,000 |
| 4. | Dallalul Khairat | 500,000 |
| **Jumla** | | **1,500,000** |

### 6.3.7.3 Kutokuwekewa alama za Utambulisho kwa samani za Ofisi

Kifungu nambari 58(d) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba "Afisa Masuuli wa taasisi ya umma atahakikisha utaratibu wa kuhifadhi unawekwa ili kuondosha wizi, hasara, kupotea na matumizi mabaya".

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika uwepo wa samani nyingi zinazotumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja kwa ajili ya matumizi ya kuendeshea shughuli zake za kawaida, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokuekewa kwa alama maalumu inayotambulisha aina ya mali, sehemu iliyopo na mmiliki husika wa mali hiyo jambo ambalo huwenda ikapelekea kujitokeza kwa upotevu, kuchukuliwa au kuazimwa bila ya taarifa pamoja na matumizi mabaya ya mali hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini kuchukua juhudi za haraka kuziwekea alama samani zake zote zilizokosa alama ili kuepusha kujitokeza kwa upotevu wa mali hizo.

### 6.3.7.4 Kutokufanyika kwa tathmini ya utendaji kazi (Performance Appraisal)

Kanuni nambari 93(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya 2014 inaelekeza "Kila taasisi ya umma italazimika kumfanyia tathmini ya utendaji wa kazi mtumishi wake kila mwaka. Fomu ya tathmini itatolewa na Afisi Kuu ya Utumishi wa Umma".

Ukaguzi umebaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja haifanyi tathmini ya utendaji kazi kwa watumishi wake kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya Utumishi.

Kutokufanyika kwa tathmini ya utendaji kazi kwa watumishi kunapelekea kuwakosesha haki zao za msingi kwa mujibu wa sheria ikiwemo kupata nyongeza ya mwaka, kupandishwa madaraja pamoja na stahiki nyenginezo zinazohusiana na mtumishi wa Umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja kuhakikisha unatekeleza wajibu wa kumfanyia mtumishi tathmini ili kuweza kupima ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa miongozo na taratibu za kiutumishi.

### 6.3.7.5 Kutokuwepo kwa Mpango Maalum wa Mafunzo

Kanuni nambari 74(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014 inazitaka "Taasisi zote za Serikali kuandaa mpango maalum wa mafunzo pamoja na kutenga fedha kwa ajili ya mafunzo hayo". Aidha kwa mujibu wa waraka wenye kumbukumbu namba CAB.40/158/01/54 na CAB.40/158/01/37 kutoka Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora unazitaka Wizara na Taasisi za umma kufanya maandalizi ya mpango wa mafunzo ili kujua mahitaji (Training Needs Assessment) na kuwasilisha mpango wa mafunzo.

Ukaguzi umebaini kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imetumia jumla ya shilingi 21,248,400 kwa ajili ya mafunzo ya muda mrefu na mfupi bila ya kuwepo kwa mpango mkuu wa mafunzo hivyo ukaguzi kushindwa kuthibitisha uhalali wa vigezo vilivyotumika kuwapata watumishi waliopewa nafasi za mafunzo ya muda mrefu au muda mfupi, vile vile kushindwa kujiridhisha juu ya uhitaji wa Halmashauri kwa nafasi za mafunzo yaliyotolewa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja kuhakikisha unaandaa mpango wa mafunzo, mpango wa tathmini ya mahitaji pamoja na bajeti ya mafunzo ili kuepusha kujitokeza kwa mizozo au malalamiko kwa watumishi wa umma watakaonyimwa nafasi ya kushiriki katika mafunzo. Mchanganuo wa watumishi waliopatiwa mafunzo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 37:Watumishi waliopatiwa mafunzo bila ya kuwepo kwa Mpango wa Mafunzo**

| Namba | Jina | Muda wa mafunzo | Mafunzo aliyopata | Muda wa kumaliza mafunzo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Moh'd Kh. Abdalla | Miaka Minne | Computer Engineering and Information Technology | 2025 |
| 2. | Faida M. Makame | Miaka Mitatu | Business Human Resources | 2023 |
| 3. | Khatib M. Khatib | Miaka Miwili | Master on Economic and Finance | 2025 |
| 4. | Hilda Kh. Juma | Miaka Mitatu | Degree on Economic and Development | 2025 |
| 5. | Abdulwarith K. Fatawi | Wiki 2 | Monitoring and Evaluation | 2023 |
| 6. | Hassan P. Ali | Wiki 2 | Waste Managemaet | 2023 |
| 7. | Shemsa Kh. Yussuf | Wiki 1 | | 2023 |
| 8. | Hamid S. Ali | Wiki 1 | | 2023 |
| 9. | Sibadili Z. Arafat | Wiki 1 | Record and Archive Management | 2023 |
| 10. | Subira Kh. Fadhil | Wiki 1 | | 2023 |
| 11. | Mtumwa S. Ali | Wiki 1 | | 2023 |
| 12. | Saleh A. Seif | Wiki 2 | Monitoring and Evaluation | 2023 |

### 6.3.8 KASMA 209 - BARAZA LA MJI WETE

Ukaguzi wa hesabu za Baraza la Mji Wete kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 6.3.8.1 Kukosekana kwa Nyaraka za uchambuzi wa madeni shilingi 33,486,026.74

Ukaguzi ulipitia hesabu ya mwisho wa mwaka iliyowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Baraza la Mji Wete na kubaini kwamba kuna madeni ya wafanyakazi na wasambazaji wa bidhaa mbalimbali kwa ajili ya Baraza yenye thamani ya shilingi 75,615,790.74. Hadi ukaguzi huu unakamilika mnamo Februari, 2024 madeni yaliyokuwa na nyaraka za uthibitisho ni shilingi 42,129,764 na hivyo kutokupatiwa nyaraka za uthibitisho wa deni la shilingi 33,486,026.74 kwa ajili ya ukaguzi jambo ambalo limepelekea ukaguzi kushindwa kuthibitisha uhalali wa madeni hayo.

Kukosekana kwa kumbukumbu za kuthibitisha uhalali wa kuwepo kwa madeni hayo kunaweza kupelekea taarifa za hesabu zilizowasilishwa kutoonyesha sura halisi na sahihi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji Wete kuhakikisha nyaraka hizo zinapatikana kwa ajili ya kufanyiwa uhakiki wa uhalali wa madeni hayo ili hatua za kuombewa malipo ziweze kuchukuliwa kwa lengo la kuepusha kujitokeza kwa malalamiko kwa watumishi wa umma na watoa huduma mbali mbali. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 38: Madeni yaliyokosa Nyaraka za Uchambuzi**

| Nam. | Mdai | Kiasi Cha Deni (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Wasambazaji/Watoa huduma | 1,927,189.74 |
| 2. | Wafanyakazi | 13,698,000.00 |
| 3. | Taasisi Nyengine za Serikali | 17,860,837.00 |
| **Jumla** | | **33,486,026.74** |

### 6.3.8.2 Malipo ya Fedha ambayo Hayajawafikia Wadai shilingi 3,165,220.74

Kwa mujibu wa kifungu namba 29(3)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 kinaleza kwamba "Katika kusimamia madeni Afisa Muhasibu atalipa madeni yote ya mikataba na fedha zote zinazodaiwa ndani ya muda ulioelezwa au uliokubaliwa".

Baada ya kupitia kumbukumbu za Afisi ya Baraza la Mji Wete zikiwemo daftari la fedha taslim na hati za malipo ukaguzi umebaini uwepo wa shilingi 3,165,220.74 ambazo zimelipwa kwa watoa huduma na taasisi mbali mbali kupitia mfumo wa ulipaji wa Baraza lakini fedha hizo hazijawafikia wadai. Hali hii inaweza kupelekea watoa huduma kutokupata haki yao ya malipo kwa wakati jambo ambalo linaweza kupelekea kukosa imani ya kufanya kazi na Baraza. Ulipwaji wa fedha usiomfikia mdai kwa muda muafaka ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Wete kuhakikisha unafanya juhudi za makusudi ili kuweza kuwalipa wadai hao. Mchanganuo wa malipo ya fedha hizo ni kama unavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 39: Malipo ya fedha ambayo hayajawafikia wadai**

| Hati Nam. | Hundi Nam. | Thamani ya Fedha (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 27/6<br>26/6/2023 | TISS | 160,633.74 | Amos Industries ltd | Malipo ya ununuzi wa maji ya kunywa kwa matumizi ya ofisi |
| 28/6<br>27/06/2023 | | 2,980,000 | Chasasa Services Station | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Diesel kwa matumizi ya Baraza la Mji Wete. |
| 29/6<br>26/6/2023 | | 24,587.00 | ZRB | Malipo ya zuio la kodi kwa mfanyabiashara. |
| **Jumla** | | **3,165,220.74** | | |

### 6.3.8.3 Hati za malipo zenye nyaraka pungufu shilingi 5,005,220.74

Kanuni ya 57(1)(2)(b) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za mwaka 2021 inaeleza kuwa malipo yote lazima yaambatanishwe na hati ya malipo ambayo imekamilika nyaraka zote kwa mujibu wa maelekezo ya Hazina na kuidhinishwa na Afisa Mhasibu.

Ukaguzi umebaini kuwa jumla ya shilingi 5,005,220.74 zimetumika kwa ajili ya malipo mbali mbali ya Baraza la Mji Wete lakini baadhi ya nyaraka husika hazikuambatanishwa katika hati za malipo ili kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Hali hii inaweza kuwa imesababishwa na uwepo wa udhibiti wa ndani usioridhisha wa uhifadhi wa vielelezo vya fedha na vielelezo vyengine vinavyohusiana na uendeshaji wa kazi za Baraza au washika fedha wameshindwa kutimiza kikamilifu majukumu yao ya kuweka udhibiti mzuri wa uwekaji wa kumbu kumbu za nyaraka muhimu hasa vielelezo vya hati za malipo jambo ambalo linaweka uwezekano wa kutokea kwa matumizi yasiyoridhisha ya fedha za umma kwenye shughuli mbalimbali za Baraza.

Kutokuambatanishwa nyaraka kamili katika hati za malipo ni kwenda kinyume na Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji Wete kuhakikisha wanaambatanisha vielelezo vyote husika vya malipo katika hati za malipo kwa wakati. Mchanganuo wa hati za malipo zenye nyaraka pungufu ni kama unavyoonekana katika jadweli lifuatalo: -

**Jadweli Nambari 40: Hati za malipo zenye nyaraka pungufu**

| Hati Nam. | Hundi Nam. | Thamani (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 18/8<br>15/8/2022 | TSS | 1,840,000 | Salim Awadh Salim | Malipo kwa ajili ya gharama za chakula. |
| 27/6<br>26/6/2023 | | 160,633.74 | Amos Industries ltd | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa maji ya kunywa kwa matumizi ya ofisi. |
| 28/6<br>27/6/2023 | | 2,980,000 | Chasasa Services Station | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Diesel. |
| 29/6<br>26/6/2023 | | 24,587 | ZRA | Malipo ya zuio la kodi kwa mfanyabiashara. |
| **Jumla** | | **5,005,220.74** | | |

*Chanzo: Hati za malipo*

### 6.3.8.4 Kutokulipwa kwa deni la muda mrefu la ukodishwaji wa Bekari shilingi 6,200,000

Kwa mujibu wa kifungu nambari 29(3)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 kinamtaka Afisa Muhasibu kulipa madeni yote ya mikataba na fedha zote zinazodaiwa ndani ya muda ulioelezwa au uliokubaliwa.

Ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Mji Wete linadaiwa na Bwana Salum Ali Moh'd wa Wete deni ambalo limetokana na kulikodisha Baraza bekari iliopo Bomani Wete kwa bei ya shilingi 150,000 kwa mwezi.

Aidha, ukaguzi umebaini Baraza liliingia katika makubaliano ya ukodishwaji wa bekari hio tangu mwaka 2017 na kulipa deni la miaka mitatu hadi mwaka 2019. Kuanzia tarehe 01.01.2020 hadi ukaguzi unakamilika mnamo mwezi Disemba, 2023 Baraza limelipa shilingi 1,000,000 kwa hati nambari 33/5 ya tarehe 29/5/2023 na hivyo kubakiza deni la shilingi 6,200,000.

Kutokuwalipa wafanyabiashara kwa wakati kunawadhoofisha wafanyabiashara hao na hivyo kukosa imani na Baraza na Serikali kwa ujumla na pia ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza kuhakikisha madeni yote yanafuatiliwa na kulipwa kwa wakati ili kuepusha uzorotaji katika utoaji wa huduma.

### 6.3.8.5 Dosari Katika Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Daladala

Katika kuhakikisha utoaji wa huduma bora kwa jamii Baraza la Mji Wete wameanzisha mradi wa ujenzi wa vituo sita (6) vya kusubiria daladala (Bus Shed) katika maeneo mbali mbali ya Wilaya ya Wete.

Katika mradi huo Baraza la Mji Wete limeingia mkataba wenye kumbu kumbu namba SMZ/D11/W/Q/2022-23/19 na KHC Company Limited kwa thamani ya shilingi 29,700,000 kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivyo (bus shed) ambavyo vimejengwa katika maeneo ya Amani road, Mchangamdogo, Madenjani, Maziwani road, Mzambarau Karim na Mtambwe Kidundo road.

Dosari zilizojitokeza katika utekelezaji huo ni kama zifuatazo:-

- Kukosekana kwa barua ya kumpata (kumuomba) mkandarasi kuja kufanya kazi ya ujenzi.
- Kukosekana kwa ushindani wa bei kwa Wakandarasi tofauti (Three quotation).
- Kutopelekwa Rasimu ya mkataba kwa Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) ili kupatiwa ushauri wa kitaalamu.
- Kwa mujibu wa kifungu nambari 1 cha Masharti Maalum ya Mkataba (SCC 1) kinaeleza kwamba kipindi cha uangalizi wa kazi (defect liability period) ni siku 360 ambapo mkandarasi atamaliziwa 3% ya malipo lakini malipo yote yamefanyika ndani ya miezi minne (malipo ya kwanza yamefanyika 28/10/2022 na ya mwisho yamefanyika tarehe 10/01/2023).
- Kwa mujibu wa muhtasari wa kikao cha mapatano (Negotiation Meeting Minutes) cha tarehe 16/09/2022 unaeleza kuwa malipo yatafanyika sehemu tatu ambapo 50% baada ya kusaini mkataba, 45% baada ya kumaliza kazi na 3% baada ya kipindi cha uangalizi wa kazi (defect liability period). Ukaguzi umebaini kwamba malipo yote yamefanyika kwa awamu mbili ambapo malipo ya awali ni 50% na malipo ya mwisho ni 50%.

Kufanyika kwa malipo bila ya kuzingatia makubaliano ya mkataba kunaweza kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma pindipo Mkandarasi atakaposhindwa kutekeleza masharti ya mkataba waliyokubaliana.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza kuhakikikisha kuwa vipengele vyote vya mikataba vinatekelezwa kama ilivyokubaliwa.

### 6.3.9 KASMA 210 - BARAZA LA MANISPAA CHAKE CHAKE

Ukaguzi wa hesabu za Baraza la Manispaa Chake Chake kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 6.3.9.1 Kutokuwiana kwa taarifa za fedha za bajeti baina ya mpango kazi na ripoti ya utekelezaji shilingi 65,064,609

Katika ukaguzi uliofanyika kupitia taarifa za utekelezaji zilizoandaliwa na Baraza la Manispaa Chake Chake zimebainisha uwepo wa tofauti wa taarifa za fedha zilizoainishwa na kuwasilishwa baina ya mpango kazi wa Baraza na ripoti ya utekelezaji.

Ukaguzi umebaini kuwa jumla ya shilingi 100,000,000 zilibainishwa katika taarifa ya mpango kazi na shilingi 165,064,609 zilibainishwa katika ripoti ya utekelezaji kwa lengo la ukamilishaji wa Mradi wa ujenzi wa maduka 20 katika soko la Chake Chake. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokuwiana kwa taarifa za fedha za bajeti zilizorikodiwa na kuonesha uwepo wa tofauti ya shilingi 65,064,609.

Kutokana na tofauti iliyobainika hapo juu ukaguzi umepata shaka juu ya uhalisia wa taarifa mbili hizo jambo ambalo linaweza kupelekea kujitokeza kwa kiashiria cha ukiukwaji wa taratibu za ufungwaji wa hesabu kukosa kuakisi viwango vya uhasibu kitaifa na kimataifa hatimae taarifa za hesabu kutokuonyesha sura halisi na sahihi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Chake Chake Pemba kuhakikisha kwamba kunakuwa na uwiano wa taarifa za fedha zinazotayarishwa na kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

#### 6.3.9.2 Kukosekana kwa mkataba wa ununuzi wa mafuta shilingi 69,050,540

Kwa mujibu wa kifungu nambari 42(2) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kwamba "Taasisi ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma itapanga mpango wake wa ununuzi na uondoshaji kwa kutumia vigezo vinavyokubalika na hususan utazingatia kutumia mfumo wa mikataba maalumu kwa namna inavyohitajika kutoa huduma bora, zenye gharama nafuu na kwa njia inayoweza kubadilika kwa bidhaa zinazohitajika kila mara au zinazojirudia kila baada ya muda".

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 69,050,540 zimelipwa na Baraza la Manispaa Chake Chake kwa kituo cha mafuta cha Chake Petrol Station kwa ajili ya ununuzi wa mafuta bila ya kuwepo kwa mkataba. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kutokupata huduma iliyo bora na ya uhakika pamoja na uwezekano wa kutokea kwa ununuzi holela wa mafuta. Aidha, ni kwenda kinyume na kifungu nambari 42(2)(b) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza kuhakikisha wanafunga mikataba kwa ununuzi wa bidhaa zote wanazotumia kila mara au zinazojirudia kila baada ya muda kama Sheria inavyoolekeza. Mchanganuo wa mafuta yaliyonunuliwa bila kufungiana mkataba na mtoa huduma ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 41:Malipo yasiyokuwa na mkataba wa ununuzi wa mafuta**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi Kilicholipwa (Tsh.) | Alielipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 30/07 27/7/2022 | TT | 5,907,220 | Chake Petrol Station | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa matumizi ya kazi za Baraza. |
| 48/08 26/08/2022 | | 5,907,220 | | |
| 01/10 27/10/2022 | | 5,907,220 | | |
| 13/11 02/11/2022 | | 5,907,220 | | |
| 36/12 22/12/2022 | | 5,907,220 | | |
| 39/01 24/01/2023 | | 5,907,220 | | |
| 26/02 07/02/2023 | | 5,907,220 | | |
| 54/03 28/03/2023 | | 9,000,000 | | |
| 05/04 13/04/2023 | | 9,600,000 | | |

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi Kilicholipwa (Tsh.) | Alielipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 45/05 24/05/2023 | TT | 5,000,000 | Chake Petrol Station | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa matumizi ya kazi za Baraza. |
| 06/06 13/06/2023 | | 4,100,000 | | |
| **Jumla** | | **69,050,540** | | |

*Chanzo: Kumbukumbu za Hati za Malipo*

### 6.3.9.3 Kukosekana kwa usawa wa taarifa za mapato baina ya Mfumo wa MUTM na Taarifa nyengine za mapato shilingi 22,247,000

Kanuni ya 105(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inamtaka Afisa Mhasibu wa taasisi ya Umma kufanya usuluhishi wa kibenki kila mwezi au wakati wowote kama itakavyoelekezwa na miongozo kutoka Hazina au toleo lolote ambalo litatolewa na Mhasibu Mkuu wa Serikali.

Baada ya kupitia taarifa mbali mbali za mapato ukaguzi umebaini kwamba taarifa za mapato za Baraza la Manispaa Chake Chake zinatofautiana. Utofauti wa mapato yaliyokusanywa unadhihirisha kwamba baadhi ya mapato yanaweza kuwa yanakusanywa nje ya mfumo na hivyo kushindwa kuonekana kwenye taarifa zinazotoka kwenye mfumo. Tofauti hizi pia zinapelekea taarifa za mapato zinazoandaliwa kutoaminika na hesabu za mwisho wa mwaka za Baraza zinazondaliwa kwa kutumia taarifa hizo huweza siziwe na usahihi. Taarifa za mapato tulizozipitia ni pamoja na taarifa za mfumo wa ukusanyaji mapato (MUTM), taarifa za benki (Bank Statement), taarifa za mapato za kila mwezi pamoja na daftari la kukusanyia mapato ya kila siku (Daily Analysis Book). Utofauti uliobainika kwa kiasi kikubwa ulitokana na kutokufanyiwa kwa usuluhishi baina ya taarifa kama ilivyoelekezwa katika kanuni.

Kutokuwiana kwa taarifa za makusanyo ya mapato ya mwaka kunapelekea kutopatikana kwa uhalisia wa mapato yaliokusanywa katika Baraza.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Chake Chake kuhakikisha kwamba taarifa zinazohusiana na fedha za mapato zinakuwa sahihi ili kuwezesha wadau wa taarifa hizo kuwa na imani nazo. Mchanganuo wa utofauti wa taarifa hizo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 42:Tofauti ya taarifa za Mapato baina ya Mfumo wa MUTM na Taarifa nyengine za Mapato**

| Namba | Taarifa zenye utofauti | Tofauti (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Taarifa ya Mfumo wa Ukusanyaji Mapato (MUTM) na Daftari la kukusanyia mapato ya kila siku. (587,803,420 – 592,817,920) | 5,014,500 |
| 2. | Taarifa ya Mfumo wa Ukusanyaji Mapato (MUTM) na taarifa za Benki (Bank Statement). (587,803,420 – 596,419,420) | 8,616,000 |
| 3. | Taarifa ya Mfumo wa Ukusanyaji Mapato (MUTM) na Taarifa za kila mwezi za mapato. (587,803,420 – 596,419,920) | 8,616,500 |
| **Jumla ya tofauti iliyobainika** | | **22,247,000** |

*Chanzo: Taarifa za fedha*

## 6.3.10 KASMA 211 - BARAZA LA MJI MKOANI

Ukaguzi wa hesabu za Baraza la Mji Mkoani kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

### Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi

### 6.3.10.1 Baraza Kutokuchangia shilingi 3,744,617.5 za Asilimia 10 zitokanazo na Mapato ya Ndani kwenye Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Ibara ya 202(h) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2020 - 2025 inazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kuchangia asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwenye Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa madhumuni ya kutanua wigo wa uwezeshaji wa wananchi kiuchumi hususan makundi maalum ya wajasiriamali ikiwemo wanawake asilimia 4, vijana asilimia 4, na asilimia 2 kwa watu wenye ulemavu.

Ukaguzi umebaini kuwa Baraza la Mji Mkoani kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 liliweza kukusanya jumla ya shilingi 371,474,665 na liliwasilisha fedha zenye thamani ya shilingi 33,402,849 sawa na asilimia 9 kwenye Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambao upo chini ya Afisi ya Rais, Kazi Uchumi na Uwekezaji kwa ajili ya kuwawezesha vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ambapo kiasi halisi kilichotakiwa kuwasilisha ni shilingi 37,147,466.5 na kufanya uwepo wa tofauti ya shilingi 3,744,617.5 sawa na asilimia 1 ambazo hazijawasilishwa jambo ambalo ni kwenda kinyume na miongozo iliyotolewa na Serikali. Hali hii inapelekea kutokufikiwa kwa lengo la Serikali la kuwawezesha wananchi kiuchumi hususan makundi maalum ya vijana, wanawake na wenye ulemavu.

Hadi ukaguzi unakamilika, Baraza la Mji Mkoani lilikuwa halijaziwasilisha fedha hizo katika Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji jambo ambalo ni kwenda kinyume na Muongozo uliotolewa na Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha wanafuata kikamilifu maagizo ya Serikali Kuu kwa kuwasilisha michango yao kikamilifu na kwa wakati ili kufikia dhamira njema ya Serikali ya kuwawezesha wananchi kiuchumi na hivyo wananchi kuzidisha imani kwa Serikali yao.

### 6.3.10.2 Utofauti wa Mapato yaliyokusanywa baina ya Taarifa za Benki (Bank Statements) na taarifa nyengine za Mapato shilingi 11,974,020

Kanuni ya 105(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2021 inamtaka Afisa Mhasibu wa taasisi ya Umma kufanya usuluhishi wa kibenki kila mwezi au wakati wowote kama itakavyoelekezwa na miongozo kutoka Hazina au toleo lolote ambalo litatolewa na Mhasibu Mkuu wa Serikali.

Baada ya kupitia taarifa mbali mbali za mapato ukaguzi umebaini kwamba taarifa za mapato za Baraza la Mji Mkoani zinatofautiana. Utofauti wa mapato yaliyokusanywa baina ya taarifa unadhihirisha uwepo wa udhibiti wa ndani usioridhisha. Tofauti hizi pia zinapelekea taarifa za mapato zinazoandaliwa kutoaminika na hesabu za mwisho wa mwaka za Baraza zinazondaliwa kwa kutumia taarifa hizo huweza siziwe na usahihi. Taarifa za mapato zilizopitiwa ni pamoja na taarifa za benki (Bank Statement), taarifa za mapato za kila mwezi pamoja na daftari la fedha taslim (Analysis Book). Utofauti uliobainika kwa kiasi kikubwa ulitokana na kutokufanyiwa kwa usuluhishi baina ya taarifa kama ilivyoelekezwa katika kanuni.

Kutokuwiana kwa taarifa za makusanyo ya mwaka kunapelekea kutopatikana kwa uhalisia wa mapato yaliokusanywa katika Baraza. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza kuhakikisha kwamba taarifa zinazohusiana na fedha za mapato zinakuwa sahihi ili kuwezesha wadau wa taarifa hizo kuwa na imani ya kuzitumia. Mchanganuo wa utofauti wa taarifa hizo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 43: Utofauti wa Taarifa za Mapato

| Namba | Taarifa Zenye Tofauti | Tofauti (Tsh.) |
|---|---|---|
| 1. | Taarifa za Benki (Bank Statement) na Daftari la Fedha Taslim. (374,936,665– 367,553,645) | 7,383,020 |
| 2. | Taarifa za Benki (Bank Statement) na taarifa za mwisho wa mwaka (Financial Statement). (374,936,665– 373,807,665) | 1,129,000 |
| 3. | Taarifa za Benki (Bank Statement) na Taarifa za kila mwezi za mapato. (374,936,665– 371,474,665) | 3,462,000 |
| **Jumla ya Tofauti** | | **11,974,020** |

*Chanzo: Taarifa za fedha*

### 6.3.10.3 Hati za malipo zenye nyaraka pungufu shilingi 5,001,763.2

Kanuni ya 57(1)(2)(b) za Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 imeeleza kuwa malipo yote lazima yaambatanishwe na hati ya malipo ambayo imekamilika nyaraka zote kwa mujibu wa maelekezo ya Hazina na kuidhinishwa na Afisa Mhasibu.

Ukaguzi umebaini kuwa jumla ya shilingi 5,001,763.2 zimelipwa kwa Ndugu Khamis Ali Muhammed kupitia hati namba 341/03 ya tarehe 29/03/2023 ikiwa ni malipo ya ununuzi wa chakula cha Siku Kuu kwa ajili ya watumishi wa Baraza la Mji Mkoani. Dosari iliyobainika ni kutokuambatanishwa kwa nyaraka muhimu ili kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Hali hii imesababishwa na kutokuwepo kwa uimara wa udhibiti wa ndani wa uhifadhi wa vielelezo vya fedha na vielelezo vyengine vinavyohusiana na uendeshaji wa kazi za Baraza. Aidha, washika fedha wameshindwa kuweka udhibiti mzuri wa uwekaji wa kumbu kumbu za nyaraka muhimu hasa vielelezo vya hati za malipo.

Kutokuambatanishwa kwa nyaraka kamili katika hati za malipo ni kwenda kinyume na Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 .

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuambatanisha nyaraka zote husika katika hati za malipo mara tu baada ya malipo kukamilika.

### 6.3.11 KASMA 212 - HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI

Ukaguzi wa hesabu za Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 6.3.11.1 Dosari zilizojitokeza katika ununuzi wa pikipiki

Ukaguzi ulifanya mapitio ya kumbukumbu za manunuzi pamoja na hati za malipo na kubaini kwamba jumla ya shilingi 3,400,000 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa Pikipiki aina ya TVS 150 kwa ajili ya matumizi ya Afisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni.

Dosari zilizobainika katika ununuzi wa pikipiki hio ni kama zifuatazo:-

a. Kukosekana kwa nyaraka za umiliki wa Pikipiki hio kinyume na kifungu nambari 64(1) cha Sheria nambari 6 ya Afisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021.
b. Kutokukatiwa bima kinyume na kanuni ya 124(5) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014.
c. Pikipiki kuanza kutumika kabla ya kupata nambari za usajili.

Hali hii inaweza kupelekea matumizi mabaya ya mali za umma, kuweza kutokea kwa wizi au upotevu wa mali husika pamoja na kuweza kuisababishia hasara Serikali pale itakapotokezea kupata ajali kwa chombo hicho.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kuhakikisha kuwa unafuata Sheria na Kanuni zote za Serikali ili kuepukana na janga lolote linaloweza kutokea kutokana na uzembe uliosababishwa kwa makusudi na Afisi.

#### 6.3.11.2 Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu shilingi 341,495,241

Madeni ni madai halali kwa ajili ya kulipia bidhaa au huduma zilizotolewa kwa mkopo na watoa huduma kwa Halmashauri na madai ya stahiki za watumishi. Madai kwa Halmashauri huwasilishwa na watoa huduma na bidhaa kwa njia ya hati za madai (Invoice).

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni Pemba inadaiwa jumla ya shilingi 341,495,241 na watoa huduma mbali mbali pamoja na watumishi kutokana na kupatiwa huduma. Uwepo wa madeni ya muda mrefu katika Taasisi ya Umma yanayodaiwa kutokana na huduma iliyotolewa yanatoa kiashiria cha kwamba Afisa Mhasibu wa Taasisi ya

Umma ameshindwa kusimamia ulipwaji wa madeni hayo kwa wakati kutokana na kukosekana kwa sera au muongozo wa ulipwaji wa madeni kwa wanufaika.

Kutokulipa madeni kwa wakati kunawakatisha tamaa watoa huduma na bidhaa na kunaweza kusababisha washindwe kuihudumia Halmashauri kwa mkopo hivyo Halmashauri kushindwa kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Kwa upande wa watumishi, madai yao ya muda mrefu yanapunguza hamasa na moyo wa kujitolea katika utoaji wa huduma kwa jamii. Ni muhimu kudumisha mahusiano mema ya kiutendaji kati ya Halmashauri na wadau wake, wakiwemo watumishi na watoa huduma na bidhaa, kwa kuhakikisha Halmashauri inatimiza wajibu wake kwa kulipa madeni kwa wakati. Kutokulipwa kwa madeni kwa wakati ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(1)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni Pemba kuchukuwa juhudi za makusudi kuhakikisha kwamba kunakuwa na sera ya usimamizi wa madeni ili kuepukana na uwepo wa madeni makubwa ambayo hayatoweza kulipika.

Aidha, madeni yote yalipwe ili kuepusha uwezekano wa kuwepo kwa migogoro baina ya Serikali na wananchi. Kipaumbele cha ulipaji kiwekwe kwenye madeni yaliyodumu kwa muda mrefu ikiwa ni pamoja na kufanya uhakiki wa usahihi wa madeni kabla ya kuyalipa. Mchanganuo wa malimbikizo ya madeni ya muda mrefu ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 44: Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu**

| Namba | Jina la Mdai | Kiasi cha Deni (Tshs) |
|---|---|---|
| | **Madeni ya Watoa Huduma** | |
| 1. | Khamis Yussuf Hamad | 51,489,300 |
| 2. | Moh'd Khalfan Adeyoum | 30,633,474 |
| 3. | Misufini Stationary Centre | 15,452,500 |
| 4. | Salum Suleiman Hamad | 10,000,000 |
| 5. | Mbarouk Salim Ali | 8,052,320 |
| 6. | Nourbhai Auto Services | 7,668,000 |
| 7. | Shaam Group of Companies Limited | 7,200,000 |
| 8. | Haji Omar Mkeka | 5,000,000 |
| 9. | Salim Said Iddi | 2,112,082 |
| 10. | Ofisi ya Rais Fedha na Mipango | 1,730,000 |
| 11. | Moh'd Ali Hemed | 1,200,000 |

| Namba | Jina la Mdai | Kiasi cha Deni (Tshs) |
|---|---|---|
| **Madeni ya Watoa Huduma** | | |
| 12. | Omar Khamis Hamad | 950,000 |
| 13. | Suleiman Moh'd Omar | 781,160 |
| 14. | Massoud Abrahman Massoud | 646,300 |
| 15. | Limbani Farm Inputs | 514,000 |
| 16. | Suleiman Said Omar | 464,000 |
| 17. | Kana Catering Trade | 375,000 |
| 18. | Tahfif Auto Works | 270,250 |
| 19. | Vista Auto Parts | 265,000 |
| 20. | Redio Jamii Micheweni Pemba | 250,000 |
| 21. | Rashid Salim Said | 121,000 |
| 22. | Yussuf Grafix | 120,000 |
| **Jumla Ndogo (A)** | | **145,294,386** |
| **Madeni ya Watumishi** | | |
| Posho la TUTU | | 119,260,000 |
| Posho la Nauli/Bus Fare | | 76,940,855 |
| **Jumla Ndogo (B)** | | **196,200,855** |
| **Jumla Kuu (A + B)** | | **341,495,241** |

*Chanzo: Kitengo cha Uhasibu*

### 6.3.11.3 Dosari katika ununuzi wa mashine za kukaushia mwani

Baada ya kupitia hati za malipo ukaguzi umebaini kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ilifanya ununuzi wa mashine mbili za kukaushia mwani (Solar dryer) kupitia ufadhili wa UNCDF, kutoka kampuni ya VIVUNES kwa jumla ya shilingi 53,562,000 ambapo mashine hizo zilifungwa katika jengo la kaushio lililojengwa Kiuyu Maziwang'ombe. Ukaguzi umebaini dosari zifuatazo katika ununuzi huo:-

- Kukosekana kwa nyaraka zinazoonesha mchakato mzima wa kumpata mtoa huduma.
- Kukosekana kwa hati ya madai ya malipo (Invoice).
- Kutokukatwa kwa kodi ya zuio.
- Kukosekana kwa stakabadhi ya malipo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kuhakikisha unafuata taratibu zote za manunuzi pamoja na kuambatanisha vielelezo vyote husika katika hati za malipo mara tu baada ya malipo kukamilika. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016. Mchanganuo wa hati za malipo za ununuzi wa mashine hio ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 45: Malipo ya ununuzi wa mashine za kukaushia Mwani

| Hati Namba | Hundi Namba | Thamani (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 2/11 ya 26/11/2022 | TISS | 42,759,200 | Halmshauri Wilaya ya Micheweni (VIVUNES ) | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa mashine ya kukaushia mwani. |
| 1/04 ya 5/4/2023 | | 10,802,800 | | |
| **Jumla** | | **53,562,000** | | |

# SURA YA SABA



# 7.0 TAARIFA ZA UKAGUZI WA HESABU ZA IDARA MAALUM ZA SMZ

## 7.1 UTANGULIZI

Sura hii inaelezea matokeo ya ukaguzi wa Idara Maalum za SMZ ambapo jumla ya Vikosi Vitano (5) vilikaguliwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Sura hii inaonyesha masuala muhimu yanayohitaji kushughulikiwa na Serikali, Baraza la Wawakilishi pamoja na Uongozi wa taasisi husika ili kuhakikisha ufanisi katika utendaji wa shughuli za taasisi hizo.

Yafuatayo ni matokeo ya ukaguzi kwenye ukaguzi wa Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

### 7.1.1 FUNGU D 04 - KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM)

Ukaguzi wa hesabu za Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 7.1.1.1 Kukosekana kwa bajeti ya matumizi shilingi 345,398,555

Kifungu nambari 31(3) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kwamba "Afisa Mhasibu atachukua hatua zinazofaa kutumia ndani ya bajeti iliyotengwa na kuzuia matumizi ya ziada na kuwasilisha taarifa kwa Waziri anayehusika, bodi ya usimamizi na Hazina ya Serikali".

Ukaguzi ulipitia taarifa za kibenki (Bank Statement) pamoja na madaftari ya kumbukumbu ya fedha taslim (Cash Book) na kubaini kuwa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kilifanya matumizi ya shilingi 345,398,555 kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya Kikosi bila kutengewa bajeti ya matumizi ya fedha hizo.

Kufanya matumizi bila kuwepo kwa bajeti na mpango kazi wa matumizi hayo kunaweza kupelekea upotevu wa fedha za Serikali, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kuhakikisha unaandaa bajeti ya mapato na matumizi pamoja na kufanya ufuatiliaji wa matumizi ya kila kifungu kilichoanishwa ili kuepuka kujitokeza kwa matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Mchanganuo wa matumizi yaliyofanywa bila ya kuzingatia bajeti ya matumizi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

## Jadweli Nambari 46: Matumizi yaliyofanywa bila ya kuzingatia bajeti

| Hati Namba | Aliyelipwa | Thamani (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 8/07/2022 | Mkuu wa KMKM | 14,000,000 | Uchimbaji wa kisima Mangapwani |
| | | 4,480,000 | Kuboresha sikukuu |
| | | 1,200,000 | Mshahara wa Wataalam |
| 13/7/2022 | | 3,040,000 | Nauli na posho la safari ya Pemba |
| 15/7/2022 | | 400,000 | Malipo ya Mishahara |
| 17/7/2022 | | 10,379,000 | Ujenzi wa Ngara |
| | | 5,379,000 | Ujenzi wa Ngara |
| | | 4,235,000 | Matumizi mbalimbali ya Kikosi |
| 18/7/2022 | | 4,776,000 | Malipo ya ununuzi wa vifaa |
| 19/7/2022 | | 1,150,000 | Malipo ya safari kikazi |
| | | 680,000 | |
| | | 12,410,000 | Malipo ya ununuzi wa vifaa |
| | | 3,730,000 | Malipo ya safari kikazi |
| | | 10,000,000 | Malipo kwa ajili ya ujenzi |
| | | 20,000,000 | Malipo ya matumizi mbalimbali |
| | | 57,375,225 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa |
| | | 19,143,590 | |
| 13/6/2023 | Rooi Traders Company | 40,955,100 | Malipo ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| | United Traders | 13,037,826 | |
| | United Ram Construction Company | 2,928,260 | |
| 25/6/2023 | Menei Enteprises | 16,448,391 | |
| 16/7/2022 | Mkuu wa KMKM | 14,000,000 | Malipo kwa ajili ya uchimbaji wa kisima |
| 29/7/2022 | | 5,379,000 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| 5/10/2022 | | 13,996,765 | |
| 8/10/2022 | Alhilal General Trading | 14,292,832 | |
| 5/11/2022 | Mkuu wa KMKM | 3,910,750 | |
| 9/01/2023 | | 12,779,088 | |
| 10/1/2023 | | 14,142,728 | |
| 17/2/2023 | United Traders | 21,150,000 | |
| **Jumla** | | **345,398,555** | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za Malipo,2023*

#### 7.1.1.2 Kutokufanyiwa Uchunguzi na upimaji kwa bidhaa ambazo zimepokelewa (Inspections and Test)

Kifungu nambari 10.1 cha Masharti Maalum ya Mkataba kinaeleza ya kwamba "Uchunguzi na upimaji wa bidhaa zitakazopokelewa zitafanyika kwa njia ya ubora na idadi ya bidhaa". Aidha, kifungu nambari 18.6 cha Masharti Maalum ya Mkataba kinaeleza ya kwamba "Malipo kwa mujibu wa Mkataba yatalipwa kwa Mzabuni kwa fedha za Kitanzania kama inavyoelezwa ambapo asilimia 100 ya bei ya Mkataba italipwa baada ya kupokelewa, kuchunguzwa na kukubalika kwa bidhaa".

Ukaguzi umepitia taarifa mbali mbali za upokeaji wa bidhaa na kubaini kutokufanyiwa kwa uchunguzi na upimaji wa bidhaa zinazopokelewa kama Makubaliano ya Mkataba yanavyoelekeza jambo ambalo linaweza kupelekea kupokelewa kwa bidhaa ambazo hazina ubora au ziko chini ya idadi iliyohitajika kwa mujibu wa makubaliano, na hivyo kupelekea upotevu wa fedha za umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa KMKM kuhakikisha unazingatia masharti ya mkataba ikiwemo kufanya uchunguzi na majaribio ya bidhaa zinazopokelewa ili kuepusha kujitokeza kwa dosari za kiutendaji katika utekelezaji wa kazi za miradi.

#### 7.1.1.3 Dosari zilizobainika katika Usimamizi wa Mkataba wa Ununuzi wa Decompression Chamber

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kuwa mnamo tarehe 17 Disemba, 2021 Kikosi cha KMKM kilitiliana saini ya makubaliano na Kampuni ya M/S Rom Solutions Limited kwa thamani ya shilingi 2,182,047,375 kwa ajili ya usambazaji na ufungaji wa Decompression Chamber. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kufanyika kwa malipo kwa kutumia ankara (Invoice) bila ya kufuata vigezo vilivyowekwa ikiwemo kuwasilisha cheti (certificate) cha malipo kulingana na kazi zilizokamilika jambo ambalo ni kinyume na kifungu cha 46.1 cha Masharti ya Ujumla ya Mkataba (GCC) kinachoeleza kuwa malipo ya kazi iliyofanyika yatalipwa ndani ya siku 28 baada ya kutolewa kwa cheti cha malipo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa KMKM kuhakikisha unasimamia ipasavyo mikataba inayoingia ili kuepusha kujitokeza kwa dosari ambazo zinaweza kupelekea kuitia hasara Serikali.

#### 7.1.1.4 Kuchelewa kufika kwa vifaa tiba katika eneo la Mradi

Ukaguzi ulifanya mahojiano na Afisa mpokeaji wa vifaa ambae ni Mkuu wa Idara ya Ugawaji wa KMKM na kueleza kutokupokelewa kwa vifaa tiba katika Mradi wa Decompression Chamber kulikotokana na kucheleweshwa kuwasilishwa kwa vifaa hivyo katika eneo la mradi jambo ambalo limepelekea kutokufikiwa kwa lengo lililokusudiwa na hivyo kuchelewa kukamilika kwa mradi uliokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kuhakikisha kuwa unakutana na Mzabuni ili kuweza kufanya uwasilishaji wa vifaa kulingana na makubaliano ya mkataba kwa lengo la kuepusha kujitokeza kwa dosari mbali mbali katika utekelezaji wa mradi.

#### 7.1.1.5 Kutokuwasilishwa kwa vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya shilingi 176,228,200

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kuwa mnamo tarehe 10 Januari, 2022 Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kilisaini hati ya makubaliano na Kampuni ya M/S United Traders kwa thamani ya shilingi 5,124,470,495 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi ambapo mkataba huo haukuonesha tarehe ya kukamilika kwake.

Ukaguzi umefanya mapitio ya zabuni iliyotolewa na Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo pamoja na kujiridhisha na makubaliano ya mkataba uliosainiwa pande mbili na kubaini kuwa kwa mujibu wa mchanganuo wa majadweli ya uwasilishwaji wa vifaa vya ujenzi ilibainika vifaa vyenye thamani ya shilingi 176,228,200 ambapo hadi ukaguzi unakamilika vifaa hivyo havikuwasilishwa kwa mujibu wa makubaliano yaliyofanyika.

Kutokuwasilishwa kwa vifaa hivyo kunaweza kutoa viashiria vya kukosekana kwa umakini wa usimamizi wa mikataba jambo ambalo huwenda likapelekea kujitokeza kwa vitendo vya ucheleweshwaji wa kukamilika kwa mradi na hatimae kutaigharimu Serikali kutumia fedha za ziada kwa ajili ya ukamilishaji wa mradi huo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kuongeza jitihada na umakini kwa kumsimamia mtoa huduma aweze kuwasilisha vifaa vilivyobaki ili kuweza kukamilisha mahitaji ya utekelezaji wa mradi kwa wakati. Mchanganuo wa vifaa ambavyo havijawasilishwa ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 47: Vifaa vya ujenzi ambavyo havijawasilishwa na mzabuni**

| Namba | Aina ya Kifaa | Mahitaji ya Vifaa kwa mujibu wa Mkataba (A) | Vifaa Vilivyopokelewa (B) | Vifaa ambavyo havijapokelewa C= (A-B) | Bei ya Mkataba (Tsh.) (D) | Thamani ya Vifaa ambavyo havijapokelewa (Tsh.) (C) X (D) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Saruji | 6779 | 3750 | 3029 | 18,500 | 56,036,500 |
| 2 | Mchanga | 163 | 130 | 33 | 300,000 | 9,900,000 |
| 3 | Tofali | 29344 | 21,633 | 7711 | 2,700 | 20,819,700 |
| 4 | Nondo m16 | 1921 | 1372 | 549 | 56,000 | 30,744,000 |
| 5 | Nondo m12 | 1451 | 1012 | 439 | 32,000 | 14,048,000 |
| 6 | AC 1.5 ton | 23 | 20 | 3 | 2,000,000 | 6,000,000 |
| 7 | Feni | 32 | 30 | 2 | 150,000 | 300,000 |
| 8 | Gari ya Mawe | 17 | 15 | 2 | 190,000 | 380,000 |
| 9 | Gari ya Kifusi | 15 | 14 | 1 | 200,000 | 200,000 |
| 10 | Gari ya Kokoto | 83 | 21 | 62 | 330,000 | 20,460,000 |
| 11 | Mbao 2x2 | 759 | 642 | 117 | 13,000 | 1,521,000 |
| 12 | Mbao 2x6 | 432 | 80 | 352 | 37,000 | 13,024,000 |
| 13 | Mbao 1x10 | 38 | 18 | 20 | 52,000 | 1,040,000 |
| 14 | Bati | 277 | 250 | 27 | 65,000 | 1,755,000 |
| **Jumla** | | | | | | **176,228,200** |

*Chanzo: Taarifa za Ukaguzi, 2023*

### 7.1.1.6 Malipo ambayo hayakufuata taratibu za manunuzi shilingi 246,985,389

Kwa mujibu wa kanuni nambari 57(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2020, inaeleza kwamba Taasisi ya Ununuzi haitoruhusiwa kuvunjavunja manunuzi kwa lengo la kukwepa uitishaji wa zabuni (split contract).

Ukaguzi umebaini kwamba Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kimefanya malipo yenye thamani ya shilingi 246,985,389 kwa ajili ya upatikanaji wa huduma mbali mbali za uendeshaji wa majukumu ya Kikosi. Miongoni mwa matumizi ya fedha hizo ni kama ifuatavyo:-

- Kufanyika kwa uhaulishaji wa fedha zenye thamani ya shilingi 57,375,224 kwa ajili ya usambazaji wa vifaa vya ujenzi awamu tofauti Ngara Kibweni.
- Kufanyika kwa malipo ya fedha zenye thamani ya shilingi 51,229,165 kwa ajili ya usambazaji wa vifaa mbalimbali vya ujenzi wa Mnara wa Mbao.

- Kufanyika kwa matumizi ya shilingi 138,381,000 kwa ajili ya ununuzi wa chakula cha walinzi wa malindo 15 ya nje ya kambi kwa miezi tofauti.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni ukiukwaji wa taratibu za manunuzi zilizopelekea kujitokeza kwa kitendo cha ununuzi kwa njia ya kuvunjwavunjwa ili kukwepa utoaji wa zabuni kwa mujibu wa sheria.

Kufanya ununuzi kwa njia ya kuvunjavunja kunapelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na malipo ya wazabuni wanaoingia mikataba ya kazi au usambazaji wa bidhaa au huduma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kuweka msisitizo katika usimamizi wa ununuzi unaofanyika kwa lengo la kuzingatia matakwa ya Sheria ya Ununuzi ili kuepuka athari inayoweza kujitokeza kutokana na kushindwa kusimamia matakwa ya Sheria hiyo. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 48: Malipo ambayo hayakufuata taratibu za manunuzi**

| Hati Namba | Thamani (Tsh.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| **Ununuzi wa Vifaa vya Ujenzi Ngara Kibweni** | | | |
| 13/08/2022 | 14,343,806 | MKUU WA KMKM | Uhaulishaji wa fedha kwa ajili ya usambazaji wa vifaa vya ujenzi wa Ngara Kibweni kwa awamu tofauti. |
| 04/09/2022 | 14,343,806 | | |
| 04/09/2022 | 14,343,806 | | |
| 05/09/2022 | 14,343,806 | | |
| **Jumla Ndogo (A)** | **57,375,224** | | |
| **Ununuzi wa Vifaa vya Ujenzi wa Mnara wa Mbao** | | | |
| 11/1/2023 | 13,919,025 | MKUU WA KMKM | Malipo ya fedha kwa ajili ya usambazaji wa vifaa mbalimbali vya ujenzi wa Mnara wa Mbao. |
| 12/1/2023 | 11,265,400 | | |
| 13/1/2023 | 14,952,530 | | |
| 15/1/2023 | 11,092,210 | | |
| **Jumla Ndogo (B)** | **51,229,165** | | |
| **Ununuzi wa Chakula cha Walinzi wa Malindo 15** | | | |
| 1/8 ya 29/07/2022 | 13,076,000 | MOSAL TRADING ENTERPRISES | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa chakula cha walinzi wa malindo 15 ya nje ya kambi kwa miezi tofauti |
| 1/9 ya 29/08/2022 | 13,238,000 | MKUU WA KMKM | |
| 4/10 ya 24/10/2022 | 13,510,000 | KMKM CANTEEN | |
| 1/12 ya 28/11/2022 | 13,810,000 | | |
| 16/9 ya 22/09/2022 | 13,210,000 | MKUU WA KMKM | |
| 7/12 ya 23/12/2023 | 13,810,000 | | |
| 3/2 ya 04/02/2023 | 14,155,000 | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 13/4 ya 02/04/2023 | 14,245,000 | MKUU WA KMKM | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa chakula cha walinzi wa malindo 15 ya nje ya kambi kwa miezi tofauti |
| 25/4 ya 06/04/2023 | 14,245,000 | | |
| 20/6 ya 02/06/2023 | 15,082,000 | | |
| **Jumla Ndogo (C)** | **138,381,000** | | |
| **Jumla Kuu (A+B+C)** | **246,985,389** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Nyaraka za Kumbukumbu za Hati za Malipo, 2023*

### 7.1.1.7 Kukosekana kwa mikataba ya ulinzi baina ya Kikosi cha Kuzuia Magendo na Kampuni za mafuta shilingi 45,000,000

Kifungu nambari 63(3) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa kazi itatolewa kwa kuwepo na mkataba uliosainiwa na pande mbili baina ya mtoa huduma na mpokeaji wa huduma.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya taarifa za kibenki (Bank Statement) pamoja na taarifa za fedha taslim za hesabu za KMKM na kubaini kwamba Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kimepokea jumla ya shilingi 45,000,000 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kutokana na huduma ya ulinzi katika eneo la Mtoni (Depot) bila ya kuwepo kwa Mikataba ya makubaliano ya Ulinzi na Makampuni ya Mafuta.

Kukosekana kwa mikataba ya kazi za ulinzi kunaweza kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za mapato yanayotokana na utoaji wa huduma isiyokuwa na mafungamano ya kisheria.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kuchukua hatua za kuhakikisha kazi zote zinazofanywa ziandaliwe mikataba maalum itakayoonesha tarehe ya kuanza na kumaliza, gharama ya mkataba, na masharti mengineyo yanayohusiana na uvunjwaji, adhabu au gharama za tozo zitokanazo na kushindwa kwa pande moja kutekeleza masharti waliyokubaliana. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Jadweli Nambari 49:Mapato yatokanayo na kazi ya Ulinzi wa Kampuni za Mafuta**

| Namba | Jina la Kampuni | Kiasi cha Fedha kilichopokelewa (Tsh.) |
|---|---|---|
| 1 | GAPCO | 15,750,000 |
| 2 | United Group | 13,500,000 |
| 3 | Zanzibar Petroleum | 15,750,000 |
| **Jumla** | | **45,000,000** |

*Chanzo: Uchambuzi wa nyaraka za malipo, 2023*

### 7.1.1.8 Malipo yaliyofanywa kwa njia ya Fedha Taslimu shilingi 42,565,000

Kanuni ya 58(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2021 inaeleza kwamba malipo yote ya matumizi ya Taasisi za Kibajeti na Serikali za Mitaa lazima yafanywe kwa kutumia njia za kieletroniki.

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kimefanya malipo yenye thamani ya shilingi 42,565,000 kwa ajili ya ununuzi na upatikanaji wa huduma mbali mbali. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni Kikosi kutokutumia mfumo wa kibenki na badala yake kufanya matumizi kwa njia ya mfumo wa fedha taslim jambo ambalo huenda likapelekea uwepo wa viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za umma au kujitokeza kwa udanganyifu unaotokana na ulipwaji wa malipo.

Kufanya matumizi kwa njia ya fedha taslimu ni kwenda kinyume na Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kuhakikisha kwamba malipo yote yanafanyika kwa njia ya mfumo wa kibenki kwa lengo la kuhakikisha Serikali inapata mapato yatokanayo na kodi ya zuio kwa watoa huduma mbali mbali pamoja na kuondoa uwezekano wa matumizi yasiyoridhisha ya fedha za umma. Mchanganuo wa malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 50: Malipo yaliyofanyika kwa njia ya fedha taslimu**

| Hati Namba | Thamani (Tsh.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 42/7/2022 | 10,379,000 | MKUU WA KMKM | Malipo kwa ajili ya ujenzi wa banda la Fiber boat |
| 31/7/2022 | 4,776,000 | | Malipo kwa ajili ya utengenezaji wa life Jacket. |
| 33/7/2022 | 12,410,000 | | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali. |
| 3/10/2022 | 5,000,000 | | |
| 8/12/2022 | 10,000,000 | | |
| **Jumla** | **42,565,000** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za Malipo, 2023*

### 7.1.1.9 Kutotekelezeka kwa baadhi ya miradi ya Maendeleo shilingi 14,420,000,000

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kilipanga kutekeleza miradi ya maendeleo mbalimbali yenye thamani ya shilingi 14,420,000,000. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokuzingatiwa kwa mpango kazi kulikopelekea kutokutekelezeka kwa wakati miradi hiyo jambo ambalo linaweza kupelekea kujitokeza kwa ongezeko la gharama linalosababishwa na kupanda kwa bei za bidhaa na hatimae gharama ya utekelezaji wa miradi hio kutoendana na gharama za awali. Aidha, uchelewaji wa utekelezaji wa miradi unapelekea kukosekana kwa tija iliyokusudiwa ya kuwasogezea wananchi huduma karibu na makaazi yao.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kuhakikisha unasimamia vyema utekelezaji wa miradi iliyopangwa kwa lengo la kuleta ufanisi na upatikanaji wa huduma bora pamoja na kukiwezesha Kikosi kuongeza mapato na hatimae kuweza kujitegemea. Mchanganuo wa miradi hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 51:Miradi ambayo haikutekelezwa**

| Jina la Mradi | Tarehe ya Kuanza | Tarehe ya Kukamilika | Makisio | Fedha iliyoingizwa na kutumika | Asilimia ya Utekelezaji (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| Mradi wa uzamiaji na Uokozi | 2021/2022 | 2024/2025 | 9,320,000,000 | 1,745,637,900 | 18.8 |
| Mradi wa Ujenzi wa Mahanga ya KMKM | 2021/2022 | 2023/2024 | 3,000,000,000 | 2,043,396,170 | 68 |
| Ujenzi wa Vituo vya Uzamiaji na Uokozi | 2021/2022 | 2023/2024 | 2,100,000,000 | 0 | 0 |
| **Jumla** | | | **14,420,000,000** | | |

*Chanzo: Mpango Kazi na Utekelezaji wa KMKM, 2022/2023*

## KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM) PEMBA

### 7.1.1.10 Dosari Katika utoaji wa zabuni za Usambazaji wa vifaa vya Ujenzi

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) Zanzibar kimepewa jukumu la ujenzi wa miradi mbali mbali ya masoko na madarasa katika Mkoa wa Kaskazini Pemba. Katika utekelezaji wa kazi hizo KMKM imetoa zabuni ya usambazaji wa vifaa vya ujenzi kwa kampuni ya United Traders Enterprises ya Saateni Zanzibar.

Katika ukaguzi uliofanyika dosari mbalimbali zinazohusu utoaji wa zabuni hiyo zilibainika kama ifuatavyo;

a. Kutokuwepo kwa kumbukumbu za utolewaji wa zabuni za ununuzi wa vifaa vya ujenzi.

b. Mikataba ya zabuni ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi baina ya Kikosi cha KMKM na Kampuni ya United Traders Enterprises na Iddi Hamad Ali haikupatikana kwa ukaguzi.

c. Kukosekana kwa uthibitisho wa usajili wa Kampuni katika Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

d. Kutokuwepo kwa mchanganuo wa vifaa ambavyo mfanyabiashara huyo amepewa kazi ya kuvisambaza.

e. Kutokujulikana kwa idadi ya fedha zilizotumika katika utekelezaji wa kila mradi pamoja na vifaa halisi vilivyotumika katika kila mradi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa KMKM Pemba kuhakikisha unafuata sheria na taratibu za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo sheria na taratibu za utoaji wa zabuni.

### 7.1.1.11 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 434,782,608

Kanuni ya 57(1)(2)(b) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2021 inaeleza kuwa malipo yote lazima yaambatanishwe na hati ya malipo ambayo imekamilika vielelezo vyote kwa mujibu wa maelekezo ya hazina na kuidhinishwa na Afisa Mhasibu.

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 434,782,608 zimetumika kwa matumizi mbali mbali lakini vielelezo husika havikuambatanishwa na hati hizo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutokuambatisha vielelezo katika hati za malipo kunapelekea kushindwa kuthibitisha uhalali wa malipo hayo na pia ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa KMKM Kamandi ya Pemba kuhakikisha unazifuata taratibu za malipo kiukamilifu ikiwemo kuambatanisha vielelezo vya malipo katika hati husika za malipo kwa wakati. Mchanganuo wa hati za malipo zenye vielelezo pungufu ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 52: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu**

| Hati Namba | Hundi Namba | Thamani (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 6/7 ya 6/7/2022 | TT | 260,869,565 | United Traders Enterprises. | Uhaulishaji wa fedha kwa ajili ya kumlipa United Traders Enterprises kwa malipo ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa madarasa na masoko. |
| 17/7 ya 19/7/2023 | | 173,913,043 | | |
| **Jumla** | | **434,782,608** | | |

*Chanzo: Hati za malipo.*

## 7.1.2 FUNGU D 02 - JESHI LA KUJENGA UCHUMI

Ukaguzi wa hesabu za Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar (JKU) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

### 7.1.2.1 Kutokuwepo kwa Mpango Maalum wa Mafunzo

Kanuni nambari 74(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inazitaka "Taasisi zote za Serikali kuandaa mpango maalum wa mafunzo pamoja na kutenga fedha kwa ajili ya mafunzo hayo". Aidha, kwa mujibu wa waraka wenye kumbukumbu namba CAB.40/158/01/54 na CAB.40/158/01/37 kutoka Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora unazitaka Wizara na Taasisi za umma kufanya maandalizi ya mpango wa mafunzo ili kujua mahitaji (Training Needs Assessment) na kuwasilisha mpango wa mafunzo.

Ukaguzi umebaini kwamba Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar halikuandaa Mpango Mkuu wa mafunzo ambao ungesimamia masuala yote yanayohusiana na mafunzo kwa watendaji wake na kuuwasilisha kwa mujibu wa kanuni na toleo nililolinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar kuhakikisha unaandaa mpango wa Mafunzo, mpango wa tathmini ya mahitaji pamoja na bajeti ya mafunzo ili kuepusha kujitokeza kwa mizozo au malalamiko kwa watumishi wa umma watakaonyimwa nafasi ya kushiriki katika mafunzo.

### 7.1.2.2 Ucheleweshwaji wa uwasilishwaji wa Vifaa vya Ujenzi

Kwa mujibu wa barua ya tarehe 08 Agosti, 2023 kutoka Idara ya Majenzi na Viwanda JKU Pemba kwenda kwa Mkuu wa Zoni Pemba inaelezea mahitaji ya Vifaa vya ujenzi kwa Jengo la Afisi ya Wawi Pemba.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Idara ya Ujenzi na Viwanda ya JKU Pemba inayotekeleza mradi wa ujenzi wa jengo la Afisi Kuu ya JKU Wawi Pemba imesitisha ujenzi wa jengo hilo kutokana na kuchelewa kuletwa vifaa vya ujenzi ambavyo wameviomba ili kukamilisha ujenzi huo kwa wakati.

Aidha, imebainika Idara ya ujenzi iliomba kuwasilishiwa vifaa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi mnamo tarehe 08 Agosti, 2023 lakini hadi ukaguzi unakamilika vifaa hivyo havijawasilishwa jambo ambalo linaweza kupelekea kutokukamilika kwa mradi huo kwa wakati uliopangwa na hatimae kuingiza hasara Serikali kutokana na mabadiliko ya bei za bidhaa siku hadi siku.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar kuhakikisha linafanya ufuatiliaji wa vifaa hivyo kwa lengo la kuweza kupatikana haraka ili kutimiza malengo yaliyokusudiwa kwa ufanisi na kwa wakati. Aidha, ni vyema kuzingatia masharti ya mkataba ikiwemo kuangalia uwezekano wa kutoza adhabu ya fidia kulingana na idadi ya siku alizochelewa kwa mujibu wa mkataba husika. Mchanganuo wa vifaa vilivyochelewa kuwasilishwa ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 53:Vifaa vilivyochelewa kuwasilishwa katika eneo la ujenzi**

| Nambari | Vifaa vya Umeme | Kiwango |
|---|---|---|
| 1. | Main switch 3Phase | 1 pc 6*12 |
| 2. | Waya 4mm | 9 Rolls |
| 3. | Taa za ukutani | 100 |
| 4. | Siling holder | 15 pcs |
| 5. | Connector Box | 100 Pcs |
| 6. | Angle holder | 20 pcs |
| 7. | Intermidiate switch | 4 pcs |
| 8. | Engle Sever lamp | 35 pcs |
| 9. | Two gang two Way | 8 Pcs |
| 10. | Grout | Box 2 |
| 11. | Wall taiz | Srm 430 |
| 12. | Gypsum | 100 Pkt |
| 13. | Rangi nyeupe | ndoo 50 |
| 14. | Rangi cream ya mafuta | ndoo 15 |

| | | |
|---|---|---|
| 15. | Rangi ya antifangas ya Cream | ndoo 12 |
| 16. | Rangi nyeusi | ndoo 4 |
| 17. | Rangi ya Cream ya Maji | ndoo 25 |
| 18. | PVC | Pipe 4 |
| 19. | Sim Tank | 5000 ltr |
| 20. | PPR Pipe | 1 |
| 21. | PPR Gate valve1 | valve1 |
| 22. | Flexible Pipe | 3 FTS |
| 23. | Misumari ya kufungia basen | 9 Pcs |
| 24. | Bash 1 | Ps 1 |

*Chanzo: Barua ya maombi ya Vifaa vya ujenzi*

### 7.1.2.3 Kukosekana kwa Uhalisia katika utayarishwaji wa nyaraka za Makisio ya Gharama za Ujenzi (BOQ) zilizopelekea kuwepo tofauti shilingi 258,747,000

Ukaguzi ulitembelea Mradi wa Afisi Kuu Wawi, Chambani pamoja na Bambi Kim na kubainika uwepo wa mapungufu mbali mbali katika utayarishwaji wa BOQ na mahitaji halisi ya ujenzi huo, jambo ambalo linaweza kuathiri gharama halisi zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo. Kuwepo kwa ongezeko la gharama za makadirio ya kazi kutapelekea kuathiri bajeti ya ujenzi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi kuhakikisha kuwa unazipitia kwa pamoja nyaraka za Makisio ya Gharama za Ujenzi (BOQ) baina ya Watayarishaji, Idara ya Majenzi na Viwanda. Mchanganuo wa gharama zilizosababisha tofauti kujitokeza baina ya nyaraka za Makisio ya Gharama za Ujenzi (BOQ) pamoja a Gharama halisi zilizotumika ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 54:Kutokuwepo kwa uhalisia katika utayarishwaji wa nyaraka za BOQ**

| Mahitaji | Kiwango cha BOQ | Kiwango Halisi | Tofauti | Thamani (Tsh.) | Tofauti (Tsh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| Concrete Bolcks Grade A 6" | 6,200 | 13,000 | 6,800 | 3,000 | 20,400,000 |
| Aggregate Trip | 65 | 89 | 24 | 750,000 | 18,000,000 |
| **Reinforcement of Yield:** | | | | | |
| 16mm diameter | 32 | 33 | 1 | 2,900,000 | 2,900,000 |
| 12mm diameter | 22 | 24 | 2 | 2,900,000 | 5,800,000 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 8mm diameter | 4 | 5 | 1 | 3,000,000 | 3,000,000 |
| Binding wire | 6 | 58 | 52 | 100,000 | 5,200,000 |
| Gypsum Powder | 280 | 300 | 20 | 40,000 | 800,000 |
| Saw | 2 | 6 | 4 | 5,000 | 20,000 |
| Safety Helment | 90 | 100 | 10 | 20,000 | 200,000 |
| Wooden Float | 4 | 34 | 30 | 30,000 | 900,000 |
| Spirit level Small size | 25 | 26 | 1 | 20,000 | 20,000 |
| **Crane machine with all Accessories:** | | | | | |
| 2*4*20 | 4,250 | 8,000 | 3,750 | 25,000 | 93,750,000 |
| 2*2*20 | 3,250 | 6,103 | 2,853 | 17,000 | 48,501,000 |
| 1*10*18 ficial board | 350 | 1,150 | 800 | 50,000 | 40,000,000 |
| Roof Sheet nails of 5′ | 100 | 400 | 300 | 7,000 | 2,100,000 |
| Roof Sheet nails of 4′ | 100 | 450 | 350 | 7,000 | 2,450,000 |
| Roof Sheet nails of 3′ | 75 | 325 | 250 | 7,000 | 1,750,000 |
| Roof Sheet nails of 2.5′ | 25 | 75 | 50 | 7,000 | 350,000 |
| Concrete nails 4″ | 10 | 250 | 240 | 6,500 | 1,560,000 |
| Concrete nails 3″ | 5 | 454 | 449 | 6,500 | 2,918,500 |
| 2G1W Switch | - | 15 | 15 | 20,000 | 300,000 |
| Box Screw | 2 | 50 | 48 | 9,500 | 456,000 |
| Conduit Pipe 20mm(Omani) | 40 | 1,050 | 1,010 | 4,000 | 4,040,000 |
| PPR pipe1″(UK) | 2 | 25 | 23 | 25,000 | 575,000 |
| WallPuty | - | 4 | 4 | | - |
| 4mm wire | - | 6 | 6 | 1,300,000 | 7,800,000 |
| Connector Bar | - | 30 | 30 | 24,000 | 720,000 |
| Marine Board | - | 550 | 550 | 100,000 | 55,000,000 |
| Props | - | 1,000 | 1,000 | 15,000 | 15,000,000 |
| Vishoka | - | 20 | 20 | 35,000 | 700,000 |
| Nyundo | - | 10 | 10 | 18,000 | 180,000 |
| Kopla | - | 2 | 2 | 86,000 | 172,000 |
| Reflactor | - | 60 | 60 | 15,000 | 900,000 |
| Disc | - | 2 | 2 | 15,000 | 30,000 |
| Cut Out | - | 3 | 3 | 42,000 | 126,000 |
| Single switch Socket | - | 10 | 10 | 10,000 | 100,000 |
| Nondo 10mm | - | 30 | 30 | 40,000 | 1,200,000 |
| 2*6 | - | 4,400 | 4,400 | 40,000 | 176,000,000 |
| Union Box | - | 4 | 4 | 36,000 | 144,000 |
| Nipple Socket | - | 27 | 27 | 25,000 | 675,000 |
| **Jumla** | | | | | **258,747,000** |

*Chanzo: Uchambuzi wa Nyaraka za Makisio ya Gharama za Ujenzi (BOQ)*

### 7.1.2.4 Dosari zilizobainika katika ujenzi wa Majengo ya Ofisi na Mahanga ya Askari

Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar linatekeleza miradi mbali mbali ya ujenzi ikiwemo ujenzi wa majengo ya Ofisi pamoja na ujenzi wa Mahanga ya Askari Unguja na Pemba. Katika utekelezaji wa miradi hiyo ukaguzi ulitembelea maeneo mbali mbali ya utekelezaji na kubaini uwepo wa dosari zifuatazo:-

#### (a) Kutozingatiwa kwa Huduma za uzimaji wa moto na Usalama katika Majengo yanayojengwa na Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar (JKUZ)

Ukaguzi ulitembelea maeneo ya Ujenzi wa Mahanga na Ofisi za Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar na kujionea ujenzi unaoendelea kufanyika ambapo ukaguzi umebaini ya kwamba JKUZ haikuzingatia huduma za uzimaji wa moto na usalama kwa watumiaji wa majengo hayo. Majengo hayo ni kama yafuatayo:

i. Jengo moja la Ofisi na Mahanga mawili ya Wanafunzi Bambi Kim Unguja.

ii. Jengo la Ofisi ya Zoni ya JKU Wawi Pemba.

iii. Jengo moja la Ofisi na Mahanga mawili ya Wanafunzi Chambani Pemba.

#### (b) Kuanza kuharibika kwa dari za majengo

Mnamo tarehe 28 Novemba, 2023 Ukaguzi ulitembelea miradi ya Ujenzi wa Mahanga ya Wanafunzi pamoja na Afisi ya Kambi ya JKUZ Bambi na kubaini kuwepo kwa dosari katika dari za majengo ambazo zimeshaanza kuharibika kabla ya majengo kutumika.

Kitendo cha kuanza kuharibika kwa dari kabla ya mradi kukamilika na kukabidhiwa kinatoa ishara ya utekelezaji wa mradi uliofanywa chini ya kiwango kubalifu jambo ambalo huwenda likapelekea kuchakaa kwa majengo kwa haraka, kuendelea kuvuja na kuharibika kwa vifaa na samani, kutapelekea kutumika kwa gharama ya ziada ya kufanya ukarabati kwa muda mfupi jambo ambalo ni kuisababishia hasara Serikali ya kufanya matumizi nje ya bajeti.

#### (c) Uwekaji usioridhisha wa viluva (Interlock Paving Block)

Katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Mahanga ya Askari pamoja na majengo ya Ofisi ya Kambi ya JKU Bambi Kim, ukaguzi ulijionea utekelezaji wa mradi huo ukiwa upo katika uwekaji wa Viluva (Interlock Paving Block) katika eneo la nje ya majengo hayo.

Dosari iliyobainika ni utekelezaji usioridhisha wa upangaji wa Viluva ambavyo baadhi yake kuonekana kufanya shimo na vyengine kutokupangika vizuri na kupelekea kujitokeza kwa tatizo la kutuwama kwa maji, kufanyika kwa mabonde na miinuko na vyengine kubainika vikiwa vimeota majani na kutokuonesha taswira nzuri ya utekelezaji wa mradi huo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar kuongeza umakini wa usimamizi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo kufanya usimamizi wa kila hatua ili kuepusha kujitokeza kwa kitendo cha kufanya ukarabati kabla ya kukabidhiwa kwa miradi ya Serikali.

### 7.1.2.5 Malipo ambayo hayakufuata Taratibu za Manunuzi shilingi 144,966,683

Kwa mujibu wa kanuni nambari 57(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2020, inaeleza kwamba Taasisi ya Ununuzi haitoruhusiwa kuvunjavunja manunuzi (split contract) kwa lengo la kukwepa uitishaji wa zabuni.

Ukaguzi umebaini kwamba Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar limefanya manunuzi ya shilingi 144,966,683 kwa utaratibu wa kuvunjavunja kwa mtoa huduma Green Land General Supply Company kinyume na kanuni iliyonakiliwa hapo juu.

Kufanya ununuzi kwa njia ya kuvunjavunja kunapelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na malipo ya wazabuni wanaoingia mikataba ya kazi au usambazaji wa bidhaa au huduma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar kuweka msisitizo katika usimamizi wa ununuzi unaofanyika kwa lengo la kuzingatia matakwa ya Sheria ya Ununuzi ili kuepuka athari inayoweza kujitokeza kutokana na kushindwa kusimamia matakwa ya Sheria hiyo. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 55:Malipo ambayo hayakufuata taratibu za manunuzi**

| Tarehe ya Malipo | Aliyelipwa | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|
| 20/07/2022 | Green Land General Supply Company | 2,847,762 |
| 22/07/2022 | | 40,497,056 |
| 30/07/2022 | | 46,715,732.08 |
| 19/07/2022 | | 13,436,088 |
| 05/10/2022 | | 4,660,764.72 |
| 12/10/2022 | | 9,164,201.04 |
| 19/01/2023 | | 251,725.50 |
| 06/02/2023 | | 735,000 |
| 10/02/2023 | | 24,019,607.86 |
| 09/03/2023 | | 2,638,746.14 |
| **Jumla Kuu** | | **144,966,683.34** |

## JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU) PEMBA

### 7.1.2.6 Uwepo wa mashine ambazo hazitumiki zenye thamani ya shilingi 44,918,400

Kifungu nambari 61(2) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinawataka Maafisa Masuuli kuhakikisha kwamba mali za umma zinatumika kwa tija na manufaa kulingana na jukumu litakalotekelezwa.

Ukaguzi umebaini kwamba Jeshi la Kujenga Uchumi Zoni ya Pemba limefanya malipo ya shilingi 44,918,400 kwa ajili ya ununuzi wa mashine ya kufyatulia matofali iliyogharimu shilingi 25,500,000 pamoja na mashine ya kufanyia mikate ya bekari kwa shilingi 19,418,400 kwa ajili ya kujiongezea mapato na mashine hizo kupelekwa katika kambi ya Msaani kwa ajili ya kuanza kazi. Hadi ukaguzi unakamilika mashine hizo bado hazijafanyiwa kazi kama ilivyokusudiwa jambo ambalo limepelekea kutokupatikana kwa tija iliyokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi Pemba (JKU) kuhakikisha unatenga fedha za kutosha katika bajeti ili kuiendeleza miradi inayoibuliwa na kuweza kuleta tija iliyokusudiwa.

### 7.1.2.7 Nyaraka za gari za JKU kuonyesha umiliki wa watu binafsi

Kwa mujibu wa kifungu nambari 64(1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba "Taasisi ya Umma itahifadhi nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali".

Ukaguzi umebaini kuwa Jeshi la Kujenga Uchumi Pemba (JKU) linamiliki gari aina mbali mbali lakini baadhi ya gari hizo nyaraka zake zinaonesha kuwa na umiliki wa watu binafsi katika nambari za usajili badala ya Jeshi hilo. Nyaraka za gari kuonyesha zinamilikiwa na watu binafsi kunaweza kusababisha mgogoro baina ya Jeshi na wananchi na pia kunaweza kupelekea matumizi mabaya ya gari hizo. Hali hii inaweza kuwa imetokana na ununuzi wa gari zishazotumika au kutokubadilisha umiliki baada ya kununua.

Nyaraka za gari kuonyesha umiliki wa watu binafsi ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokitaja hapo juu. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi Zoni ya Pemba kuhakikisha kwamba gari zake zote wanazipatia nyaraka zinazoonyesha kumilikiwa na Jeshi ikiwa ni pamoja na kushirikiana na Wakala wa Usajili wa Mali na Biashara kwa lengo la kufuatilia utaratibu mzima wa upatikanaji wa nyaraka hizo.

Mchanganuo wa gari ambazo nyaraka zake zinaonyesha kumilikiwa na watu binafsi ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 56: Gari za JKU zinazoonyesha kumilikiwa na watu binafsi**

| Namba | Aina ya Gari | Jina la Umiliki | Namba ya Usajili | Namba Inayotumika |
|---|---|---|---|---|
| 1. | RRADO S/WAGON | Rashid Moh'd Soud | Z 912 FY | JKU 140 |
| 2. | SUZUKI ESCUDO | Kombo Ali Hamdu | Z164 JA | JKU 143 |
| 3. | MAZDA | Ali Azizi Ali | Z387 GJ | JKU 141 |
| 4. | COASTER BUS | Mariam Shabani Chavala | Z 593 KA | JKU 150 |
| 5. | CARRY SUZUKI | Taarifa za umiliki zimekosekana | Z971 JG | Nambari haikupatikana |

*Chanzo: Nyaraka za Umiliki wa Vyombo*

### 7.1.2.8 Kufanya Matumizi ya Fedha za Makusanyo ya Mapato Kinyume na Utaratibu shilingi 190,151,180

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Jeshi la Kujenga Uchumi Zoni ya Pemba kwa mwaka wa fedha 2022/2023 limekusanya jumla ya shilingi 190,151,180 kutokana na vyanzo vyake mbali mbali vya mapato.

Dosari iliyobainika ni kutokuwepo kwa makadirio ya mapato pamoja na kutokuingizwa kwa mapato hayo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali jambo ambalo limepelekea Jeshi hilo kufanya matumizi ya mapato hayo bila ya kuwa na kibali kutoka Baraza la Mapinduzi.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa matumizi yasiyoridhisha ya fedha za Serikali, aidha ni kwenda kinyume na kanuni nambari 39(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Zoni ya Jeshi la Kujenga Uchumi Pemba kufuata taratibu, miongozo na sheria zilizowekwa ili kupata uhalali wa kutumia fedha wanazokusanya. Mchanganuo wa makusanyo na matumizi hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 57: Makusanyo ya mapato yaliyotumika kinyume na taratibu**

| Namba | Muda wa Makusanyo | Kiasi cha Fedha Kilichokusanywa na Kutumika (Tshs) |
|---|---|---:|
| 1. | Julai, 2022 | 700,000 |
| 2. | Ogasti, 2022 | 12,482,692 |
| 3. | Septemba, 2022 | 19,560,586 |
| 4. | Oktoba, 2022 | 15,645,362 |
| 5. | Novemba, 2022 | 20,405,950 |
| 6. | Disemba, 2022 | 5,200,000 |
| 7. | Januari, 2023 | 11,247,084 |
| 8. | Februari, 2023 | 52,286,932 |
| 9. | Machi, 2023 | 13,571,792 |
| 10. | Aprili, 2023 | 22,991,952 |
| 11. | Mei, 2023 | 5,467,938 |
| 12. | Juni, 2023 | 10,590,892 |
| **Jumla** | | **190,151,180** |

*Chanzo: Daftari la Kukusanyia Mapato*

### 7.1.3 FUNGU D 03 - CHUO CHA MAFUNZO

Ukaguzi wa hesabu za Chuo cha Mafunzo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 7.1.3.1 Utambuzi wa mapato kinyume na Muongozo

Kwa mujibu wa maelezo ya taarifa za fedha za hesabu za mwisho wa mwaka Chuo cha Mafunzo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 zimefungwa kwa kuzingatia msingi na muongozo wa uandaaji wa hesabu za kimataifa "IPSAS cash basis". Aidha, miongoni mwa baadhi ya Msingi hiyo ni "IPSAS 1" ambayo inatoa muongozo wa ufungaji wa hesabu kwa njia ya "Cash basis" ambayo inaitaka taasisi husika kuripoti taarifa zake za mapato ya mwaka husika.

Muongozo wa Uandaaji wa hesabu (IPSAS Cash Basis) unaelekeza kuwa kumbukumbu za mapato na matumizi yataingizwa kwenye vitabu vya mahesabu wakati malipo halisi yanapopokelewa au kutolewa, ukaguzi umebaini kuwa Chuo cha Mafunzo kinatambua mapato yao baada ya kutoa matumizi (Profit) jambo ambalo ni kwenda kinyume na Muongozo wa ufungaji wa hesabu (IPSAS Cash Basis).

Kufanya hivyo kunapelekea Chuo cha Mafunzo kushindwa kutoa hesabu sahihi ya mapato waliokusanya kwenye vyanzo vyao vya mapato.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuhakikisha kwamba unaandaa hesabu zake kwa mujibu wa viwango vya hesabu vinavyoelekeza.

#### 7.1.3.2 Utumiaji usioridhisha wa rasilimali za Chuo cha Mafunzo

Ukaguzi umepitia taarifa mbali mbali za Chuo zikiwemo taarifa za kibajeti kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Chuo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo mapato yote ya Chuo yalikadiriwa kuwa ni shilingi 125,690,855.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 Chuo kilikusanya jumla ya shilingi 102,251,500 sawa na asilimia 81 ya makadirio kutoka katika vyanzo vyake, vile vile kwa kupitia mpango kazi umeeleza kuwa Chuo kitaweka miundombinu ya umwagiliaji katika makambi na kupatia idara ya uzalishaji Pembejeo za kilimo na ufugaji na utumiaji mzuri wa ardhi kwa ajili ya kilimo.

Ukaguzi ulitembelea kambi za Chuo cha Mafunzo zilizopo Ubago, Hanyegwa Mchana, Langoni, Kinumoshi, kiwanda cha Ushoni pamoja na Idara mbali mbali

za uzalishaji na kubaini kwamba licha ya kuwa na mipango mizuri Chuo cha Mafunzo bado kumekuwa na ufanisi wa chini wa ukusanyaji wa mapato jambo ambalo linatia shaka kwa ukaguzi kujihakikishia kuwa Chuo cha Mafunzo kinaweza kutekeleza dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba vikosi vya Ulinzi na Usalama vinajitegemea kutokana na shughuli zake za uzalishaji.

Kushindwa kutumia rasilimali zake vizuri inaweza kupelekea kwa Chuo cha Mafunzo kushindwa kutumia vyema rasilimali ya ardhi na watu katika uzalisahaji na hatimae kukosekana kwa mapato.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kufanyia kazi mapendekezo ya ukaguzi ili kwenda sambamba na dhamira ya Serikali ya awamu ya nane ya kuhakikisha kwamba vikosi vya Ulinzi na Usalama vinajitegemea kutokana na shughuli zake za uzalishaji.

#### 7.1.3.3 Dosari zilizobainika katika zabuni nambari SMS/DO4/G/RNCB/2022 /2023/02 ya Ununuzi wa Chakula cha Askari na Wanafunzi

Kanuni ya 125(1)(2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2021 inaeleza kuwa kutakuwa na makadirio ya thamani ambayo ni misingi ya kazi za ununuzi; na zabuni yoyote iliyotathiminiwa na iko juu au chini ya makadirio ya thamani ya manunuzi, kadiri itakavyokuwa, haitaidhinishwa isipokuwa ikiwa inakidhi masharti kama ilivyoainishwa katika miongozo iliyotolewa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji Zanzibar.

Aidha, kifungu cha 43(2) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza "Ununuzi au uondoshaji wa mali za umma utaanzishwa au kuendelea baada ya kuthibitishwa kwamba fedha zote kwa kiwango kamili na kwa muda wote zitakuwepo wakati wa kuingia mkataba".

Chuo cha Mafunzo kilitangaza zabuni ya ununuzi wa Chakula cha Askari na Wanafunzi kwa njia ya ushindani usio wa wazi ikiwa na makadirio ya shilingi 1,440,000,000. Nyaraka za wazabuni watatu zilifunguliwa tarehe 13 Septemba, 2022 na kufanyiwa tathmini. Tarehe 23 Novemba, 2022 Chuo cha Mafunzo kilisaini mkataba na Mkangas General Supplies wa pendekezo la ununuzi na usambazaji wa Chakula cha Askari na Wanafunzi kwa jumla ya shilingi 2,625,439,045 kuwa ndie mzabuni aliyekuwa na kiwango cha chini. Hii imepelekea kuwepo kwa ongezeko la shilingi 1,185,439,045 sawa na asilimia 82.32 ukilinganisha na makadirio ya awali. Kwa mujibu wa taratibu za manunuzi Zabuni hiyo haikupaswa kuidhinishwa na ilitakiwa kutangazwa upya ili kupata bei shindani.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuhakikisha kwamba, unafanya tathmini ya kina pale wanapoamua kufanya makadirio ya hesabu kwa mahitajio ya ununuzi mbali mbali ili kupata hesabu sahihi.

#### 7.1.3.4 Dosari zilizobainika katika zabuni nambari SMS/DO3/G/RNCB/ 2022/2023/03 ya Ununuzi wa Mafuta

Kanuni ya 125(1)(2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya 2021 inaeleza kuwa kutakuwa na makadirio ya thamani ambayo ni misingi ya kazi za ununuzi, na zabuni yoyote iliyotathiminiwa na iko juu au chini ya makadirio ya thamani ya manunuzi, kadiri itakavyokuwa, haitaidhinishwa isipokuwa ikiwa inakidhi masharti kama ilivyoainishwa katika miongozo iliyotolewa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji Zanzibar.

Aidha, kifungu cha 43(2) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa "Ununuzi au uondoshaji wa mali za umma utaanzishwa au kuendelea baada ya kuthibitishwa kwamba fedha zote kwa kiwango kamili na kwa muda wote zitakuwepo wakati wa kuingia mkataba".

Chuo cha Mafunzo kilipanga kupitia mpango wake wa manunuzi kuwepo kwa zabuni nambari SMS/DO3/G/RNCB/2022/2023/03 ya ununuzi wa mafuta yenye jumla ya shilingi 55,281,473.

Aidha, ukaguzi umepitia taarifa za malipo yaliyofanywa kwa ajili ya ununuzi wa Mafuta na kubaini kuwepo jumla ya shilingi 121,318,500 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Petrol na jumla ya shilingi 55,281,473 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Diesel kutoka Kijangwani Petrol Station kwa Unguja na Chasasa Service Station Pemba.

Kufanyika kwa matumizi hayo kumepelekea kuwepo kwa ongezeko la jumla ya shillingi 121,318,500 ambapo ni sawa na asilimia 219.46 ukilinganisha na makadirio ya awali. Kwa mujibu wa taratibu za manunuzi Zabuni hiyo haikupaswa kuidhinishwa na ilitakiwa kutangazwa upya ili kupata bei shindani.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuhakikisha kwamba, unafanya tathmini ya kina pale wanapoamua kufanya makadirio ya hesabu kwa mahitajio ya ununuzi mbali mbali ili kupata hesabu sahihi.

### 7.1.3.5 Mazingira yasiyoridhisha ya Makaazi ya Askari wa Chuo cha Mafunzo

Mnamo tarehe 06 Disemba, 2023 ukaguzi ulifanya ziara ya kutembelea Kambi za Vyuo vya Mafunzo Zoni ya shamba kwa upande wa Unguja kwa lengo la kuangalia utekelezaji wa mipango na kazi za Chuo cha Mafunzo kilichojipangia kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Aidha, ukaguzi ulibaini kuwepo kwa Mazingira yasiyoridhisha ya Makaazi ya Askari wa Chuo cha Mafunzo katika maeneo ya Makambi ya Chuo cha Mafunzo yaliyokuwepo katika maeneo mbali mbali kwa upande wa Unguja. Kambi hizo ni kama zifuatazo:-

- Kambi ya Chuo cha Mafunzo Hanyengwa Mchana.
- Kambi ya Chuo cha Mafunzo Ubago.
- Kambi ya Chuo cha Mafunzo Kinu Moshi.
- Kambi ya Chuo cha Mafunzo Langoni.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuhakikisha kwamba, unafanya juhudi za maksudi ili kuinusuru hali hiyo inayozikabili nyumba za Maaskari hao kwa ajili ya maakazi yao.

## 7.1.4 FUNGU D 06 - KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Kikosi cha Valantia Zanzibar (KVZ) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

### 7.1.4.1 Kutokuwepo kwa mpango maalum wa mafunzo

Kanuni nambari 74(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014 inazitaka "Taasisi zote za Serikali kuandaa mpango maalum wa mafunzo pamoja na kutenga fedha kwa ajili ya mafunzo hayo". Aidha kwa mujibu wa waraka wenye kumbukumbu namba CAB.40/158/01/54 na CAB.40/158/01/37 kutoka Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora unazitaka Wizara na Taasisi za umma kufanya maandalizi ya mpango wa mafunzo ili kujua mahitaji (Training Needs Assessment) na kuwasilisha mpango wa mafunzo.

Ukaguzi umebaini kwamba Kikosi cha Valantia Zanzibar hakikuandaa Mpango mkuu wa mafunzo ambao ungesimamia masuala yote yanayohusiana na mafunzo kwa watendaji wake na kuuwasilisha kwa mujibu wa kanuni na toleo lililonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi cha Valantia Zanzibar kuhakikisha unaandaa mpango wa mafunzo, mpango wa tathmini ya mahitaji pamoja na bajeti ya mafunzo ili kuepusha kujitokeza kwa mizozo au malalamiko kwa watumishi wa umma watakaonyimwa nafasi ya kushiriki katika mafunzo.

### 7.1.4.2 Malipo yaliyofanyika kinyume na Masharti ya Mkataba shilingi 841,290,169.62

Kifungu nambari 18.6 cha Masharti Maalum ya Mkataba wa ununuzi wa Chakula baina ya Kikosi cha Valantia Zanzibar na Mtoa huduma M/s Magomeni Jitini kinaeleza ya kwamba "Asilimia 90 ya Malipo ya Mkataba yatalipwa wakati wa upokeaji wa bidhaa na wakati wa uwasilishaji nyaraka kama zilivyoainishwa katika kifungu 10 Masharti ya Jumla ya Mkataba. Aidha, Asilimia 10 ya Gharama za Mkataba zitalipwa kwa msambazaji ndani ya siku thelathini (30) baada ya tarehe ya kutolewa cheti cha kukubalika kwa bidhaa kutoka katika Taasisi ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Ukaguzi umepitia hati za malipo na kubaini kuwepo kwa malipo ya jumla ya shillingi 841,290,169.62 ambayo yamelipwa kwa msambazaji M/s Magomeni Jitini kwa asilimia mia moja (100%) kinyume na masharti maalum ya Mkataba.

Kufanya malipo bila ya kuzingatia masharti ya mkataba kunaweza kukapelekea kujitokeza kwa migongano pindipo upande mmoja wa mkataba utakaposhindwa kutelekeza masharti waliyokubaliana.

Aidha, kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa matumizi ambayo hayakutakiwa kufanyika kutokana na kutokufatwa kwa masharti ya Mkataba kama walivyokubaliana.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi cha Valentia Zanzibar kuhakikisha wanafanya malipo kwa mujibu wa makubalino ya Mkataba kama pande zote mbili zilivyokubaliana na si vyenginvyo.

### 7.1.4.3 Kutokufanyika kwa uchunguzi kwa bidhaa ambazo zinapokelewa

Kifungu nambari 10.1 cha Mkataba wa ununuzi wa Chakula baina ya Kikosi cha Valantia Zanzibar na Mtoa huduma M/S Magomeni Jitini kinaeleza ya kwamba "Uchunguzi na upimaji wa bidhaa utafanyika kwa asilimia 50 ya mbinu za kiuchunguzi."

Ukaguzi umepitia taarifa za kumbukumbu ya mapokezi ya bidhaa za chakula kwa ajili ya matumizi ya Askari na kubaini kutokuwepo kwa ripoti za uchunguzi wa bidhaa zilizopokelewa kwa ajili ya matumizi ya Askari.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kupokelewa kwa bidhaa ambazo zimeshapitwa na muda au kuharibika, vile vile kunaweza kusababisha kupokelewa kwa bidhaa zilizo tofauti kwa mujibu wa makubalino ya mkataba kulinganisha na idadi, kiwango na ubora.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi cha Valantia Zanzibar kuhakikisha unafuata Masharti ya Mkataba kama walivyokubaliana.

## KIKOSI CHA VALANTIA (KVZ) PEMBA

### 7.1.4.4 Kufanya matumizi ya makusanyo ya mapato kinyume na utaratibu shilingi 74,153,383

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi cha Valantia Zoni ya Pemba kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kimekusanya jumla ya shilingi 74,153,383 kutokana na vyanzo vyake mbali mbali vya mapato.

Dosari iliyobainika ni kutokuwepo kwa makadirio ya mapato pamoja na kutokuingizwa kwa mapato hayo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali jambo ambalo limepelekea Kikosi hicho kufanya matumizi ya mapato hayo bila ya kuwa na kibali kutoka Baraza la Mapinduzi.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa matumizi yasiyoridhisha ya fedha za Serikali, aidha ni kwenda kinyume na kanuni nambari 39(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za mwaka 2021. Mchanganuo wa makusanyo na matumizi hayo ni kama yafuatavyo:-

**Jadweli Nambari 58:Makusanyo ya mapato yaliyotumiwa kinyume na utaratibu**

| Namba | Muda wa Makusanyo | Kiasi cha Fedha Kilichokusanywa na Kutumika (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Julai, 2022. | 5,900,000 |
| 2. | Ogasti, 2022. | 5,500,000 |
| 3. | Septemba, 2022. | 7,578,805 |
| 4. | Oktoba, 2022. | 2,231,373 |
| 5. | Novemba, 2022. | 20,405,950 |
| 6. | Januari, 2023. | 11,700,000 |
| 7. | Februari, 2023. | 7,237,255 |
| 8. | Machi, 2023. | 6,700,000 |
| 9. | Mei, 2023. | 4,700,000 |
| 10. | Juni, 2023. | 2,200,000 |
| **Jumla** | | **74,153,383** |

## 7.1.5 FUNGU D 05 - KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI

Ukaguzi wa hesabu za Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar (KZU) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

### Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi

### 7.1.5.1 Ukiukwaji wa taratibu za malipo ya Posho mbali mbali

Kwa mujibu wa kifungu nambari 60(a-i) cha Kanuni ya Tume ya Utumushi ya Idara maalum ya 2002 kimeeleza kuwa: Maafisa na askari wa Idara Maalum watapaswa kulipwa maposho mbalimbali kama yatakavyokuwa yakipangwa na Tume kipindi baada ya kipindi kwa mujibu wa ujuzi, vyeo na mazingira mengineyo kama yalivyofafanuliwa katika kifungu nambari 60(a-i) cha Kanuni ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum ya 2007.

Ukaguzi umefanya mapitio katika hati za malipo, mfumo wa malipo (payroll), maandalizi na utekelezaji wa bajeti pamoja na kanuni, miongozo na sheria mbali mbali zinazohusiana na ulipwaji wa stahiki kwa watumishi wa Idara Maalum.

Ukaguzi umebaini Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimefanya malipo ya maposho kwa Maafisa na Askari wake mbali mbali ambapo malipo hayo hulipwa kinyume na utaratibu uliowekwa na Tume ya Utumishi ya Idara Maalum. Katika dosari

hiyo ilibainika uwepo wa baadhi ya wapiganaji kulipwa malipo pungufu ya posho la mazingira magumu la asilimia 15 na posho la nyumba la asilimia 10 ambapo thamani ya fedha inayolipwa hailingani na asilimia ya fedha iliyotakiwa kulipwa kwa mujibu wa miongozo na kanuni za Tume ya Utumishi ya Idara Maalum ya 2007.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kufanya mapitio mapya ya stahiki za wapiganaji wake ili kuweza kufanya maboresho ya bajeti ya stahiki za maafisa na wapiganaji kuendana na uhalisia wa fedha wanayotakiwa kulipwa. Mchanganuo wa posho zinazolipwa kwa baadhi ya wapiganaji hao ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 59:Ukiukwaji wa taratibu za malipo ya Posho mbali mbali**

| Namba ya Uajiri | Posho linalostahiki kulipwa kulingana na mshahara kwa mwezi (Tsh.) (A) | Posho linalolipwa (Tsh.) (B) | Tofauti ya Posho (Tsh.) (A-B) |
|---|---|---|---|
| **POSHO LA MAZINGIRA MAGUMU (15% YA MSHAHARA)** | | | |
| 938730 | 162,150 | 75,000 | 87,150 |
| 738689 | 175,500 | 75,000 | 100,500 |
| 738801 | 162,150 | 75,000 | 87,150 |
| 139103 | 139,700 | 75,000 | 64,700 |
| 138707 | 212,550 | 75,000 | 137,550 |
| **Jumla Ndogo (X)** | **852,050** | **375,000** | **477,050** |
| **Namba ya Uajiri** | **Posho linalostahiki kulipwa kulingana na mshahara kwa mwezi (Tsh.) (C)** | **Posho linalolipwa (Tsh.) (D)** | **Tofauti ya Posho (Tsh.) (C-D)** |
| **POSHO LA NYUMBA (10 % YA MSHAHARA)** | | | |
| 938730 | 108,100 | 10,000 | 98,100 |
| 738689 | 175,500 | 20,000 | 155,500 |
| 738801 | 108,100 | 10,000 | 98,100 |
| 139103 | 139,700 | 20,000 | 119,700 |
| 138707 | 141,700 | 20,000 | 121,700 |
| **Jumla Ndogo (Y)** | **673,100** | **80,000** | **593,100** |
| **Jumla Kuu (X+Y)** | **1,525,150** | **455,000** | **1,070,150** |

*Chanzo: Nyaraka za Mishahara kwa mwaka wa fedha 2022/2023*

#### 7.1.5.2 Kutokuandaliwa kwa Sera za Kikosi cha Zimamoto na Uokozi

Kifungu nambari 6 (1-2) cha Sheria namba 9 ya mwaka 1999 ya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimezitaja kazi za Kamishna wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi ikiwa ni pamoja na Uandaaji wa Sera za Kikosi zinazohusiana na masuala ya Viwango, Mafunzo, Uongozi na mambo mengine yanayohusiana na utendaji wa shughuli za kikosi cha Zimamoto na Uokozi.

Timu ya ukaguzi ilifanya mahojiano na Maofisa na Askari wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi juu ya uwaandaji wa sera hizo na matumizi yake na kubaini Kikosi hakikuandaa Sera ambazo zingetumika katika ufanyaji wa kazi za kikosi za kila siku kinyume na matakwa ya sheria tajwa hapo juu, hali ambayo imepelekea kutokufanyika kwa baadhi ya shughuli za Kikosi kwa ufanisi na uweledi.

Kazi za Kikosi cha Zimamoto na Uokozi zinategemea kuwepo kwa sheria, kanuni, miongozo na sera mbali mbali ambazo zitakwenda kurahisisha shughuli za ufanyaji wa kazi za Kikosi hivyo basi kutokuwepo kwa baadhi ya sera na miongozo kunaweza kupelekea baadhi ya kazi za Kikosi kutokufanyika kwa ufanisi na uweledi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kuchukua jitihada za haraka za ufanikishaji wa uandaaji wa sera na miongozo ya Kikosi ili kuweza kufanya kazi katika viwango vinavyohitaji.

#### 7.1.5.3 Kukosekana kwa uhalisia wa Makadirio ya matumizi na utekelezaji wake shilingi 2,197,000,298

Katika kupitia nyaraka mbalimbali, ikiwemo ripoti ya utekelezaji wa mpango kazi wa Kikosi kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2023 na kubaini kuwepo fedha zilizoingizwa kwa shughuli makhususi ambazo zimepindukia fedha za makadirio ambazo zilipangwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali ziliomo kwenye mpango kazi wao.

Aidha, ukaguzi umebaini kuwepo kwa ongezeko la shilingi 2,197,000,298 ambalo limetokana na kuingizwa kwa fedha kinyume na zilizoombwa kwenye shughuli makhususi zilizoainishwa katika Kikosi hicho. Hata hivyo ukaguzi umeshindwa kupata maelezo ya kina kuhusiana na kuwepo kwa ongezeko hilo.

Kutokana na tofauti ya kima kikubwa cha fedha kilichobainika ukaguzi umefanya tathmini ya kina baada ya kuwasilisha hoja hii kwa uongozi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi na kutokupatiwa majibu toshelevu, hivyo dosari hii huwenda ilisababishwa na kukosekana kwa umakini wa utekelezaji wa miongozo ya bajeti pamoja na uhalisia wa kinachofanyika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kuongeza umakini katika upangaji wa Mpango Kazi ili uweze kuendana na uhalisia wa taarifa za utekelezaji wake. Jadweli lifuatalo linaonyesha ongezeko la fedha hizo:

### Jadweli Nambari 60:Tofauti iliyobainika baina ya fedha halisi na makisio

| Idara husika | Huduma/shughuli | Kupitia mpango kazi | Kupitia ripoti ya utekelezaji | Tofauti |
|---|---|---|---|---|
| Utawala na Fedha | S.1.1<br>Kutoa huduma za uokozi na uzimajimoto kwa wakati | 388,400,000 | 523,690,947 | 135,290,947 |
| | S.1.2<br>Kuwajengea uwelewa wananchi na Taasisi kuhusu tahadhari ya majanga ya moto | 10,000,000 | 243,576,002 | 233,576,002 |
| | S.1.5<br>Kuwapatia maafisa na wapiganaji mafunzo ya uzimaji moto na uokozi ndani na nje ya nchi | 20,000,000 | 133,942,004 | 113,942,004 |
| | S.2.3<br>Kuziwezesha timu kushiriki katika michezo | 70,000,000 | 208,418,953 | 138,418,953 |
| | S.2.4<br>Kuwapatia maafisa na wapiganaji posho na likizo | 20,000,000 | 50,000,000 | 30,000,000 |
| | S2.2.1<br>Ujenzi wa vituo vya uokozi na uzimaji moto, nyumba na mahanga ya kulala Maafisa na Askari. | 1,230,000,000 | 2,792,772,392 | 1,562,772,392 |
| **Jumla** | | **1,755,400,000** | **3,952,400,298** | **2,197,000,298** |

*Chanzo: Nyaraka za Bajeti na utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2022/2023*

### 7.1.5.4 Dosari katika utekelezaji wa Mkataba wa ununuzi wa Vifaa vya Ujenzi shilingi 3,480,000,000

Kanuni ya 20(1-2) (f) na 58(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2020 inaeleza Kipindi cha mkataba kinachoruhusiwa kitatoa tathmini ya kweli ya wakati ambapo mzabuni anayefaa anaweza kutarajiwa kukamilisha uwasilishaji wa bidhaa, kukamilisha kazi, au kukamilisha kutoa huduma, kwa kuzingatia tarehe inayotarajiwa ya kukamilika na eneo husika.

Ukaguzi ulipitia Mkataba wa ununuzi wa vifaa vya ujenzi uliongiwa baina ya KZU na M/S Osaju Company ltd wenye kumbukumbu nambari SMZ/DO5/G/NCB/2021-2022/11 wa tarehe 31/12/2021 kwa thamani ya shilingi 3,480,000,000 pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na kubaini kwamba mkataba huo haukuainisha muda wa kukamilisha ununuzi wa vifaa hivyo.

Aidha, katika kupitia hati za malipo ukaguzi ulibaini kuwepo kwa muda mrefu wa uwasilishwaji wa Vifaa vya Ujenzi kwa ajili ya Unguja na Pemba ambapo Mkataba umeendelea kutumika kwa muda wa miaka miwili (2) kutokana na kutokuanishwa kwa muda wa umalizikaji wa Mkataba.

Kuwepo kwa muda mrefu wa uwasilishwaji wa vifaa vya ujenzi kwa ajili ya Unguja na Pemba kunaweza kupelekea kutofikiwa lengo la Serikali kutokana na kutokukamilika kwa wakati shughuli zilizopangwa kufanyika kwa wakati husika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kuwa makini wakati wa uandaaji na utekelezaji wa mikataba ili kuona shughuli zote zilizopangwa zinakamilika kwa wakati husika kwa mujibu wa Mipango ya Serikali. Aidha, ni vyema Kikosi kuunda timu ya ufuatiliaji wakati wa mchakato wa manunuzi na wakati wa uandaaji na utekelezaji wa Mkataba.

### 7.1.5.5 Dosari katika usimamizi wa Miradi ya Maendeleo ya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi

Ukaguzi ulipitia Mkataba wa ununuzi na usambazaji wa vifaa vya Ujenzi uliongiwa baina ya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi na M/S Osaju Company Ltd wenye kumbukumbu nambari SMZ/DO5/G/NCB/2021-2022/11 wa tarehe 31/12/2021 kwa thamani ya shilingi 3,480,000,000 pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Baada ya kufanyika kwa hatua hiyo Ujenzi ulianza rasmi katika maeneo yaliyoainishwa ndani ya Mkataba kama ifuatavyo:-

- Ujenzi wa Hanga la Askari Mahonda.
- Ujenzi wa Ofisi za Kanda Kaskazini Unguja Mahonda.

- Ujenzi wa Hanga na Nyumba za Askari Finya.
- Ujenzi wa Kituo cha Zimamoto na Uokozi Wete.

Ukaguzi ulitembelea Miradi hiyo katika maeneo yaliyoainishwa kwa kuangalia hatua za utekelezaji pamoja na hali ya usimamizi wa miradi na kubaini kuwepo kwa dosari zifuatavyo:-

### a) Kuta za majengo hazikujengwa kwa viwango vinavyohitajika

Ukaguzi ulitembelea Mradi wa Hanga na Nyumba za Askari Finya Pemba na kubaini uwepo wa kuta zilizojengwa kwa viwango visivyoridhisha hali inayoweza kupelekea Majengo kutokuwa na ubora kwa matumizi ya baadae.

### b) Kutumika kwa matofali yasiyokuwa na viwango vinavyohitajika

Ukaguzi ulitembelea Mradi wa Hanga na Nyumba za Askari Finya Pemba na kubaini kuwepo kwa matofali ambayo hayakuwa na viwango kwa ajili ya matumizi ya ujenzi huo. Matofali hayo yaliyopokelewa na Kikosi kutoka kwa Mzabuni aliyepewa kazi hiyo. Aidha ukaguzi ulifanya mahojiano na baadhi ya mafundi na kututhibitishia kuhusu kuyakataa Matofali hayo kutokana na kutokukidhi viwango vinavyohitajika katika aina ya ujenzi iliyopo pamoja na baadhi ya tofali hizo kuwa na dosari mbali mbali.

### c) Uwezekaji usioridhisha wa paa la majengo ya Mahanga ya Askari

Ukaguzi ulibaini hali ya kuharibika kwa dari za majengo (Roof) kwa Jengo la Kituo cha Zimamoto na Uokozi Wete na Hanga la Askari Mahonda, hali iliyosababishwa na uwezekaji usioridhisha wa mapaa ya majengo hayo, hali iliyopelekea kuanza kuvuja wakati wa mvua.

### d) Utunzaji wa vifaa vya ujenzi usioridhisha vikiwa ghalani

Ukaguzi ulitembelea bohari za Vifaa vya ujenzi katika maeneo ya ujenzi na kubaini kuwepo kwa uhifadhi usioridhisha wa vifaa vya ujenzi ambavyo vimepokelewa kwa muda mrefu jambo ambalo huwenda likapelekea kuharibika vifaa hivyo kabla ya kuanza kutumika na hatimae kukisababishia Kikosi kutumia gharama za ziada kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vilivyoharibika na kupelekea kuingiza hasara Serikali na hatimae kupelekea kutokufikiwa kwa lengo lililokusudiwa.

**e) Kupitwa kwa muda kwa bidhaa kutokana na kutotumika kwa muda mrefu**

Ukaguzi ulitembelea maeneo ya Kikosi kwa Unguja na Pemba na kubaini kuwepo kwa vifaa vya ujenzi ambavyo vimepitwa na muda wa matumizi hali iliyosababishwa na kutotumika kwa wakati kwa vifaa hivyo.

Aidha, ukaguzi ulifanya mahojiano na Maafisa wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Kituo cha Kigunda na kubaini kuwepo kwa ujenzi uliosimama wa Ofisi za KZU ambapo vifaa vya ujenzi huo ikiwemo ndoo za rangi, gypsum boards, pamoja na vifaa vyenginevyo vikiwa vimemaliza muda wa matumizi kutokana na tarehe zilizobainishwa katika vifunganishio vyake, hii imetokana na kusimama kwa ujenzi wa kituo cha Kigunda Kanda ya Kaskazini Unguja kwa muda mrefu jambo ambalo litapelekea kutumika kwa gharama ya ziada pale ujenzi huo utakapoanza kwa awamu nyengine na kuisababishia hasara Serikali kwa kuibebesha mzigo wa matumizi ya fedha yasiyokuwa na tija.

Kutokana na dosari zilizoainishwa hapo juu ukaguzi umebaini dosari hizo zimesababishwa na uwepo wa vitendo vya uzembe wa kutokuzingatia miongozo na taratibu za ujenzi zinavyoelekeza na hatimae kupelekea upotevu wa fedha za umma kwa kununua vifaa kwa wingi kabla ya mahitaji ya matumizi ya vifaa hivyo na hasa ukizingatia vifaa hivyo vina muda maalum wa matumizi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kuongeza umakini katika usimamizi wa miradi ya maendeleo kwa kufanya matumizi kulingana na upatikanaji wa fedha pamoja na kununua vifaa kulingana na mahitaji wakati wa utekelezaji wa kazi husika ili kuepuka kujitokeza kwa kumalizika muda wa matumizi wa vifaa hivyo kabla ya mahitaji.

### 7.1.5.6 Upungufu wa vifaa vya kuzimia moto

Katika kutembelea miradi mbalimbali ya maendeleo pamoja na mali za Kikosi, ikiwa ni pamoja na zana za kuzimia moto, ukaguzi umebaini kuwa kikosi kina upungufu mkubwa wa vifaa vya kuzimia moto kama vile magari ya kuzimia moto, bwiza, water relay jambo ambalo linapelekea kikosi kushindwa kutekeleza dhamira yake ya kusogeza huduma karibu na jamii na kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ufanisi mkubwa.

Magari yaliyopo ni yenye ujazo wa lita 1500 za maji ambapo baada ya muda mfupi gari inashindwa kuendelea kutoa huduma kutokana na ukosefu wa maji, jambo ambalo linaondosha ufanisi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi.

Ukosefu wa vifaa vya kuzimia moto unaweza kupelekea kupunguza ufanisi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi katika kutekeleza majukumu yake pindipo majanga ya moto yanapotokezea.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kuhakikisha unaandaa bajeti maalum (ya dharura) inayohusiana na ununuzi wa magari na vifaa vya zimamoto vya kisasa na kuiwasilisha Serikalini kwa lengo la kupewa kipaombele cha haraka ili kunusuru utokeaji wa majanga ambayo hawatakuwa na uwezo wa kuyakabili kulingana na vifaa vilivyopo sasa. Mchanganuo wa magari hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 61:Hali halisi ya Magari katika vituo vya Zimamoto na Uokozi**

| Namba | Namba ya Gari | Aina ya Gari | Hali Halisi ya Gari |
|---|---|---|---|
| **Kituo cha Zimamoto Mjini** | | | |
| 1. | KZU 279 | Man | Nzuri |
| 2. | KZU 271 | Isuzu | Afadhali |
| 3. | KZU 238 | Fuso | |
| 4. | KZU 193 | Fuso | |
| 5. | KZU 236 | Rav 4 | |
| 6. | KZU 275 | Land Crusser | |
| **Kituo cha Zimamoto M/Kwerekwe** | | | |
| 1. | KZU 227 | Nissan | Afadhali |
| 2. | KZU 265 | Land Crusser (Pampa) | |
| **Kituo cha Zimamoto Bandarini** | | | |
| 1. | KZU 252 | Nissan | Afadhali |
| **Kituo cha Zimamoto Buyu** | | | |
| 1. | KZU 202 | Canter | Afadhali |
| 2. | KZU | Toyota Hilax | |
| **Kituo cha Zimamoto Uwanja wa Ndege Unguja** | | | |
| 1. | KZU | Nafco 01 | Afadhali |
| 2. | KZU | Nafco 02 | |
| 3. | KZU 256 | Noah | |
| 4. | KZU 262 | Ambulance | |
| **Kituo cha Zimamoto Kitogani** | | | |
| 1. | KZU 239 | Fuso | Afadhali |
| 2. | KZU 258 | Ashok | |
| 3. | KZU 266 | Land Crusser (Pampa) | |
| 4. | KZU 213 | Eveco | |
| 5. | KZU 277 | Navara | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Kituo cha Zimamoto Marumbi** | | | |
| 1. | KZU 194 | Fuso | Afadhali |
| **Kituo cha Zimamoto Mahonda** | | | |
| 1. | KZU 192 | Fuso | Afadhali |
| 2. | KZU 274 | Rav 4 | |
| **Kituo cha Zimamoto Kigunda** | | | |
| 1. | KZU 250 | Nissan | Afadhali |
| **Kituo cha Zimamoto Nungwi** | | | |
| 1. | KZU 231 | Fuso | Afadhali |
| **Ofisi ya Chanjaani Pemba** | | | |
| 1. | KZU 240 | Prado | Afadhali |
| 2. | KZU 219 | Rav 4 | |
| 3. | KZU 217 | Pickup | |
| 4. | KZU 223 | Issuzu | |
| 5. | KZU 218 | Canter | |
| 6. | KZU 195 | Tata | |
| **Kituo cha Zimamoto Chanjaani Pemba** | | | |
| 1. | KZU 248 | Nissan | Afadhali |
| 2. | KZU 246 | Issuzu | |
| 3. | KZU 261 | Pamper | |
| **Kituo cha Zimamoto Mkoani Pemba** | | | |
| 1. | KZU 260 | Isuzu | Afadhali |
| **Kituo cha Zimamoto Wete Pemba** | | | |
| 1. | KZU 233 | Fuso | Afadhali |
| **Kituo cha Zimamoto Kijichame Pemba** | | | |
| 1. | KZU 271 | Benz | Afadhali |
| **Kituo cha Zimamoto Uwanja wa Ndege Pemba** | | | |
| 1. | KZU 278 | Man | Nzuri |
| 2. | KZU 265 | Scania | |
| 3. | KZU 270 | Caravan | Afadhali |
| **Gari Mbovu** | | | |
| 1. | SMZ 3599 | Eveco | Mbovu |
| 2. | KZU 213 | Eveco | |
| 3. | SMZ 3603 | Ambulance | |
| 4. | | Ambulance | |
| 5. | | Toyota Hilax | |
| 6. | | Curmbas | |
| 7. | | Titano | |
| 8. | | Isuzu | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 9. | | Canter | Mbovu |
| 10. | | Canter | |
| 11. | | Toyota Rav A4 | |
| 12. | | Toyota Rav A5 | |
| 13. | | Ditroet | |
| 14 | | Tata | |
| 15. | | Fuso | |
| 16. | | Isuzu | |
| 17. | | Ditroet | |
| 18. | | Amarok | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Taarifa za Mali za Kikosi, 2023*

## KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU) PEMBA

### 7.1.5.7 Kufanya matumizi ya fedha za makusanyo ya mapato kinyume na utaratibu shilingi 10,200,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Pemba kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kimekusanya jumla ya shilingi 10,200,000 kutokana na vyanzo vyake mbali mbali vya mapato.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokuwepo kwa makadirio ya mapato pamoja na kutokuingizwa kwa mapato hayo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali jambo ambalo limepelekea Kikosi hicho kufanya matumizi ya mapato hayo bila ya kuwa na kibali kutoka Baraza la Mapinduzi.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa matumizi yasiyoridhisha ya fedha za Serikali, aidha ni kwenda kinyume na kanuni nambari 39(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Zimamoto na Uokozi Pemba kufuata taratibu, miongozo na sheria zilizowekwa ili kupata uhalali wa kutumia fedha wanazokusanya. Mchanganuo wa makusanyo na matumizi hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 62 : Makusanyo ya mapato yaliyotumiwa kinyume na taratibu**

| Namba | Muda wa Makusanyo | Kiasi cha Fedha Kilichokusanywa na Kutumika (Tsh.) |
|---|---|---|
| 1. | Ogasti, 2022. | 500,000 |
| 2. | Septemba, 2022. | 2,800,000 |
| 3. | Oktoba, 2022. | 500,000 |
| 4. | Novemba, 2022. | 600,000 |
| 5. | Disemba, 2022. | 600,000 |
| 6. | Januari, 2023. | 2,760,000 |
| 7. | Aprili, 2023. | 1,140,000 |
| 8. | Juni, 2023. | 1,300,000 |
| **Jumla** | | **10,200,000** |

*Chanzo: Daftari la Kukusanyia Mapato*

## 8.0 HITIMISHO

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 nilifanya ukaguzi kwa kuzingatia mifumo ya udhibiti wa ndani, taratibu za ununuzi, utayarishaji wa taarifa za fedha na nyaraka zilizoambatishwa kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizowekwa pamoja na kuzingatia viwango Kubalifu vya Kitaifa na Kimataifa vya Taasisi za Juu za hesabu zinazotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi za Juu za Ukaguzi ambazo zinahusu ukaguzi wa kisekta.

Nimetoa hati za ukaguzi kwa kuzingatia taarifa za fedha nilizozikagua na kuzitolea ripoti ya ukaguzi kwa kila taasisi ambayo niliikagua. Aidha, nilitoa barua ya ukaguzi (Management letter) zinazoonyesha dosari kwa kila Taasisi niliyoikagua na pale ambapo dosari hiyo ilikosa majibu na ushahidi sahihi ilichukuliwa na kubainishwa katika kitabu hichi kuwa ni dosari iliyokosa majibu.

Ni matumaini yangu kwamba watumiaji wa taarifa hii watanufaika na kujifunza kwa yale yote yaliyoelezwa na kubainishwa kwa uwazi ikiwemo Wakuu wa Taasisi kuweza kuyafanyia kazi na kufanya maboresho ili dosari hizo zisiweze kuendelea kujitokeza kwa mwaka ujao. Katika suala hili nitashukuru kama nitapokea maoni kutoka kwa watumiaji wa ripoti hii juu ya jinsi ya kuiboresha zaidi au kunipa miongozo ya namna ya kutanua wigo wa kazi zangu katika siku zijazo.

Nichukue fursa hii kwa dhati kumshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa jitihada zake anazoendelea kuzichukua kuijengea uwezo Afisi yangu katika utekelezaji wa majukumu yake ikiwemo kuboresha stahiki na maslahi ya watumishi, kunipa nguvu na kuniunga mkono wakati wa uwasilishaji wa taarifa zangu pamoja na

kuzitolea maelezo na maelekezo kwa Viongozi mbalimbali wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya namna ya kufanya maboresho ya dosari zinazobainika katika Taasisi zao.

Aidha, natoa shukurani zangu za dhati kwa viongozi wote wanaotenga muda wao kumshauri Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na kumuunga mkono na kumpa moyo katika harakati za kuliongoza Taifa hili na nia yake njema ya kulileteа maendeleo na mafanikio ikiwemo kuboresha maslahi ya mwananchi mmoja mmoja katika uibuaji wa miradi ya maendeleo yenye lengo la kukuza kipato na uchumi wa Nchi hii.

Mwisho kabisa niwashukuru wale wote waliojitokeza kuniunga mkono kwa namna moja au nyengine na kufanikisha upatikanaji wa taarifa hii bila ya kuwasahau Waandishi wa Habari kwa namna walivyojitoa kuitangaza na kuifikisha taarifa hii kwa kutumia vyombo vyao mbali mbali vya ndani na nje ya Nchi.